

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Nane – Tarehe 22 Aprili, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe.Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Aha! Kiongozi wa Upinzani amerejea kumbe! Mheshimiwa pole kwa safari ya Canada. Karibu tena! (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa muda wa sekunde moja, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kurudi salama. Spika wa Bunge la Canada anakupa salaam na nimempa ujumbe wa kumwalika, anasema atakuja Tanzania kabla hatujavunja Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu; Serikali mara nyingi hufanya manunuzi kwa kutumia Sheria ya *Procurement Act*. Lakini tumeshuhudia Serikali mara nyingi imefanya manunuzi na hatimaye Serikali huwa inarudishiwa chenji kama vile ya ununuzi wa rada. Ni sababu zipi zinazosababisha kufikia kiwango hiki cha Serikali mpaka kurudishiwa chenji, Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sina hakika kama nimemwelewa vizuri! Kurudishiwa nini?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Wakati tuliponunua rada, baada ya kutokea kashfa ndani yake, nilimsikia Waziri Membe akisema kwamba Serikali ya Tanzania imerudishiwa chenji na Serikali ya Uingereza baada ya kuonekana kwamba manunuzi yale hatukuyanunua kwa bei halisi. Sasa nasema, kwa nini Serikali hii mpaka inafikia pahala inarudishiwa chenji wakati iko *Procurement Act* inayotuongoza namna bora ya kufanya manunuzi ya Serikali kama vile ambavyo tulifanya kwenye Richmond hivyo hivyo, na kila pahala, manunuzi yameelezwa vizuri katika *Procurement Act*, lakini bado Serikali inanunua vitu kwa bei ya juu zaidi mpaka inafika pahala inarudishiwa chenji, ni sababu zipi za msingi?

**WAZIRI MKUU:** Labda nikiri kwamba mimi silijui hilo la kurudishiwa chenji. Lakini kama Serikali tunaendelea kuheshimu sana utaratibu wa kisheria uliopo na mara zote tumeutumia kwa kadri tulivyoweza. Lakini, kama ulikuwa na jambo mahsus, mimi nafikiri ningefurahi sana kupata jambo mahsus katika swali lako.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Aliyesema kwamba tumerudishiwa chenji ni Waziri wa Mambo ya Nje ambaye ni Waziri wa Serikali ambayo wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Msimamizi wa Serikali. Lakini, labda niseme kwamba kipindi kilichopita tulipitisha sheria hapa ya kuongeza nyongeza ya matumizi ya pesa ya *1.3 trillion shillings* kwa ajili ya kufidia wale waliopata matatizo katika kilimo na kutokana na mtikisiko wa uchumi. Kati ya pesa hizo, mpaka sasa ni kama shilingi bilioni 2.3 zimetumika, kwa hiyo bado vile vile Serikali imekuja Bungeni kuomba *1.7 trillion*, lakini pesa halisi zilizotumika siyo zile ambazo zimeombwa na Bunge, ni dhahiri kwamba kuna chenji nyininge imebaki ambayo Bunge hili halikuweza kuidhinisha. Ni kwa nini utaratibu huu wa makisio halisi ya Serikali wa kununua au kutoa fedha kulipa hayawi halisi kila siku Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**SPIKA:** Kwa mujibu wa Nyongeza ya Sita ya Kanuni zetu, swali linalofuata lazima liwe la nyongeza, lisiwe jipyka kabisa. Sasa suala la fedha tuliyopitisha ya kulipia athari za kiuchumi halihusiani hata kidogo na chenji. Kwa hiyo, tunaendelea Waheshimiwa!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wazee wa zamani walikuwa wanasema mwiba ukiapo ndipo utokeapo. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala lolote ambalo linahusu Mambo ya Muungano linapotaka kutoka au kuongezwa ni lazima ipatikane theluthi mbili ya Zanzibar na theluthi mbili ya Tanzania Bara ili jambo hilo lipate ufanisi. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 1969 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha suala la mafuta kuwa ni la Muungano, lakini katika Sherehe za Mapinduzi kule Pemba ambapo wewe ulikuwapo, tulimsikia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa.....

**SPIKA:** Mheshimiwa, nenda kwenye swali! Labda niwasomee tena, hizi Kanuni tunazitunga ili turahisishe mambo yetu hapa. Nyongeza ya Sita; Mwongozo kuhusu Maswali kwa Waziri Mkuu. Inasema: “Maswali kwa Waziri Mkuu yatakuwa ni ya papo kwa papo”. Ndiyo hiyo tunafanya. Kifungu cha (4) cha Nyongeza ya Sita kinasema: “Maswali na majibu katika kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu yawe mafupi”. Sasa ukianza dibaji ndefu sana, unawanyima fursa wengine kuuliza swali. Swali ni moja kwa moja kwenye swali! (*Makofi*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mwaka 1968 Bunge lilipitisha uamuzi kwamba suala la mafuta litakuwa ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, kauli iliyotolewa na Rais wa Zanzibar kule Pemba ambapo wewe ulikuwapo; kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Kikwete amekubali kuwa suala hili lisiwe la Muungano bila kurudisha katika Bunge hili Tukufu; unasemaje kuhusu suala hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Leo nadhani tuna tatizo kidogo. Ukimwuliza Waziri Mkuu atoe maoni kuhusu kauli ya Rais, humtendei haki! Kwa sababu Rais ndiye Mkubwa wake, ndiye aliyemteua. Sasa ukisema yeche na maoni gani kuhusu kitendo cha Rais, inakuwa ni kitu ambacho kina athari kubwa. Kwa hiyo, tunaendelea. (*Makofî*)

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ni wasimamizi wakuu wa majukumu katika vijiji na kwa kuwa utekelezaji wa mambo yote unawategemea wao, Kilimo kwanza wao, MKUKUTA wao na kadhalika. Lakini kwa muda mrefu wamekuwa hawana posho za uhakika za kuweza kujikimu; na kwa kuwa Wabunge tumeomba muda mrefu sana; na kwa kuwa sasa tunaingia katika mchakato wa Bajeti; Waziri Mkuu unasema nini juu ya viongozi hawa amba ni muhimu sana katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za nchi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Mpina kwa jambo hili jema. Ni kweli kabisa kwamba Serikali za Vijiji ndizo hasa zinatekeleza majukumu karibu yote ambayo Serikali imekabidhiwa. Kwa hiyo viongozi wake ni watu muhimu sana na wanastahili kuenziwa kwa namna mbalimbali. Lakini, kubwa la pili ni kwamba katika mfumo ulivyo sasa, tulishalisema, naomba nirudie tena kulisema. Tulishaelekeza kwamba katika fedha ya Serikali ya ruzuku inayorejeshwa kutokana na Serikali kuamua kuondoa baadhi ya vyanzo vya mapato, tulikwisheselekeza kwamba asilimia kama ilivyokuwa zamani itatolewa na kurejeshwa kwa Serikali za Vijiji na zitagawanywa kwa mpangilio ule ule uliokuwepo kabla hatujaondoa vyanzo vile vya mapato. Kwa hiyo, matumaini yangu ni kwamba Halmashauri makini ambazo zinathamini na kutambua umuhimu wa viongozi hawa zitakuwa zinatekeleza. Sasa kama kuna Halmashauri ambazo bado haziterkezei maelekezo hayo, bado tunazisihi zifanye hivyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Kwanza, nichukue nafasi tu kulaani kitendo cha walimu kuchapwa viboko katika Jimbo langu.

**SPIKA:** Mheshimiwa, halihusiani kabisa hilo! (*Kicheko*)

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Kwa kuwa, licha ya Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kutokuwa na posho yoyote, lakini bado kuna viongozi watendaji wa Serikali ambao wamekuwa kila tukio likitokea wanawakamata na kuwaweka ndani bila kutafuta ufumbuzi na kutumia taaluma yao kupeleleza na kuchunguza tatizo liko wapi. Huwakamata na kuwaweka ndani kwa visingizio kwamba wamechochea au wamefanya nini. Sasa, je, kwa kuwa Wenyeviti hawa baadaye hugundulika kwamba hawana hatia na wamedhalilika na wamefedheheshwa. Serikali inatoa fidia gani kwa viongozi hawa na wale waliowawekwa ndani kinyume cha utaratibu wanachukuliwa hatua gani?

**SPIKA:** Jamani, lazima nizilinde Kanuni, najua wengine mтанuna. Lakini, swal la msingi lilikuwa ni kulipwa posho kwa hawa Watendaji wa Vijiji na Wenyeviti. Swal la nyongeza linakuwa ni jinsi wanavyokamatwa na kuchapwa viboko. Kanuni zinasema, swal la nyongeza lazima liendane na swal la msingi; kuchapwa viboko na kulipwa posho wala havilingani. Kwa hiyo, tunaendelea Waheshimiwa.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kule Zanzibar kuna Taasisi moja ya Sayansi za Bahari (*Institute of Marine Sciences*) ambayo sasa ni miaka 10 tangu imeanzishwa kujengwa na ujenzi umeanza mwaka 2006. Lakini hivi sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, majengo hayo yametelekezwa na Mkandarasi amehama hata *site* ile ya ujenzi. Je, Serikali inasema nini kuhusu ujenzi wa *Institute* hii kama zinavyojengwa *Institute* nyingine nchini Tanzania?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimemwelewa sana ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji. Kama imetokea hivyo, ni *very unfortunate* kwa sababu Serikali inatakiwa kuwa makini sana katika mambo haya. Lakini, nimelisikia, nitalifanya kazi na baadaye nitakupa maelezo mazuri. (*Makofî*)

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mkoani Kigoma kuna kijiji ambacho kiko mpakani kabisa mwa Burundi na Tanzania, kijiji hicho ni kijiji cha Kagunga, kuna Kituo cha Polisi ambacho kina Polisi wanaume watupu, pale hakuna wanawake. Sasa, wakati akina mama wanapovuka mpaka kwenda Burundi huwa wanakaguliwa na askari wanaume.

Mheshimiwa Spika, ni lini wanawake hao watapatiwa askari mwanamke ambaye atakuwa anawakagua?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi nina hakika dada yangu Mheshimiwa Sijapata, angekuwa hata ameniambia jambo hili mapema, si ajabu tungekuwa tumeishapeleka polisi siku nyingi sana. Yaani kweli kungoja mpaka leo. Lakini hata hivyo nimekuelewa, nitamwambia Mheshimiwa Masha, nadhani tutapata mama wa kupeleka pale na aweze kufanya kazi iwe nyepesi zaidi.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa mwezi Oktoba mwaka huu ni mwezi wa uchaguzi; na tangu chaguzi za huko nyuma na naamini na chaguzi zitakazokuja, zimekuwa zinafanyika mapumziko Jumapili; na siku ya Jumapili kwa baadhi ya waumini ni siku ya ibada.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, huoni kwamba imefika wakati sasa ikateuliwa siku katikati ya wiki ikawa siku ya siku kuu kwa ajili ya uchaguzi kama zinavyofanya nchi zingine ili kuwapa fursa waumini wanaoabudu siku ya Jumapili waende wakaabu na wapate muda mrefu wa kupiga kura siku ambayo siyo siku ya ibada?

**SPIKA:** Mh! Leo, Alhaj Msambya unatetea...! (*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, hata mimi nimefurahi kweli, nikasema leo siku nzuri sana. Lakini, Mheshimiwa Spika, uamuzi ulifanywa kwa nia njema kabisa, hatukutaka kuvuruga siku za kazi kwa ajili ya jambo hili kwa kujuua kwamba tunayo siku ambayo ikitumiwa vizuri, inaweza ikawa zuri zaidi. Jumapili kweli ni siku ambayo baadhi ya madhehebu ya dini wanaitumia kwa ajili ya mambo ya sala na mambo mengine.

Lakini utaratibu ulivyo, uchaguzi unaanza, vituo vinafunguliwa tangu alfajiri, mapema sana na tunaendelea nao mpaka saa 10 jioni. Uko muda wa kutosha kabisa kwa Mtanzania ambaye anataka kweli kupiga kura kuweza kupiga kura. Sijaona kwamba inaingiliana kwa namna yoyote ile na mambo mengine ya kidini kwa sababu muda uliopo unatosha kabisa.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, juzi tarehe 19 Aprili, 2010, Bunge lako Tukufu liliridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Wabunge wote tulipitisha hapa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, baada ya pale, nilipata simu kutoka kwa viongozi wa chama na viongozi wa Serikali waishio katika Mikoa ya Mipakani hasa Mkoa wa Kilimanjaro, Kagera na Tanga, wakinihakikishia kwamba ardhi yetu ya mipakani imechukuliwa kwa kiasi kikubwa sana na wenzetu ambao wanaishi karibu na sisi. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Je, Serikali itachukua hatua gani ya dharura ya kufanya sensa na kwenda kuangalia kama kweli ardhi yetu ya mipakani imechukuliwa na wenzetu ili irudishwe mara moja?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Anne Kilango ametolea mfano wa Mkoa wa Kilimanjaro kama sehemu mojawapo ambayo inaweza kuwa imeathiriwa kwa kiasi hicho. Lakini, mimi najiuliza, ninavyojuua mimi Mkoa wa Kilimanjaro ndilo eneo ambalo wana matatizo makuwa sana ya ufinyu wa ardhi.

Kwa hiyo, kama kuna hali yoyote ya wageni kuchukua ardhi, ama itakuwa imefanywa na Watanzania wenyewe na haiwezi kuwa kwa namna nyingine yoyote kwamba kuna mabavu yametumika au njia nyingine za kifisadi zimetumika.

Kwa hiyo, nataka kwanza, nitoe wito kwa Watanzania kwamba ardhi ni mali, ni vizuri wakaendelea kutambua hilo na kwa kadri itakavyowezekana kuhakikisha wanailinda.

Lakini sisi tutachukua hatua za kufutilia kuona ni wapi na utaratibu gani umetumika kwa watu ambao siyo raia wa nchi hii kupata ardhi pamoja na Mkoa wa Kilimanjaro. Na mimi nitashukuru sana Mheshimiwa Kilango kama utaweza kunisiaidia nikajua ni maeneo yapi yaliyochukuliwa ili hatua ziweze kuchukuliwa haraka.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumbaku ina madhara makubwa ya afya na madhara mabaya sana ya afya kwa binadamu.

Nafikiri na hii ndiyo sababu Bunge letu Tukufu likapitisha Sheria ya Udhhibit wa tumbaku mwaka 2003 na pia likaridhia Mkataba wa Kimataifa wa *WHO* wa kudhibiti mazao ya tumbaku mwaka 2004.

Katika mkataba huo, pamja na mambo mengine, tunatakiwa tuondoe mabango ya sigara barabarani, tuongeze maonyo ya madhara ya afya kwenye paketi ya sigara, tuzuie watoto wasiende kununua sigara na kadhalika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni lini angalau basi mabango haya ambayo yanaonyesha utanashati wa sigara tutayaondoa katika miji yetu mikuu? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, zao la tumbaku ni zao la biashara kama mazao mengine mengi yalivyo. Zao la tumbaku kama yalivyo mazao mengine yanaweza kuwa na athari za kiafya. Kwa hiyo, tutaendelea kuhimiza yote mawili wale amba mnaona kuvuta sigara mnatambua itawaletea madhara mwendelee na msimamo huo, wale amba wanaona pamoja na jitihada zote za kutoa elimu wanaona bado ni lazima wavute sigara endeleeni kuvuta kwa sababu madhara yake mnayajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninachosema, Mheshimiwa Ali Tarab hapa ni kwamba sehemu kubwa ni uamuzi wa mtu mmoja mmoja (*individual*) kama ambavyo mnaambiwa msinywe pombe lakini mnakunywa pombe, msinywe makali mnakunywa makali, msinywe gongo mnakunywa gongo *what more do you want?* Serikali inajitahidi sana kwa hiyo, tutaendeleza hizi jitihada.

Mabango hayo unayosema kinachosemwa ni kwamba Bango lile pamoja na kutangaza weka onyo lakini sigara ina madhara ya afya na mimi nakuambia watu wanayajua na mimi nakumbuka kuzungumza na daktari mmoja na yeye alikuwa anavuta sigara sana (*chain Smoker*) nikamwuliza daktari, inakuwaje unavuta sigara nyingi hivyo. Akasema kuwa kuna sababu nyingi sana ambazo watu wanakufa; na huyo alikuwa ni daktari (*Kicheko*).

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika ninashukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni kufuatia utafiti wa Mwanaharakati mmoja anaitwa Msemakweli ilibainika kwamba kuna baadhi ya viongozi wa Serikali na Wanasiasa amba wana *degree fake*.

Lakini vilevile ikaonekana kwamba *TCU* ambacho ndiyo chombo kimeundwa kisheria kwa ajili ya kwenda kuvifanyia upembusi na kujua uhalali wake walikuwa wakiwaita hawa watu kwenda kuhalalisha yeti vyao, aliyejitokeza ni Mheshimiwa

Mathayo ambaye alikuwa *cleared* na Mheshimiwa Makongoro ambaye aliamua kwenda Mahakamani. Sasa kwa kuwa hili suala linahusu baadhi ya viongozi wa Serikali yako. Serikali imechukua hatua gani zozote binafsi za kuweza kujiridhisha uhalali wa hizo *degree*?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeeleweka nadhani.

**SPIKA:**Hata kama ungeeleweka wewe mwenyewe umesema suala hili liko Mahakamani. Na likiwa liko Mahakamani jibu lolote hata kama linamhusu kiongozi mwingine tutakuwa sisi Bunge tumeonyesha mwelekeo kama Serikali ikijibu hivyo tumeonyesha mwelekeo fulani ambao utakuwa siyo haki kwa hiyo, tunaendelea.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 15 Machi, 2010 gazeti la Serikali la Habari Leo liliandika habari kuhusu *Harambee* iliyofanyika Mkoa wa Kigoma ambayo iliongozwa na Mheshimiwa Celina Kombani Waziri aliyochangisha shilingi milioni 112. Sina tatizo na hilo. Tatizo langu liko pale niliposoma na kuona kwamba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma ilichangia shilingi milioni 7.5. Je, fedha hizi kwa Chama cha Mapinduzi. Je, fedha hizi zilitoka kwenye kifungu gani cha Bajeti cha mkoa huo. (*Makofi*).

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri nimemwelewa vizuri sana lakini kama gazeti lilisema tu kwamba kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kinachoweza kuwa kilifanyika ni Watumishi wa Mkoa ule katika ofisi hiyo kuchangishwa mchango ili kuchangia chama chao jambo ambalo halikatazwi hata kidogo lakini ungesema kwamba na hundi imetengenezwa ikaandikwa kutoka kwenye ofisi hiyo kwa maana kwamba fedha inayotokana na fedha za Serikali pengine ningelazimika kwenda hatua moja mbele zaidi.

Lakini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huwa inatokea na mara nyingi tunachangishwa, ni kama mimi ukisema ofisi ya Waziri Mkuu lakini nimewachangisha watumishi wangu kuchangia chama cho chote kile.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni ilipokuwa inafanywa mitihani ya kidato cha sita kuna baadhi ya shule hasa pale Dar es salaam walinyag'anywa vifaa vinavyowasaidia wanafunzi kufanya mitihani katika mitihani ya sayansi kama Hisabati na Kemia na Fizikia. Na vifaa hivyo ni *Calculator* ambayo sote tunaelewa kuna baadhi ya *Calculator* zinaruhusiwa baadhi ya shule waligomea wakaruhusiwa kurudia mitihani wengine hawakupewa fursa hiyo, katika mazingira haya Serikali inasemaje tutawatahini vipi wanafunzi huku ambao wengine wamepata fursa hii na wengine hawakupata?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba mimi nilikuwa silijui hilo lakini kwa kuwa, ni jambo linahusu sekta ya wizara yangu ya elimu nitamwomba Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe aliangalie tuone tatizo hasa lilikuwa ni nini, utaratibu hasa unasemaje na kama kuna baadhi walipewa fursa hiyo licha ya kwamba walitumia *Calculator* na wengine wakanyimwa na lenyewe

wataliangalia vilevile labda baadaye anaweza kuja kutoa kauli hapa kueleza kilitokea nini.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hali halisi inajionyesha kuwa wale *invigilators* wanaosimamia mitihani hii wengine kwa utashi wao tu binafsi wanakuwa hawaelewi kinachoendelea.

Wanachukua maamuzi kama haya ambayo kwa kweli ni ya kuidhalilisha Serikali kwa sababu Serikali iko *fair* sana katika mambo muhimu kama haya. Sasa unasemaje wakati si umefika sasa wa kufanya *Vetting* nzuri kwa hawa ma- *invigilator* wawe *at least* wana mwelekeo wa elimu na wanajua ni nini umuhimu wa vifaa hivyo katika mitihani?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema mimi kujidai mwamba hapa ni mtaalamu wa masuala yote pamoja na elimu nitakuwa sijitendei haki na wala sitendi haki kwa Watanzania. Profesa Jumanne Maghembe atalishughulikia ni yeze atatueleza taratibu hasa zikoje na ni kiwango gani hawa wasimamizi siku zile za mitihani wanapewa maelekezo yanayoeleweka na tutapata ufumbuzi wa tatizo hili na pengine ndiyo itakuwa njia rahisi ya kuwaambia Umma nini hasa utaratibu kuhusiana na mitihani hiyo.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa Serikali imetenga shilingi bilioni 22 na kuzikabidhi Benki ya Rasilimali ya Tanzania kwa ajili ya mikopo kwa wakulima. Lakini benki hiyo sharti lao mojawapo ni kwamba mkulima hawezi kupata mkopo mpaka awe amechangia asilimia kumi ambayo ni sawasawa kwa bei ya sasa ya trekta ni sawa sawa na shilingi milioni kumi wakati benki ya Kigeni ambayo iko Tanzania ya *Federal Bank of the Middle East* inatoa asilimia tano ambayo ni sawaswa na shilingi milioni tano.

Je, hauoni sasa ni wakati muafaka wa kutoa nafuu zaidi kwa wakulima wetu kupitia hili dirisha la kilimo? (*Makofit*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, rai ya Ndugu yangu Dr. Juma Ngasongwa nadhani ni nzuri tu lakini nadhani tulipokuwa tumekaa na kulitazama jambo hili tulijaribu kuangalia mambo mengi na hatimaye tukafikia uamuzi ambao tulidhani katika mazingira tulio nayo unaweza kuwa ni mzuri zaidi.

Lakini hili jambo linaweza kuzungumzwa tukaona kama bado tunaweza tukashuka chini zaidi maana hatuelewi benki hiyo nyingine misingi yake ikoje ya mtaji wake ambayo imeweza kufikia kiasi hicho cha chini, rai ni nzuri lakini tutaangalia tuone kama tunaweza.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kutekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani katika mauzo ya korosho Wilaya ya Tandahimba hivi sasa

wakulima wake wameanza kulipwa malipo ya tatu maarufu kama *bonus*. Malipo hayo yamejaa malalamiko na kero kubwa kiasi cha wakulima kuziba barabara kwa magogo na mawe na kufanya viongozi wa vyama vy a msingi kufungiwa kwenye magodauni na hii inatokana na .....

**SPIKA:** Nenda kwenye Swal Mheshimiwa siyo maelezo mafuru.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, nimalizie hilo ili Mheshimiwa apate *concept* yangu kidogo. Hii inatokana na viongozi wa Chama cha Ushirika TANECU kuwakata wakulima kwa maelezo kuwa wanafidia fedha kutohakana na kesi kati yao na LIBER VALLEY ambayo mkulima hahusiki. Mko a umejitahidi lakini kuna dalili kwamba inaonekana kuna kushindwa, kama kiongozi wa Serikali unatoa kauli gani kumaliza kero na malalamiko kwa sababu wanaathirika watu ambao hawahusiki kwenye mabarabara yale. (*Makofit*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri nilifanya ziara Mko a wa Lindi na Mtwara. Kwanza nachukua nafasi hii kuwapongeza sana ndugu zangu wakulima wa Mtwara kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya katika kuendeleza kilimo cha korosho kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana. Lakini pili nilitaka vilevile nitumie nafasi hii kuwapongezeni sana kwa ujumla mfumo wa stakabadhi ghalani katika Mko a wa Mtwara umekuwa na mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizozipata nilipokuwa pale zilinitia moyo na tutaendelea kutumia mfumo kama mfano kwa upande wa Mko a wa Mtwara.

Lakini tatu nilipokuwa pale lipo jambo vilevile ambalo nilijifunza ukiondoa hili ambalo amenieleza Mheshimiwa Njwayo kwamba utaratibu wa kufanya makisio ya gharama ambazo zinatakiwa kwenda kwenye Vyama vy a Ushirika kwa maoni yangu nilipopitia ile orodha nilisema makato yale yalikuwa na riba kubwa sana, ambayo yangeweza kutazamwa tukapunguza zile gharama kwa kiasi kikubwa ili kumwezesha mkulima kupata zaidi kuliko anavyopata hivi leo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani jambo kubwa hapa ni kuendelea kusihi Mko a sababu nilitoa maagizo haya kwamba wakae chini watazame hizi gharama nyingine ambazo zimeingizwa chini ya visingizio mbalimbali kama unyaufu, mara sijui nini kuna vitu vingi sana pale vingine ambavyo unaona kabisa kwamba hapa si sahihi.

Kwa hiyo, nitachukua hatua kwa kuzungumza na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara nadhani tutaelewana hata hilo ulilonieleza tutalifanya ni sehemu ya jambo hili ili tuweze kuyamaliza ili wale wakulima wasikate tamaa. Wameshafika mahali pa kutia moyo, na ni vizuri tukaendelea kuwatia moyo. Nakuomba sana univumilie kidogo nitalifanya kazi na nitakupa maelezo ya uhakika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge huo ndiyo mwisho wa kipindi cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunamshukuru sana nina hakika mtakubaliana nami katika kazi hiyo hiki kipindi cha maswali kwake ni moja ya vipindi vigumu sana kwa binadamu yoyote kwa sababu haji amejiandaa hajui kuna mtu atauliza kuhusu korosho na nini, lakini basi tunashukuru sana Mungu amempa kipaji cha kuweza kujibu maswali vizuri sana.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 95

#### **Malimbikizo ya Mishahara ya Walimu**

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO** aliuza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kuwalipa walimu malimbikizo ya Mishahara yao ya miezi kumi na tano (15), na kwa kuwa, walimu walioko Manispaa ya Singida mkataba wao unaisha Oktoba 2009 kabla ya kulipwa.

Je, Serikali haioni kuwa kutolipa walimu hawa wastaafu mishahara ya miezi kumi na tano (15) ni kinyume na Utawala Bora?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti maalum , kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la kuchelewa kwa malipo ya madai ya malimbikizo ya mishahara ya walimu wastaafu waliokuwa wanafundisha kwa mkataba katika Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, walimu waliokuwa kwenye mkataba wengi wao walichelewa kuingizwa katika orodha ya malipo ya mishahara kutokana na kuchelewa kuwasilishwa kumbukumbu zao Wizarani.

Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa madai ya walimu wastaa fu wa Mkoa wa Singida yameshawasilishwa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa ajili ya malipo. Aidha malipo yatafanywa kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namshurukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mahiza ni mionganini mwa Manaibu Waziri wenyewe uwezo wa juu katika utendaji wa kazi. Na kwa kuwa, madai haya ya walimu ambayo ninaulizia leo kwa mara ya nne yalipelekewa taarifa ya maombi Wizarani mara nne, mara tatu kwa njia ya posta, mara ya nne Afisa Elimu wa Mkoa alipelekwa kwa mkono wake na kumkabidhi Afisa Bakar Issa wa kitengo cha ualimu toka mwaka jana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa uwezo wake hajui kwamba kuna kila sababu za uzembe ofisini kwake yuko tayari kufuatilia kuona uzembe huu nani kaufanya ili aweze kumwajibisha na kuondoa dosariambazo Chama cha Mapinduzi kina chafuliwa?

Mheshimiwa Spika, swalii la Pili, kwa kuwa, Serikali ya CCM haina umasikini wa kushindwa kulipa walimu wanane kwa muda wote huu. Je, kuna sababu gani ya kusubiri mpaka miezi yote hiyo, mpaka mwisho wa mwezi wa sita au wa saba huko kwa nini suala hili ambalo limeshakuwa kero likatekelezwa mara moja ukizingatia kati ya watu wanane hawa mwalimu mmoja amekwisha fariki ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, madai ya walimu hawa ni dahahiri yalipelekwa mahala pasipo husika. Bwana Bakari Issa ni mtumishi katika Idara ya ualimu madai haya yalipaswa kupeleka kwa Afisa Utumishi Mkuu wa Wizara. Kwa maana hiyo yalipotea na ndiyo maana baada ya kuuliza kwako mara kadhaa Mheshimiwa tumefanya kila tunachowenza, tumefuatilia na tulibaini orodha yote ya mafaili yale yalipelekwa mengine TAMISEMI, wakati mengine yakapelekwa Utumishi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, hatimaye kwa pamoja Wizara zote tatu tumekubaliana madai hayo sasa yamewasilishwa Hazina. Suala la kwamba CCM haina umasikini wa kushindwa kulipa ni sawa ni kweli lakini tunapokuja katika kanuni na Sheria za Kiutumishi Chama kitazielekeza Serikali zake kuhakikisha wajibu unatimizwa. Ndiyo maana tumemwahidi tutawalipa kabla ya mwaka huu wa fedha. Kwa mwalimua mbaye tayari ameshatangulia mbele ya haki tunatoa pole kwa familia na kwamba taratibu za mirathi zitakapofanywa haki yake itapatikana. (*Makofî*)

Na. 96

#### **Vigezo Vya Ugawaji Fedha za Matumizi ya Kawaida**

**MHE. YOB YUSTINO NDUGAI** aliuliza:-

(a) Je, mgao wa fedha za Matumizi ya Kawaida (OC) kwa Vyuo Vikuu vya Umma unafanywa kwa kuzingatia vigezo gani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha za matumizi za kawaida katika Vyuo Vikuu vya Umma, huzingatia vigezo vifuatavyo:-

(i) Aina ya programu inayotolewa na chuo husika. Mfano, gharama za uendeshaji wa programu za masomo ya sayansi ni za juu kuliko zile za programu za masomo ya sanaa;

(ii) Idadi ya wanafunzi katika chuo husika;

(iii) Mfumo wa utoaji wa elimu na gharama za uendeshaji wa Vyuo Vikuu Huria ni tofauti na vyuo vingine;

(iv) Mpango Mkakati wa Chuo Kikuu husika na bajeti inayowasilishwa kutoka vyuoni; na

(v) Uwezo wa kiuchumi wa Serikali unaoamua ukomo wa bajeti katika mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mgawo wa fedha unaotolewa na Serikali kwa Vyuo Vikuu vya Umma, hupata mapato ya ndani kwa miradi mbalimbali inayotekelizwa. Mathalani upo mradi wa maendeleo wa kuboresha sayansi na teknolojia katika Vyuo Vikuu wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100. Aidha, wadau wengine wa maendeleo wanatoa misaada katika kuboresha taaluma, tafiti na huduma.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri na nitamuuliza swalii moja tu la nyongeza. Kabla ya swalii hilo la nyongeza, ni-*declare interest* kwamba, mimi ni Mwakilishi wa Bunge hili katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma ni moja ya Vyuo vinavyokua kwa haraka sana nchini, sasa hivi tuna wanafunzi 19,000 na 1,000 wata-*graduate* Novemba mwaka huu, watabaki 18,000. Oktoba mwaka huu tutadahili wanafunzi 10,000 kwa wakati mmoja, kwa hiyo, tutakuwa na wanafunzi 28,000 by November mwaka 2010. Lakini *OC* ambayo inatolewa kwa Chuo Kikuu cha Dodoma ni karibu sawasawa au chini ya *OC* wanayopewa Chuo cha Ardhi, ambao wana wanafunzi kama 3,000.

Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba jambo hili linahitaji kuangaliwa vizuri ili Chuo hiki kipewe fursa ambayo kinastahili? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza kwa kuwa Mwakilishi wa Bunge ndani ya Chuo cha Dodoma. Suala la *OC* ni suala ambalo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pekee haiwezi kulitatua. *OC* inayogawiwa hutokea Hazina, kwa hiyo, kadiri inavyopatikana ndivyo nasi tunavyogawana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niseme tu, Serikali inatambua kukua kwa haraka kwa Chuo Kikuu cha Dodoma, vivyo hivyo na Vyuo Vikuu vingine.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie kile kidogo tunachokipata na kikubwa kikipatikana tutaongezeeana. (*Makofî*)

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu elimu ya juu ni suala la Muungano na kwa sababu Zanzibar pia inacho Chuo Kikuu cha Umma kimoja ambacho kimeanzishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; je, katika mgawo huu wa fedha kwa matumizi ya Vyuo Vikuu vya Umma Chuo hicho kimepata kiasi gani kutoka Mfuko wa Wizara inayosughulikia Elimu ya Juu kutoka Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, Chuo anachokizungumzia Mheshimiwa Mbunge kipo Zanzibara chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa maana hiyo ruzuku yao wataipata kupitia kule. (*Makofî*)

Na. 97

### **Misururu Mirefu Katika Mabenki**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa mashine za kutolea pesa katika Mabenki (*ATM*) zimekuwa zinaharibika mara kwa mara na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa mashine hizo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa dhati wa kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, baadhi ya wakati mashine za benki zinazotumika kutoa pesa (*ATM*), zinakuwa na matatizo na hivyo kuleta usumbufu kwa wateja. Matatizo ya *ATM* yanatokana zaidi na Kukatika kwa umeme hivyo kupelekeea kutokuwepo kwa mfumo wa mawasiliano kwa muda. Vile vile, baadhi ya wakati benki hulazimika kukatisha huduma za mashine za *ATM* kutokana na mashine hizo kuishiwa fedha.

Hata hivyo, Serikali kupitia Benki Kuu imeshalionna tatizo hili na Benki Kuu tayari imeanzisha mchakato wa kuwa na mfumo mmoja wa malipo ya *ATM* (*National Switch*), ambao utatoa fursa kwa mteja mwenye kadi ya *ATM* kutumia mashine ya *ATM* ya Benki yoyote nchini, bila kulazimika kutumia mashine ya *ATM* ya Benki yake tu. Mpango huu utakapokamilika, utaondosha kabisa usumbufu unaojitokeza.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, uharibifu unaozungumziwa kwenye suala hili siyo uharibifu ambao unasababishwa na umeme wala benki kusitisha huduma kwa ajili ya kuweka hela; ni ule wa mwananchi kusafiri kutoka nyumbani kufika kwenye *ATM* anaambiwa *ATM* imeharibika, anapanda *bus* anakwenda kituo kingine anaambiwa *ATM* imeharibika, kwa hiyo, siku nzima anazunguka akitafuta huduma ya fedha asipate.

Mheshimiwa Spika, kama ni siku ya *week end* au siku ya sikukuu, basi kama amepata dharura inakuwa ni tatizo kubwa sana.

Kwa kuwa *ATM* nyingi zinazoingizwa ndani ya nchi ni mbovu, ambazo zimepitwa na wakati na zilishatumika hata nchi za nje zikaonekana kwamba hazifai tena; hili lilithibitishwa na Naibu Waziri wa Fedha alipoongea na vyombo vyta Habari siku ya tarehe 7 Oktoba 2009, alisema mwenyewe kwamba, *ATM* nyingi ni mbovu na zinakuwa hazifanyi kazi:-

(a) Kwa nini Serikali inaruhusu *ATM* mbovu kuingia ndani ya nchi ambazo hazina tija? (*Makofi*)

(b) Ili kuweza kuondoa tatizo hili kwa wananchi; kwa kuwa wengi wamehamasika na wameingia benki na wanataka huduma kupitia *ATM*; Serikali iko tayari sasa kuhakikisha kwamba *ATM* zinazoingia ndani ya nchi ni za kisasa ili kuhakikisha kwamba wananchi wanakidhi mahitaji yao kwa wakati? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba, baadhi ya wakati tunapokwenda kuangalia au tunapotaka kwenda kutoa fedha kupitia hizi mashine za

*ATM*, tukiona imeandika *out of service; not necessarily* kwamba ile mashine ni mbovu; ile mashine baadhi ya wakati huwa haina fedha na fedha hizi haziwekwi kila zinapomalizika; kuna *time period*.

Mheshimiwa Spika, katika mashine hizi kuna *cassette* tano, zinatia *denomination* zote, ina *capacity* ya milioni ishirini; inapotekea wateja wakawa wengi ile hela inakwisha mapema zaidi inabidi usubiri mpaka muda wake unapofika ndiyo waweze *ku-replace*, siyo kila wakati wana-*replace* hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Sakaya kwamba, kweli baadhi ya hizi mashine zilikuwa mbovu, lakini tayari tumeshaongea na mabenki haya kwamba, waingize mashine mpya na tayari benki nyingi sasa hivi wameleta mashine mpya na hizo zilizopo nyingi ni mpya.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Sakaya avute subira, tatizo hili litatatuka pale ambapo tutakuwa tuna mtandao wa pamoja. Kama una *ATM* ya *NMB* hulazimiki kutoa pesa kwenye Benki ya *NMB*, utakwenda *CRDB*, utakwenda kwenye benki yoyote ile utatoa pesa na utatumia. Ahsante sana.

**MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, katika mashine za *ATM* imeandikwa kwamba, huduma saa 24, nimemsikia Mheshimiwa Mkuchika akiwa mkali sana juu ya muda; mkataba ni wa pande mbili na unapaswa kutekelezwa kama ulivyowekwa, watu wengi wanatumia *ATM* wakisafiri kwa sababu za kiusalamu wasitembee na hela, watu wengi wanakwenda benki wakati wana wagonjwa wakitegemea watapata huduma saa 24:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuwasaidia Watanzania wanaoathirika kwa sababu mkataba huu unavunjwa hasa kwa zile benki ambazo zinafanya hivyo na tumezipgia kelele mara nyingi kama vile *NBC* ambazo mashine zake zimeonekana mara nyingi ni mbovu au hazina hela? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeche kwamba, tumeandika kwenye *ATM* huduma ni saa 24, lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Dokta Slaa, Serikali imeliona hili kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi na ili kutatua tatizo hili, tuna *solution* mbili tu.

Mheshimiwa Spika, *solution* ya kwanza itakuwa ni *very expensive*; ni gharama kwa benki kwa sababu itabidi tubadilishe hizi mashine badala ya kuja na kaseti ambazo zinatoa *capacity* ya milioni 20, zije na kaseti ambazo zina *capacity* kubwa sana. *Solution* ya pili ni ile niliyoisema kwamba, tutaunganisha mitandao ya benki zote, utakuwa hulazimiki tena wewe kwenda kwenye benki yako, utakwenda benki yoyote ile na utatoa hela, wao wenyewe mabenki watafanya *reconciliation*.

Mhehsimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Slaa avute subira, tunakwenda huko. (*Makofi*)

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Je, ni lini *ATM* hizo zitakuwa nyingi? Sambamba na uharibifu wa mara kwa mara kwa mashine hizo za *ATM*, lakini kuna usumbufu mkubwa wa wananchi kusimama kwa muda mrefu pale kwenye *ATM* kutokana na uchache wa mashine hizo hasa hapa Dodoma, mtu anaweza akatoka asubuhi mpaka saa saba hajarudi nyumbani; je, Serikali inalichukulia hatua gani ya haraka suala hilo ili kuongeza *ATM* sehemu mbalimbali hasa hapa Dodoma? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hoja hapa ya Wabunge kwa niaba ya Wananchi wanachosema ni kwamba, *ATM* hizi ni za viwango vya chini na zinatumia teknolojia ya zamani na Serikali ina wajibu kwa wananchi wa kuhakikisha tunapata huduma bora; hebu lenga hapa. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali lako na swali la Mheshimiwa Faida kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Mimi sikuuliza swali bali nilifafanua tu, nina wajibu wa kufafanua mambo yake vizuri. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane na wewe kwamba, tukirudi nyuma miaka kumi, kumi na tano iliyopita, hatukuwa na *ATM* Tanzania, tunakwenda huko na jitihada tutafanya ili tuwe na *ATM* ambazo zitakuwa ni bora zaidi ili ziweze kuhudumia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kujibu swali la Mheshimiwa Faida nataka nimwambie tu kwamba, kwa upande wa Dodoma, wananchi wengi wameweka fedha zao kupitia Benki ya *NMB* na wachache wameweka kupitia *CRDB* na wachache zaidi wameweka fedha zao kupitia Benki ya *Barclays*, ukitembea kwenye Benki ya *Barclays* hakuna foleni unachukua unaweka unaondoka. Tufanye mambo mawili; kwanza, tutawashawishi *NMB* waongoze *ATM machine* kwa upande wa Dodoma, lakini vile vile tutawashawishi wananchi wengine ambao bado hawajafungua akaunti, wafungue kupitia haya mabenki mengine. (*Kicheko*)

Na. 98

#### **Mji wa Gairo Kupatiwa Maji Safi na Salama**

**MHE. AHMED M. SHABIBY** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya Mwaka 2008/2009 Serikali iliahidi kuipatia maji safi na salama miji tisa ikiwa ni pamoja na Mji wa Gairo:-

- (a) Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia wapi?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa sasa inahitajika jitihada za makusudi ili kutekeleza ahadi hiyo ambayo pia ilitolewa na Mheshimiwa Rais?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Shabiby, lenye sehemu (a) na (b), yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Gairo ni mionganoni mwa Miji tisa iliyochaguliwa kusanifiwa na kujengewa miradi ya maji chini ya ufadhilli wa Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo ya (*AFD*). Miji mingine ni Utete, Mpwapwa, Kibiti, Ikwiriri, Kilosa, Mvomero, Turiani na Kibaigwa. Wakati wa usanifu, msaada wa fedha ulitolewa na kazi zilifanyika katika Miji yote tisa ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Usanifu wa miundombinu ya maji na uandaaji wa vitabu vyta zabuni.
- (ii) Kufanya mapitio na kutoa mapendekezo ya kisheria kuhusu vyombo vyta uendeshaji baada ya ujenzi wa miradi kukamilika.
- (iii) Uchimbaji wa visima vyta utafiti/majaribio.

Mheshimiwa Spika, baada ya usanifu kukamilika na gharama za awali za ujenzi kujulikana, ilibainika kuwa fedha iliyotengwa haitoshi kutekeleza miradi ya maji katika miji yote tisa. Hivyo, kulingana na kiasi cha fedha na kazi zilizotarajiwa kufanywa kwa Miji hiyo, Miji ya Utete na Mpwapwa ilichaguliwa kutekelezwa na ujenzi wa miradi ya maji kuanza mwezi Januari, 2009. Kwa sasa ujenzi huo uko katika hatua za mwisho. Serikali ya Tanzania iliamua miradi ya maji saba iliyobaki ikiwa ni pamoja na Gairo, itekelezwe kwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*).

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuchukua jukumu la kutekeleza Mradi wa Gairo, ilitangaza zabuni ya kutafuta mkandarasi wa kujenga mradi. Nafurahi kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na wakazi wa Mji wa Gairo kwamba, mchakato wa kumpata mkandarasi sasa umefikia hatua ya kupata idhini ya Benki ya Dunia ya kusaini mkataba wa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafuatilia kwa karibu na Benki ya Dunia na matarajio yangu ni kwamba, ifikapo mwezi Juni, 2010 kazi ya ujenzi inaweza kuanza.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa vile Naibu Waziri amejibu kwamba mchakato wa kumpata mkandarasi upo na hapo hapo amejibu kwamba tayari ameshapata idhini ya kusaini mkataba wa ujenzi; hapo sijaelewa; je, mkandarasi ameshapatikana kwa sababu kama hajapatikana huyu Benki ya Dunia atasaini na nani; na kama amepatikana ni nani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda nifafanue swali la nyongeza la Mheshimiwa Shabiby kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zipo hatua mbalimbali katika kupata idhini, hatua tulioifika ni kwamba, mkandarasi yule amekwishapatikana na akishapatikana utaratibu wa kupitia makabrasha yale unakamilika, lakini ukishafikia hatua ya mwisho kabisa, unapelekwa tena Benki ya Dunia kupata ridhaa ya mwisho. Kwa hiyo, hapo ndipo tulipo sasa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimetaa matumaini kwamba, baada ya mkandarasi kusatikana, kilichobakia ni Benki ya Dunia kupitia yale yote ambayo yamekubaliwa na kusema basi tieni sahihi na endeleeni na kazi; siyo kwamba tunaanza mchakato upya.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la upatikanaji wa maji safi na maji salama katika Mji wa Gairo linafanana kabisa na upatikanaji wa maji safi katika Jiji letu la Dar es Salaam; na kwa kuwa katika Ripoti ya *REPOA* inaonesha kwamba asilimia 31 ya matumizi ya maji majumbani bado ni machafu na asilimia saba tu kutokana na taarifa ya *DAWASCO* Wakazi wa Dare es Salaam ndiyo wanaopata huduma ya majitaka; na kwa kuwa kwa kutopata huduma ya maji safi na salama ya kunywa kumeuongezea Mji wa Dar es Salaam kupata magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu; je, ni lini Serikali sasa itawapatia Wakazi wa Dar es Salaam maji safi na salama ya kunywa? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimuweke sawa Mheshimiwa Lucy Owenya kwamba, taarifa sahihi au taarifa ambazo tunazitumia ni taarifa zinazotolewa na Serikali. Upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, taarifa zetu zinaonesha kwamba wastani ni wa asilimia 68. Sasa kuhusu upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, tumekuwa tukieleza hapa kwamba ni kweli kwamba, hatujaweza kuwapatia maji wananchi wote wa Jiji la Dar es Salaam kama tulivyokuwa tumepanga. Tumeweka mipango mahususi, mipango mikubwa kabisa kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Sasa hivi uzalishaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam ni takriban mita za ujazo 270,000 ukilinganisha na mahitaji ya 450,000. Sasa ili kuziba pengo hili, Serikali imechukua hatua mbalimbali ambazo tumekuwa tukizieleza, ikiwa ni pamoja na kukarabati vituo vyetu mbalimbali vya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Zaidi ya hapo, tumefanya utaratibu wa kutafuta maji chini ya ardhi, mradi ambao hivi sasa tumeanza kuutekeleza.

Vilevile tumeona kwamba, ipo haja ya kuongeza maji kwa kujenga Bwawa la Kidunda. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Lucy Owenya awe subira, mipango yote ambayo tayari sasa inatekelezwa, malengo ni kuziba pengo hilo la upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na nina hakika muda si mrefu, tutakuwa tayari tumeanza kutekeleza miradi yote hii.

**SPIKA:** Kwa swalii ambalo ni refu sana na nina hakika majibu nayo mafuru sana, Mheshimiwa Jackson Makwetta.

Na. 99

### **Kukauka kwa Bwawa la Lihogosa Njombe**

#### **MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa Bwawa la Lihogosa lililoko karibu na Mji wa Njombe limeanza kukauka kutokana na uamuza wa Kampuni ya Chai (Luponde) kutumia maji ya Bwawa hili kumwagilia chai na kusababisha kufa kwa samaki, wadudu na mimea yenye faida kwa binadamu; na kwa kuwa pia kina cha maji katika Mto Mtifaru, Chamakale na Champoma kimepungua na kuathiri kilimo cha bustani kandokando ya mito hiyo:-

(a) Je, Serikali inayo taarifa juu ya madhara hayo; kama ndiyo ni kwa nini haichukui hatua za kuzuia madhara hayo yasiendelee kutokea?

(b) Kama Serikali haina taarifa ya madhara hayo; kwa nini isipeleke mabingwa wa mazingira ili kujua ukweli wa mambo na kupata ushauri wa kitaalamu ikiwa ni pamoja na kuzuia umwagiliaji wa chai kwa kutumia maji ya Bwawa hilo?

(c) Je, Serikali haioni kuwa kupungua kwa maji katika Bwawa hili kumeathiri kwa kiasi kikubwa kilimo cha vinyungu katika Vijiji vya Lusisi, Mhadzi na Igima na hivyo kuwapunguzia kipato wakazi hao, pamoja na madhara ya ongezeko la joto la juu?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kweli swalii la Mheshimiwa Makwetta ni refu na mimi nimejitahidi kulifupisha.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Jimbo la Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Lihogosa liliengwa mwaka 1958 na Kampuni ya Kubangu Miwati ya TANWAT iliyoko katika Wilaya ya Njombe, kwa ajili ya maji ya nyumbani, umwagiliaji na mifugo. Kampuni ya Chai ya Kibena ilipoanza kumiliki mashamba ya chai, ilipewa hati zenye kiasi cha maji mita za ujazo 13,254.678 kwa siku.

Pia *TANWAT* ilihamisha hati ya kutumia maji mita za ujazo 2,460.53 kwa siku kwenda kwa Kampuni ya Chai ya Kibena.

Mheshimiwa Spika, nimemwagiza Afisa wa Bonde la Mto Rufiji kukagua hati zote za kutumia maji ya Bwawa la Lihogosa na Bonde zima la Mto Rufiji na kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Serikali imebaini upungufu wa maji katika Bwawa la Lihogosa kuwa unatokana mambo yafuatayo:-

- (i) Kiasi cha maji kinachohifadhiwa katika Bwawa kimepungua kutokana na udongo uliojaa bwawani.
- (ii) Mahitaji ya maji sasa ni makubwa kuliko uwezo wa bwawa.

Tarehe 8 Januari, 2009 wataalam kutoka Ofisi ya Bonde la Mto Rufiji walikagua mashamba ya chai ya Kampuni ya Kibena na kugundua kwamba, Kampuni ya Chai ya Kibena imekwishaanza kuchukua tahadhari kwa kuanzisha teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone (*drip irrigation*) ili kuongeza tija katika matumizi ya maji. Nawapongeza sana kwa hatua hiyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, ili kurekebisha kasoro zinazojitokeza, Wizara yangu imechukua hatua zifuatazo:-

- (i) Kuunda Jumuiya ya Watumia Maji ya Mbumitilu inayojumuisha Vijiji vya Mbukwa, Mititafu na Lumbidzi.
- (ii) Kuweka alama za mipaka kuzunguka Bwawa la Lihogosa.
- (iii) Kutoa elimu ya mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji kwa wananchi na Kampuni ya Chai ya Kibena.

Mheshimiwa Spika, kinachoonekana hapa ni mgongano wa matumizi ya maji kati ya wakulima wakubwa wa Kilimo cha Chai, yaani wawekezaji na wakulima wadogo. Makundi yote mawili yanatumia maji yanayotokana na ardhi oevu katika *catchment area* ndogo inayopeleka maji katika Bonde la Mto Kilombero.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itafanya uchunguzi wa kina kuhusu upungufu wa maji katika eneo hilo kwa kuhusisha wadau mbalimbali wakiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Mazingira (*NEMC*), Chuo Kikuu Kikuu SUA, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na wadau wengine ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo kwa lengo la kuendesha kilimo cha kibiashara na kuimarisha usalama wa chakula kwa faida ya taifa zima. (*Makofi*)

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, swali lilikuwa refu kwa sababu ya uzito wa jambo lenyewe. Kwanza, nashukuru kwa hatua zinazochukuliwa, lakini naomba afanye marekebisho.

(a) Bwawa halikujengwa mwaka 1958 kama alivyosema, kwa sababu kabla ya hapo hapakuwa na bwawa, tumeanza kulijenga mwaka 1978.

(b) Kamati hiyo aliyoienda siyo vijiji vinavyozunguka hili bwawa, viko nje ya bwawa. Mimi nashangaa kwa nini kamati ambazo hazihusiani na bwawa ziundwe!

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

Sijui wanatafuta nini kwa sababu tangu mwanzo wa *project* hii ya chai, watalaan wa mazingira walikutana na wakashauri kwamba haifai kwa sababu *source* ya maji kwa bwawa hili ni mvua na siyo vijito na mmoja wa watu walioshiriki ni Profesa Mwalyosi, ambaye yupo hapa.

Sasa nasema tukikiuka misingi, misingi itatukiuka. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba, kama ni lazima tena kuendelea na Kamati wakati majibu na mapendekezo yako wazi, basi na mimi ni mdau kwa sababu natoka kijiji kimojawapo katika vijiji vinavyozunguka bwawa.

**SPIKA:** Swali tafadhalii. Alaa, ndiyo umemaliza hivyo. Ilikuwa hotuba hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Makwetta, kwa kuendelea kufuutilia suala hili la mazingira na pia Mheshimiwa Profesa Mwalyosi. Haya aliyojasema Mheshimiwa Makwetta kuhusu mwaka ambaa bwawa liliengwa na vile vijiji, namhakikishia kwamba, tutajaribu kuangalia tena kama kweli vijiji vile vilivyoandikwa pale havina *influence* au havihuksiki kabisa na vijiji vingine vinavyohusika labda viliachwa.

Katika jibu la msingi, sehemu ya mwisho nimesema kwamba, namhakikishia Mheshimiwa Makwetta kwamba, suala hili tutalifanya kazi, tutalichunguza, tutatumia wadau; nimesema Ofisi ya Makamu wa Rais, Chuo Kikuu cha Sokoine na wadau wengine, tulitazame kwa undani ili tuhakikishe kwamba, linawekwa sawa, mazingira hayaharibiki. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mawili yanayofuata, yaani swali la Mheshimiwa Profesa Sarungi kwa Wizara ya Afya na swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa kwa Wizara ya Kilimo yameondolewa, kwa sababu tangu yameulizwa ufumbuzi umekwishakupatikana. Kwa hiyo, twende ukurasa wa nane, Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 102

**TANESCO Kununua Mitambo ya Kuzalisha Umeme  
kwa Kutumia Gesi**

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY (K.n.y. MHE. MOHAMED HABIB  
MNYAA) aliuliza:-**

Kwa kuwa katika teknolojia mpya Duniani iko mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia ambayo pia huweza kubadilisha maji ya Bahari na kutengeneza maji ya kawaida ya kunywa na pia hutumika kupandisha maji na kuyasambaza mijini:-

- (a) Je, mipango ya Shirika la *TANESCO* inajumuisha suala hilo?
- (b) Je, *TANESCO* ina mpango wowote wa kununua mtambo wa namna hiyo na kuuweka Dar es Salaam ili kusaidia matatizo ya maji yaliyopo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato/teknolojia inayotumia mitambo ya kuzalisha umeme na wakati huo huo kutengeneza maji salama ya kunywa kutoka kwenye maji ya bahari unajulikana kama *cogeneration* na hatua za kutenganisha maji ya kunywa kutoka kwenye maji ya bahari inaitwa *desalination*. Mitambo inayotumia teknolojia ya *cogeneration desalination* inatumia mafuta ya *fossil fuel* (kama petroli na dizeli) na vinu vya nyukilia kuendeshea mitambo hiyo.

Mitambo hii inapatikana Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini, kutokana na uzalishaji wao wa mafuta na uwezo wao wa kupata *source* ya nyukilia.

Viwanda hivi vikubwa vya kuzalishia umeme na maji, hutumia nishati au umeme mwangi sana na miundombinu ya gharama kubwa inayofanya maji yanayotokana na maji ya bahari kuwa ghali kuliko maji ya mito, maziwa na ya chini ya ardhi. Wazalishaji wakubwa wa maji yanayotokana na maji ya bahari ni *Jebel Ali Desalination Plant* ya *United Arab Emirates*, yenye uwezo wa kuzalisha *300 million cubic meters* kwa mwaka. Kiwanda kingine ambacho ni kikubwa cha *Tamper* kipo Marekani, kina uwezo wa kuzalisha galoni 25 milioni kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mitambo hii hutumia kiasi kikubwa sana cha nishati ya mafuta na *uranium*; na kwa kuwa gharama za uwekezaji wa mitambo hiyo kwa *TANESCO* ni kubwa na pia ikichukuliwa kwamba ili kuendesha mradi wa namna hiyo hapa nchini hivi sasa, itabidi kuagiza mafuta hayo kwa wingi.

- (a) Si busara kwa sasa kujumuisha mipango ya uzalishaji wa umeme na maji kwa pamoja katika mipango ya Shirika wakati uzalishaji wa mafuta na *uranium* vipo

katika hali ya utafiti wa awali na tunavyo vyanzo mbadala na nafuu zaidi vya kupata maji.

(b) Shirika la Umeme *TANESCO* halijawa na mpango wa kununua mitambo ya namna hiyo na kwa sasa bado jitihada zinazoendelea ni kupata umeme unaotokana na vyanzo ambavyo ni nafuu zaidi.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Dar es Salaam ina matatizo ya maji na kwa sababu umeme una matatizo kutokana na kuharibika kwa transfoma mara kwa mara:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna haja ya kununua *mobile generators* ambazo zinaweza zikatoa umeme zaidi ya MW 3 kwa kusaidia Jiji la Dar es Salaam pale ambapo transfoma zinaharibika?

(b) Wizara haioni kwamba kuna sababu madhubuti ya kuwa na *mobile generators* kwa maeneo nyeti ambayo yanaharibika mara kwa mara kutokana na umeme ambaeo siyo wa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, swali la msingi lilikuwa linahusiana na *Cogeneration* na *Desalination*, matumizi ya kubadilisha maji ya bahari kuingia kuwa maji ya kawaida kwa matumizi ya umeme. Sasa hili la *mobile generator* labda nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge, *mobile generator* ulizozitaja kama ulivyosema mwenyewe, *capacity* yake ni MW 3 na inabidi uzinunue nyingi kadhaa. Matumizi ya Dar es Salaam peke yake kwa sasa hivi nadhani yanakwenda kwenye MW 250.

Sasa kwa kutegemea kwamba, MW 3 hizi zita-solve tatizo la Dar es Salaam, siyo kweli isipokuwa unachozungumzia wewe ni kitu ambacho watu wa Cuba Wanasema *Henela Syondis Luida*, ambayo ni *distributed generation* ambayo unaweka vituo vidogo vidogo ili ku-support uzalishaji katika eneo fulani, umeme unapokatika unapata vyanzo mbadala vya kuendeshea mambo madogo madogo kama hospitali na kadhalika. Sasa siyo hili unalolizungumza wewe linafanana, lakini kwa Dar es Salaam *mobile generator* za MW 3 hazitusaidii. Bado kwa Dar es Salaam *solution* ni ile ambayo Serikali inayokuja nayo ya kuzalisha MW 100 pale Dar es Salaam na kuongeza uzalishaji ndani ya Dar es Salaam ku-support uzalishaji unaotoka kwenye vyanzo ambavyo viko Kusini. (*Makofii*)

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka 2004 Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu aliliambia Bunge kwamba, Dar es Salaam ingepata maji kutokana na maji ya chumvi kwa utaratibu wa *desalination* kama alivytuambia Naibu Waziri. Je, kwa wakati ule Waziri alipotoa kauli hiyo alikuwa amefikiria angewapatia watu wa Dar es Salaam hayo kutokana na teknolojia gani maana Waziri sasa anatuambia kwamba ni ghali sana kupata hayo kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nirejee jibu langu, siyo kama uzalishaji huu hauwezekaniki hapana, sasa hivi kuna

vyanzo nadhani sikumbuki idadi kamili, lakini vipo vyanzo mbalimbali nya *Desalination* ambavyo vinatumika nchi za nje huko kwa wenzetu. Isipokuwa kwa sasa hivi, asilimia 75 ya mitambo ya *Desalination* inatokana kwenye hizi ambazo zina mafuta mengi sana, ama kwa kuzalisha au kwa kuweza ku-*subsidize*. Sasa ninachosema ni kwamba, teknolojia ipo na tunaweza tukaichukua. Je, tunaweza tuka-*afford* teknolojia hiyo kwa sasa?

Tuchukue maji baharini tuyalete gharama yake ni kubwa mno. Badala yake, Dar es Salaam kama ninavyofahamu, atanisaidia Mheshimiwa Chiza, kwa sasa kuna jitihada kubwa ya kutoa maji kwenye vyanzo vilivyokuwa chini ya ardhi. Ninafahamu hivyo kwa sababu chanzo kimoja kinatokana na Kisemvule Wilayani Mkuranga na najua kingine kiko Kimbiji na ambacho kina maji mengi tu kitakachoboresha upatikanaji wa maji Mkoa wa Dar es Salaam.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee kidogo tu kwamba, teknolojia ya *desalination* ipo duniani na hivi tunavyozungumza, yako makampuni tayari yamekwishakuja Dar es Salaam na yanafanya mazungumzo na Wizara yetu. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kinachogomba hapo ni gharama ya kutumia teknolojia hiyo. Maana wao wanataka wayachuje maji yale halafu wawauzie *DAWASA*, *DAWASA* iwauzie wananchi. Sasa gharama ya teknolojia hiyo ndiyo kinachogomba, lakini teknolojia zenyewe zipo, ndiyo jambo ambalo hivi sasa tunalichunguza. Ahsante sana.

Na. 103

### **Huduma ya Umeme Jimbo la Shinyanga Mjini**

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA** aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo mengi ya Jimbo la Shinyanga Mjini hayana huduma ya umeme:-

(a) Je, ni lini *TANESCO* itapeleka huduma ya umeme katika maeneo yasiyo na huduma hiyo kama vile ya Kizumbi, Vitongoji vya Nhelegani na Bugaya-mbelele na Kata nyininge?

(b) Je, ni lini shule mpya za Sekondari zilizojengwa na wananchi katika Jimbo la Shinyanga Mjini zitapatiwa huduma ya umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Ogessa Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Naomba nitambue jitihada za Mheshimiwa Mbunge katika kufuutilia suala la upatikanaji wa umeme katika vijiji vya Jimbo lake. Tarehe 27 Julai, 2009 hapa Bungeni na nyakati tofauti, Mheshimiwa Mbunge, ameiomba Wizara yangu kupeleka umeme katika vijiji alivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, maeneo aliyyoyataja Mheshimiwa Mbunge, tayari yana umeme japokuwa waliounganishiwa huduma hiyo ni wachache, kwa mfano, katika Kata ya Kizumbi kuna *transformer* mbili zinazohudumia wateja watano tu, mashine moja ya kusaga Tawi la Chuo Kikuu cha Ushirika na wengine watatu. Nhelegani kuna transfoma mbili ambazo zinahudumia pampu za maji, zahanati, shule ya msingi na wateja wengine amba ni wachache ukilinganisha na ukubwa wa transfoma. Bugayambelele kuna Kambi ya Jeshi ambayo ina huduma ya umeme. Tatizo linaloonekana ni mwamko mdogo wa wananchi wa maeneo husika, kuomba kupewa huduma ya umeme. Wakati Serikali ikishughulikia vikwazo vya gharama vunavyosababisha wananchi wengi kushidwa kuunganisha umeme, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine amba ni umeme umefika katika maeneo yao, kuhamasisha wananchi wa maeneo yao, kuunganishiwa huduma hii muhimu katika kuinua maisha yao.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu unaokubalika, ingekuwa vyema kama kila shule, zahanati, vituo na taasisi nyingine za maendeleo na huduma za jamii zote zingeweza kupatiwa huduma muhimu kama umeme, maji, kufikiwa kirahisi na barabara na kadhalika.

Ni ukweli kwamba, hali ya sasa ya uwezo wa Serikali yetu, siyo rahisi kugharamia mahitaji yote haya, ikiwa ni pamoja na hili la kupeleka umeme kwenye shule za sekondari zote. Utaratibu uliopo ni wa kuainisha upelekaji au kufikisha huduma hii kwa mashule pale ambapo kazi hii inakuwa sehemu ya mradi mpana wa usambazaji wa umeme. Kwa kuwa hakuna mradi kwa maeneo haya kwa wakati huu, shule zilizojengwa na wananchi zitapelekewa umeme iwapo uongozi wa shule hizo utapeleka maombi pamoja na kulipia gharama za kufungiwa umeme.

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yenye ukweli ndani yake, lakini pia pasipo ukweli kamilifu, nianze kwa kuwapongeza wenzetu wa TANESCO Shinyanga, kwa kujitahidi kusambaza huduma ya umeme licha ya bajeti ndogo. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Suala la umeme Shinyanga Mjini nimelieleza kwa muda mrefu kwa Waziri. Je, Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi Shinyanga ili kufanya uhakiki wa takwimu za wateja wanaohitaji umeme amba muda mwingi nimemweleza?

(b) Kwa kuwa kuna wateja amba wapo wanahitaji umeme na walishawasilisha TANESCO Shinyanga; kwa mfano Wananchi wa Chamaguha na hata Bugayahambere; Wizara itakuwa tayari Waziri atakapotembelea Shinyanga Mjini akiambatana na mimi kuweza kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapata huduma ya umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Charles Ogesa Mlingwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, umefanywa uwekezaji wa miundombinu wa Shinyanga Mjini, lakini matumizi bado ni madogo. Hilo kama nilivyolisema kwenye majibu ya swali la msingi; ni tatizo ambalo limeonekana siyo Shinyanga Mjini tu na maeneo mengine lipo na ndiyo maana tumemwomba Mheshimiwa Mbunge alifikishe hili jambo kwa wananchi.

Pale ambapo Serikali inaweza kuingilia kupunguza gharama, Serikali itafanya hivyo. Inakuwa ngumu labda atarajie kwamba kila mtu atakapoomba hata kama akiwa umbali wa nguzo tano, sita, basi kila ambaye yuko mbali na chanzo cha umeme aletewe umeme mpaka ndani mwake, hiyo inaweza ikawa ngumu.

Mheshimiwa Spika, sasa nimepokea pongezi kwa niaba ya TANESCO na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mlingwa kwamba, nitamshauri Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, aambatane naye kwenda Shinyanga siyo kufanya uhakiki wa tathmini, uhakiki wa tathmini unafanywa na TANESCO yenyewe na wahusika wapo tunawenza tukazipata tathmini hata hapa hapa leo hii mchana. Ninadhani kuna kazi kubwa zaidi ya Mbunge na ya Waziri kwenda kufanya ambayo ni kuongea na wananchi na kuwafahamisha kuhusu utekelezaji mzuri unaoendelea vizuri wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi.

**MHE. DKT. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Utaratibu wa huduma za umeme, simu na *utilities* nyingine kawaida, miundombinu inakuwa ni mali ya kampuni inayotoa hiyo huduma na hata kwetu hapa Tanzania, nyaya zinazowekwa na transforma huwa ni mali ya TANESCO. Umezuka mtindo ambaa una miaka mingi kwamba, TANESCO unakuta inaomba fedha kutoka kwa anayetaka ile huduma. Kwa hiyo, wanalipa kama kitangulizi. Vilevile wanalipa kitangulizi unaponunua umeme wenyewe, ina maana TANESCO inatumia fedha za wateja kufanya biashara zake.

Kwa utaratibu huu hauoni kwamba Serikali inatakiwa sasa iwaambie TANESCO wawe wanaweka huduma kwanza ili biashara ambayo ni uuzaaji wa umeme ifanyike kwa taratibu ambazo zinakubalika; kwa sababu huu mtindo wa kuendelea kuchukua fedha kutoka kwa wateja *in advance* inakuwa ni kwamba wanafanya biashara kwa kutumia fedha za wateja?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge wa Ilemela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba utaratibu huu umechukua muda mrefu kidogo na nadhani umetokana na kazi kubwa iliyokuwepo ya usambazaji *vis-a-vis* uwezo wa kufanya usambazaji wenyewe ndani ya Shirika la TANESCO. Utaratibu huu Mheshimiwa Diallo anaufahamu, umeanza miaka minane au tisa iliyopita, ambapo TANESCO hali yake ilikuwa taabani kidogo.

Huu siyo utaratibu mzuri, *unless* kama tunakubaliana kwamba, mimi ninachangia kununua hii mitambo labda kwa milioni mbili, tatu, lakini kwa muda fulani ambapo wewe utakuwepo, mimi kama TANESCO matumizi yangu ya umeme utakuwa unanikata mpaka tukimaliza deni, *then that is acceptable*.

Kwa hiyo, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Diallo kwamba, utaratibu huu inabidi uangaliwe baina ya TANESCO yenyewe, Serikali, lakini pia pana *consumer watchdogs*, wawakilishi wa wateja na watumiaji wa huduma mbalimbali kama ilivyo kwenye maji na kadhalika ili tuangalie huu utaratibu wa mteja kununua nyaya, *transformer*, nguzo na kadhalika kama unalingana na utaratibu wa *best practice* ya ufikishaji wa huduma ya umeme.

Na. 104

### **Kutoshuka Nauli za Maboti Kagunga Hadi Kigoma**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa sasa mafuta yameshuka bei kwa vyombo vya kusafiria; na kwa kuwa wasafiri wa boti kutoka Kigoma hadi Kagunga hutozwa nauli ya shilingi 4,000, bei ambayo ni ya zamani hata kabla ya kushuka kwa bei ya mafuta:-

(a) Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao ili SUMATRA Kigoma waweze kupunguza nauli hiyo iwe shilingi 2,000?

(b) Kama nauli itarekebishwa; je, ni lini sasa nauli hiyo itaanza kutumika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kigoma, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta zilianza kupungua mwezi Novemba, 2008 kutokana na kuyumba kwa uchumi wa dunia ambapo mahitaji ya mafuta yalipungua na kusababisha bei ya mafuta kupungua pia. Hata hivyo, mwenendo wa bei za mafuta kwa sasa hivi ni wa kupanda, kwa mfano, bei ya mafuta ya dizeli kwa lita imeongezeka kutoka wastani wa shilingi 1428.29 kwa lita mwezi Machi, 2009 hadi wastani wa bei kikomo wa shilingi 1720 kwa lita kufikia mwezi Machi, 2010.

Kwa upande wa Kigoma, bei kikomo kwa mafuta ya dizeli mkoani humo ni shilingi 1847 kwa lita kwa mwezi Machi, 2010.

Mheshimwia Spika, Visiwa vya Kagunga, Mtanga, Gombe na vinginevyo ndani ya Ziwa Tanganyika, huhudumiwa na usafiri wa maboti ukilinganisha na miji mingine yenye bandari ambayo huhudumiwa na meli. SUMATRA iliridhia viwango vya juu vya nauli ya usafiri wa maboti Mkoani Kigoma tarehe 13 Machi, 2008, wakati huo wastani wa bei ya dizeli kwa lita ikiwa shilingi 1700.

Hivi sasa bei ya mafuta ya dizeli kwa Mkao wa Kigoma imefikia shilingi 1847 kwa lita. Hivyo basi, bei ya mafuta ya sasa imekwishavuka kiwango cha bei ambacho kilitumika mwezi Machi, 2008.

Aidha, ukokotoaji wa nauli huangalia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na gharama za ununuza wa chombo, uchakavu, matengenezo, mishahara, bima, nishati na vilainishi. Kwa kuzingatia ya kwamba, mwenendo wa vigezo hivyo kwa sasa hivi umekuwa ni wa kupanda, uwezekano wa kupunguza nauli hiyo kwa sasa iwe shilingi 2000 ni vigumu kuufikia.

Hata hivyo, Serikali inaiagiza SUMATRA kufuatilia mwenendo wa vigezo hivyo ili vitakaporuhusu, SUMATRA ifanye mabadiliko ya nauli ipasavyo kwa manufaa ya wananchi wanaotumia huduma hiyo.

Na. 105

### **Ujenzi wa Barabara ya Masasi - Mangaka**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanza kujenga Barabara ya Masasi -Mangaka kwa kiwango cha lami kupitia Kampuni ya Tokura:-

Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya kujenga mifereji ya maji kwenye barabara hiyo ili kuboresha zaidi ujenzi wa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, Mkao wa Mtwara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa barabara ya Masasi - Mangaka

unafadhiliwa na Serikali ya Japani kuitia Shirika lake la JICA. Katika ufadhilli huu, gharama za kujenga mifereji ya maji hazikujumuishwa katika ufadhilli wa miradi na badala yake gharama hizo zilitengewa fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa Barabara ya Masasi -Mangaka kwa awamu ya kwanza yenyе urefu wa kilomita 15 imekamilika. Pia kazi ya ujenzi wa mifereji ya maji kwa sehemu hii tayari imekamilika kwa kutumia fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili hiyo. Kiasi cha shilingi milioni 430 zimetumika kugharamia ujenzi wa mifereji ya maji.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa barabara awamu ya pili, yenyе urefu wa kilomita 17.6 pia imekamilika. Fedha kwa ajili ya ujenzi wa mifereji kwa sehemu hii itatengwa kwenye bajeti ya 2010/2011.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kufahamu suala la mifereji kuanzia Masasi Mjini mpaka kufikia Mangaka. Kwenye Barabara hii kuna makutano ambayo kuna barabara inayotoka Newala, Lindi, Nachingwea na Tunduru, sehemu ambayo mara nyingi sana zinatokea ajali nyingi kwa kuwa wakati unafanyika ujenzi huu hakukujengwa *roundabout*. Je, Mheshimiwa Waziri mtakapokuwa mnatenga hela za mifereji kwa awamu ya pili; hamuwezi mkatenga pia fedha kwa ajili ya kutengeneza *roundabout* katika eneo hili nililolitaja? (*Makofî*)

(b) Kwa kuwa katika ujenzi wa barabara hii kulifanyika pia fidia kwa wale ambao walibomolewa majumba na mimea, lakini wapo akinamama wawili ambao mpaka hivi sasa hawakulipwa fidia hizo na wanahangaika na ni vikongwe na wanakaa na watoto yatima. Wanasaidiwa tu kukaa na raia wema. Je, Mheshimiwa Waziri utawasaidiaje akinamama hawa ili waweze kupata fidia hiyo ya nyumba zao? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifutavyo:-

Kama nilivyoeleza hapa kwenye kujibu swali la msingi kwamba, Serikali imetenga fedha za kutengeneza hii mifereji kwa kutumia fedha za ndani na kwa awamu ya kwanza tumeshakamilisha ujenzi huo na katika awamu ya pili kama nilivyokuwa nimesema, fedha zitatengwa katika bajeti ya mwaka unaokuja, lakini niongeze tu kwamba katika awamu ya tatu ambayo vilevile JICA imekubali kujenga, suala la mifereji sasa limeingizwa katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, katika suala la *roundabout* ni suala la utaratibu wa ujengaji, kama katika ile *design* inayotengeneza barabara hii, kigezo cha *roundabout* kipo basi hilo litazingatiwa. Kwa ombi la Mheshimiwa Mbunge, tutaweza kushirikiana na wenzetu ambao wanasmamia ujenzi kule kuona kama kuna mahali

tunaweza kufanya marekebisho hayo ili matatizo yanayojitokeza sasa hivi yasiweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, hili la pili kuhusu fidia ya hawa akina mama wawili, mimi nasikitika na kuwapa pole, maadamu ndio nalisikia hapa, niombe tu Mheshimiwa Mbunge tuweze kuwasiliana ili tuweze kuangalia ilitokeaje hawa akinamama wakarukwa katika kulipa fidia na kama haki yao ipo wataweza kusaidiwa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na tatizo kubwa la ujenzi wa barabara na hasa hivi sasa ambapo wakandarasi wamekuwa hawalipwi na baadhi ya wakandarasi, kwa mfano, mkandarasi wa Barabara ya Mwandiga - Manyovu ametishia hata kusimama kuendelea na ujenzi kwa sababu anaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni kumi na mbili na ni wakandarasi takriban nchi nzima wanaidai Serikali. Sasa Waziri anasema nini kuhusu suala hili ili kuhakikisha kwamba miradi ambayo inaendelea kujengwa inamalizwa kwa wakati?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabwe Zitto kama ifuatavyo:-

Katika mwaka huu fedha 2009/2010 ni kweli tulipata matatizo kipindi fulani cha kuwalipa makandarsi ndani ya muda ambao walipaswa kulipwa na hasa makandarsi wapya ambao mikataba yao ilisainiwa katika mwaka huu wa fedha. Tatizo hilo tumelishughulikia na sasa hivi kwa kiasi kikubwa tumewalipa makandarasi wote ambao walitakiwa kuanza kazi. Kuna upungufu mdogo tutaushughulikia tutahakikisha kwamba, tunayakamilisha ili tusiikwaze kazi ya kujenga barabara.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umeshapita sasa ni matangazo na kama kawaida naanza na wageni.

Mgeni wa kwanza ni Mheshimiwa Clemens Hach, Naibu Balozi wa Ubalozi wa Ujerumanu hapa Tanzania kutoka Dar es Salaam. *Welcome to Dodoma your Excellency, we are happy to have a representative from one most useful development partners to be with us here this morning. Thanks very much for the visit.*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Philip Marmo, ambao kwanza ni mkewe, hakuandika jina ni mkewe; ahsante sana. Wapo pia Walimu Wakuu na Waratibu Kata wa shule kumi bora za msingi mwaka 2009. Ninaomba hawa Walimu Wakuu na Waratibu Kata wa shule kumi bora za msingi tafadhali wasimame tuwatambue; hongera sana kwa kazi nzuri, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri sana mliyofanya ya kuweza kufaulisha vijana wetu. Endeleeni na kazi njema hiyo.

Miongoni mwao wapo pia Wakuu wa Shule na Walimu wa Taaluma wa shule tano bora za sekondari mwaka 2009; ahsante sana. Hawa ndiyo wa sekondari, wengine walikuwa shule za msingi. Hawa ndiyo mabingwa wa zile shule za sekondari tano

zilizofanya vizuri sana katika taaluma mwaka 2009; tunawashukuru sana kwa kazi hiyo njema endeleeni na moyo huo huo.

Wageni wengine waliopo ni Ndugu Anatory Choya, Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo. *DC* huyu aliwahi kuwa Mbunge, ingawa siyo katika Ukumbi huu.

Yupo Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Biharamulo; Ndugu Zacharia Isayi, Mwenyekiti wa Halmashauri; Ndugu Simon Mayeye, Mkurugenzi wa Halmashauri ile; Ndugu Emmanuel Tango, Afisa Elimu wa Wilaya; Ndugu Michael Hadu, Afisa Elimu wa Wilaya Sekondari; na Ndugu Peter Tahani, Katibu wa Mbunge.

Wapo pia Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum katika ujumbe huu; ahsanteni sana. Hao ndiyo wageni wa Mheshimiwa Philip Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge). (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe ni Ndugu Ami Mpungwe, Balozi Mstaafu. Haa, yule pale. Nakumbuka Ndugu Ami Mpungwe alikuwa Balozi wetu kule Afrika Kusini. Amefanya kazi nzuri sana ya kutukuka na sasa ameingia katika sekta binafsi ambako pia mambo yake yanashamiri. Ahsante sana Balozi. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami ni kutoka Moshi Vijijini ambao ni Ujumbe wa CCM Wilaya ya Moshi Vijijini wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Moshi Vijijini, Ndugu Komredi Gabriel Masenga. Kutoka Moshi Vijijini; wale pale karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni 18 wa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, ambao wanatoka Wizarani kwake, kwenye Taasisi, Wadau wa Sekta ya Madini, wakiongozwa na Katibu wa Wizara, Ndugu David Jairo; yule pale. Kamishna wa Madini, Dkt. D. Kafumu na Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO*, Bwana Ramadhani Hatibu; yule pale, karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni 15 wa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John Chiligati, ambao ni Wajumbe wa Baraza la Wazee wa CCM kutoka Kata ya Chikuyu, Manyoni. Wazee wetu kutoka Manyoni; wale pale. (*Makofi*)

Huu ni utaratibu mzuri sana wa kuwakumbuka wazee wetu hawa, siyo kuwaacha tu huko vijijini. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, kwa kufanya kitendo hiki cha kuwakumbuka wazee nao. Mara nyingi wageni wanaokuja hapa wanakuwa siyo wa aina hiyo. Karibuni sana wazee wetu na tunazidi kuwaenzi kwa kazi kubwa sana mliyofanya kutufikisha hapa. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, wakiongozwa na Kaimu Mkurugenzi wa Muungano, Ndugu Baraka Rajabu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, ambaye pia ndiye Kamanda wa Vijana wa CCM Wilaya hiyo, pamoja na kuwa ameamua kustaaafu Ubunge, lakini ana wageni wake sita ambaao ni Kamati ya Utekelezaji ya Umoja wa Vijana Wilaya ya Sumbawanga Mjini, wakiongozwa na Ndugu John Myovela. Wale pale, karibuni sana. Ahsante sana kwa kuitikia wito wa Kamanda wenu. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Capt. John Komba kutoka Shule za *Bakili Muluzi High School* na *Colleta Primary School Dar es Salaam* ambaao ni Ndugu Elias Mushendwa na Ndugu Dorah Joseph. Wageni kutoka Dar es Salaam katika zile shule mbili nilizozitaja; basi labda wapo katika Ukumbi wa *Basement*.

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo cha *UDOM*, nadhani kutoka jimboni kwake ambaao wamekuja kushuhudia shughuli za Bunge. Wanafunzi wa *UDOM* kutoka Musoma Mjini; labda nafasi ilikuwa finyu kidogo.

Wageni wa Mheshimiwa Nazir Karamagi, ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha *UDOM* wanaotoka Jimbo la Bukoba Vijijini, Jimbo lake Mheshimiwa Nazir Karamagi. Wale vijana wa Chuo Kikuu Dodoma kutoka Bukoba Vijijini.

Wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, ni Kikundi cha *Muhajirina Women* kutoka Madrassa Zaharaa Bondeni, Kondoa Kaskazini, wakiongozwa na Ndugu Zuhura Hamisi Boma, Mwenyekiti wao. Ahaa, ooh ahsante sana. (*Makofi*)

Tunawashukuru sana wageni wetu kutoka Kondoa ambaao mko katika mstari mzuri wa kumwabudu Mwenyezi Mungu. Basi mnapomwombea Mbunge wenu, msisahau katuombea Wabunge wote, kwa sababu mtihani alionao sisi sote tunao hivyo hivyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Manju Msambya ni Ndugu Silas Samson Mkusu, Mwinjilisti wa Kanisa la KKKT Nguruka, Kata na Tarafa ya Nguruka. Ahsante sana Baba, aah wengine wako huku kumbe; ahsante sana. Ahsante sana Baba Mwinjilisti kwa kumuunga mkono Alhaji Msambya. (*Kicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa Janet Mbene, ambaao ni Viongozi wa CCM na Jumuiya zake kutoka Kata ya Msasani, wakiongozwa na Mtendaji wa Kata, Ndugu Badiri Mangula. Aah karibuni sana ndugu zangu wa Msasani. Namshukuru sana Mheshimiwa Janet Mbene, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Msasani. Huyu ni Mwenyekiti wetu tunaokaa kule Msasani. Karibuni sana majirani zetu. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, ambaao ni Makatibu Wenezi wa CCM Wilaya wakiongozwa na Katibu Uenezi CCM Wilaya ya Ilala, Ndugu Said Sidde. Aaah karibuni sana ndugu zangu wa Ilala; ahsante sana. (*Makofi*)

Inaelekea huyu ndugu yetu Zungu amejizatiti kweli huko Ilala, nawahurumia wote wanaonyemelea Ilala ni tabu tu. (*Makofi*)

Wapo wageni watano kutoka Taasisi ya UMATI, wamekuja kuendesha mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Maendeleo ya Jamii, Huduma za Jamii na Fedha na Uchumi wakiongozwa na Ndugu Alfred Mutanera. Wale wa UMATI; aaah wapo upande huu, karibuni sana ndugu zetu. (*Makofi*)

Pia tunao wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Biashara (*CBE*) Dodoma, sijui kama wamepata nafasi leo, nadhani watakuwa katika eneo lingine wakitazama kwenye TV.

Wanafunzi 20 kutoka Shule ya Msingi ya Martin Luther Dodoma; nadhani nao wamepata nafasi kwenye *Basement*. Tunawapongeza sana wanafunzi na walimu wa *Martin Luther Secondary School Dodoma*. Tunaelewa kwamba, mazingira ni mazuri, wazazi wengi wanapeleka watoto wao kwenye shule hiyo. Mnao wateja hata humu mingoni mwa Wabunge kadhaa na Mawaziri ambao wameleta watoto pale. Tunawatakia mema, mna majengo mazuri. Siku moja labda mtanialika na mimi nije niangalie tu, maana huwa napita barabarani bila kuyaona. Hongera sana kwa kazi njema. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wapo wanafunzi sita kutoka AIESEC Tawi la Chuo Kikuu Dar es Salaam; wale wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Basi nadhani wamepata nafasi sehemu nydingine.

Mwisho, tunao wageni kutoka Taasisi ya *Engender Health* ambao wamekuja kuendesha mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Huduma za Jamii na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wakiongozwa na Dkt. Erick Ramirez Feroro. Wako wapi sijui? Aah wale pale, karibuni sana Dkt. Feroro na wenzako.

Yeye anaitwa *Project Chief Champion*. Basi Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu yanahuusu afya na afya ni muhimu, ukizingatia hizo ngwe zinazokuja, lazima uwe na afya nzuri; kwa hiyo ni vizuri kuhudhuria mafunzo haya ya hawa wenzetu. Ahsante. (*Makofi*)

Matangazo ya kazi zetu. Mheshimiwa John Momose Cheyo, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali, mkutane leo katika Ukumbi Na. 219, saa saba mchana.

Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu mkutane saa saba mchana katika Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kuwa, leo tarehe 22, saa kumi jioni, kutakuwa na Kikao cha Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani katika Ukumbi Na. 219, ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, anaomba Wabunge walio Wajumbe wa Kamati hiyo mkutane saa saba mchana katika Ukumbi wa *Basement*.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba Wajumbe wote wa Kamati tatu hizi; Maendeleo ya Jamii, Fedha na Uchumi na Huduma za Jamii, mkutane leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Huo ndiyo mwisho wa matangazo. Sasa nitamwomba Katibu atuelekeze katika shughuli inayofuata.

## **KAULI ZA MAWAZIRI**

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kufuatia mvua kubwa zilizonesha kuanzia tarehe 24 hadi 31 mwezi wa kumi na mbili mwaka 2009 katika Mikoa ya Dodoma na Morogoro, maeneo mengi yaliyoko kwenye Bonde la Mto Mkondoa yaliathirika vibaya sana. Athari hiyo ni pamoja na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya reli na barabara.

Kwa upande wa reli, maafa makubwa yametokea kati ya Stesheni za Kilosa na Gulwe, uharibifu huu unaweza kulinganishwa na ule uliotokea mwezi Novemba mwaka 1997 wakati wa mvua za *El-Nino*. Vile vile maeneo mengine kati ya Morogoro na Kilosa na kati ya Stesheni ya Gulwe na Msagali nayo yaliathirika.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kurejesha miundombinu ya reli iliyoharibiwa na mafuriko katika maeneo ya Kilosa Mkoani Morogoro na Gulwe Mkoani Dodoma ilianza rasmi tarehe 5 mwezi wa pili mwaka huu wa 2010 kwa upande wa Kilosa na tarehe 16 mwezi wa pili mwaka 2010 kwa upande wa Gulwe. Kwa ujumla maeneo 32 yaliathirika. Kati ya hayo, maeneo 26 ndiyo yaliathirika zaidi. Kazi za urejeshaji wa miundombinu ya reli inafanywa kwa ushirikiano kati ya Wataalam wa *RAHCO*, *TRL*, Wizara ya Miundombinu na Jeshi la Wananchi la Tanzania, ambao kwa pamoja wameifanya kazi hiyo kwa juhudhi na uadilifu mkubwa. (*Makofii*)

Kazi ilianza kwa kasi ndogo kuliko ilivyotarajiwa kutokana na matatizo ya upatikanaji wa mitambo. Tatizo hili lilitatuliwa na *RAHCO* kwa kukodisha mitambo mingi kutoka kwa makapuni binafsi. Kwa upande wa Kilosa, hali ya mvua pia imechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza kasi ya ukarabati. Kila mvua inaponyesha, kazi ya kujenga tuta husimama na wakati mwingine kulazimu kurudi nyuma kuimarisha matuta yaliyokamilika ili kudhibiti uharibifu usitokee kutokana na maji yanayoongezeka katika Mto Mkondoa. Kati ya maeneo 32 yaliyokuwa yameharibika katika njia ya reli, maeneo 20 tayari yamekarabatiwa, maeneo yaliyosalia ni 12 na kati ya hayo ni maeneo makubwa sita tu ndiyo ambayo yamesalia kukarabatiwa.

Kazi muhimu ya kujengea kingo za reli na kingo za mto ili kuzuia uharibifu unaoweza kutokea endapo mvua zitanyesha inafuata nyuma. Kazi hii imeanza na itaendelea kufanya wakati treni zinapita. Kwa upande wa Kilosa, Stesheni ya Munisagara ambayo ni ya kwanza kutoka Kilosa imefunguliwa na njia inapitika hadi kilomita 303 kutokea Dar es Salaam.

Kwa upande wa Gulwe, Stesheni ya Godegode pia ambayo ni ya kwanza kutoka Gulwe imefunguliwa na njia inapitika hadi kilomita 338 kutoka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizombwa kwa kazi hii ni shilingi 15.7. Fedha zilizokwisha kupokelewa kutoka Mfuko wa Maafa Hazina ni shilingi bilioni 10.7 na fedha zilizokwisha pelekwa *RAHCO* hadi hivi sasa ni shilingi bilioni tisa milioni mia mbili themanini na mbili. Serikali kupitia Mfuko wa Maafa Hazina, imejipanga kutoa fedha zilizosalia kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya reli. Kwa taarifa nilizozipata hivi punde tu, kabla sijasoma taarifa hii ni kwamba, Serikali imeshatoa fedha zote zilizosalia kwa ajili ya kazi ya kurudisha miundombinu hii ya reli.

Mheshimiwa Spika, baada ya vifaa na mitambo mingi kuwa vimefika eneo la kazi, ratiba ya kazi ilipitiwa na kuboreshwa. Ratiba hiyo mpya inaonesha kuwa kazi za kujenga tuta na kuunganisha reli itakamilika tarehe 14 mwezi wa tano mwaka huu wa 2010. Kazi ya kujengea kingo za tuta za reli na kingo za mto ili kuzuia uharibifu unaoweza kutokea endapo mvua kubwa zitanyesha itaendelea wakati treni zinapita. Changamoto iliyopo ni kwa upande wa Kilosa ambapo hivi sasa ni msimu wa mvua za masika. Hali hii inaweza kuathiri utendaji wa kazi na pengine kuathiri kidogo ratiba ya kukamilisha kazi yenye.

Kazi itakayokuwa imekamilika ni ile tunayooiita kazi ya muda mfupi. Kazi kubwa ya muda mrefu ya kudhibiti tuta la reli, kujenga madaraja na makalvati ya kudumu pamoja na kujenga kingo ya Mto Mkondoa, zitaendelea kutekelezwa baada ya kurudishia miundombinu ya reli kwa ngazi hii ya sasa ya dharura.

Mheshimiwa Spika, huduma za treni kuanzia Dar es Salaam zinatarajiwa kuanza mara baada ya njia kufunguliwa na kupata ruhusa kutoka kwa Idara zinazohusika kama ifuatavyo:-

- (i) Baada ya njia kufunguliwa *SUMATRA* na *TRL* watakagua njia kati ya Dar es Salaam na Dodoma ili kuangalia hali ya usalama kwa treni kupita.
- (ii) Baada ya kuridhika na usalama wa njia, *TRL* itaanza kupitisha treni za mizigo kwa muda wa siku 14 ili kujiridhisha na hali ya usalama.
- (iii) Mheshimiwa Spika, baada ya usafiri wa majaribio kwa kutumia treni za mizigo kudhihirisha usalama wa reli na *SUMATRA* kuridhia, usafiri wa abiria utaanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kwa taarifa hiyo inayotupa matumaini watumiaji wote wa reli ya kat. Katibu, kwa hatua inayofuata.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

## **Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010** *(The Mining Bill, 2010)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kusoma maelezo yanayohusu hoja yake ya Sheria ya Madini, nimetumia mamlaka yangu katika Kanuni, kuruhusu asome wakati jedwali la mapendekezo ya mabadiliko mbalimbali likiwa linakamilishwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria (CPD). Naambiwa litagawiwa katika muda kama wa saa moja hivi, lilitakiwa liwe tayari hapa, lakini sasa nimeona kwa uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, tusikilize hoja ya Mheshimiwa Waziri, tutaendelea kupata mapendekezo ya mabadiliko, yaani *schedule of amendments* wakati bado tukiwa humu ukumbini. Kwa kuwa tunaendelea hadi jioni, basi hilo halina tatizo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo, sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ili awasilishe hoja yake ya Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nikushukuru wewe binafsi kwa kuruhusu kuanza kuwasilisha Muswada huu wakati bado jedwali la mabadiliko likirekebishwa na kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, ninayo heshima kubwa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010. Muswada huu unalenga kutunga sheria mpya ya madini, itakayoongeza manufaa ya Sekta ya Madini katika kipato na ukuzaji wa uchumi katika Taifa letu, kwa kuendelea kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika sekta hii ambapo sekta binafsi itaendelea kupewa kipaumbele katika kushiriki katika kuendeleza rasilimali za madini. Sheria ya Madini inayotungwa inalenga kuongeza fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nyingine za uchumi ili kuongeza manufaa ya kiuchumi na kijamii, yatokanayo na Sekta ya Madini kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 itakayotungwa, inalenga pamoja na mambo mengine, kuongeza ushiriki wa Serikali na wa Wananchi wa Tanzania kwenye shughuli za madini. Kuweka mazingira ya Watanzania kuchimba madini ya vito na pale inapobidi, kwa ushirikiano na wawekezaji kutoka nje ya nchi ili kuhawilisha teknolojia na kupata mitaji ya uwekezaji. Kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuwatengenya maeneo na kuwapa leseni za utafutaji na uchimbaji mdogo, zenye muda wa kutosha kuwekeza na kuweka mazingira kwa migodi kutumia huduma na rasilimali zipatikanazo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa kushirikiana na Serikali, kwa pamoja tumefanya marekebisho na hasa kwa kuzingatia ushauri ambao umezaa matokeo ya kuboresha Muswada. Katika ushauri huo, pia tumezingatia ushauri

uliotolewa na Kamati ya Kumshauri Mheshimiwa Rais, iliyoongozwa na Mheshimiwa Jaji Mstaafu Mark Boman na wadau wengine kwa ujumla kuhusu Sekta ya Madini. Katika ushauri huo, yako baadhi ya masuala ambayo hayajitokezi katika Muswada huu, lakini Serikali inatambua umuhimu wake na imejipanga kuyafanya kazi kwa kina kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya masuala tuliyoshauriwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu na wadau kwa ujumla ni pamoja na uundwaji wa Mamlaka ya Madini kwa ajili ya kuindeleza na kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Madini; uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Madini na kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mahakama Huru ya Madini, yaani *Independent Mining Tribunal*, kwa ajili ya kutatua migogoro katika Sekta ya Madini. Kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka ya Madini, suala hili ni muhimu na utekelezaji wake unahitaji kuwepo na sheria itakayosimamia mamlaka hiyo. Aidha, utekelezaji wake unahitaji maandalizi na muda wa kutosha ili kufanya utafiti utakaoiwezesha Serikali kupanga na kutekeleza uanzishwaji wa Mamlaka hiyo kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Madini kwa lengo la kuimarisha uendeshaji wa Sekta ya Madini, ugharamie miradi mikubwa ya maendeleo nchini na kuleta maendeleo kwenye maeneo yenye migodi. Pendekezo hili ni zuri na Serikali italifanya kazi ili kuanzisha Mfuko huo kwa wakati muafaka. Kimsingi, wadau wanapendekeza Mfuko huo uanzishwe na uwe tokeo la Mamlaka ya Madini ambayo tunaiongelea kuianzisha. Uanzishwaji wa *Independent Mining Tribunal*, kwa lengo la kurahisisha utatuzi wa migogoro mbalimbali katika Sekta ya Madini ni ushauri utakaofanyiwa kazi kwa kuzingatia uzoefu kwenye nchi nyingine zenye maendeleo makubwa katika Sekta ya Madini na kutekelezwa kulingana na matokeo ya utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa utungaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, uliana mwaka 2009 wakati Serikali ilipotunga Sera ya Madini kwa lengo la kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya Mwaka 1998. Changamoto hizo ni pamoja na fungamanisho duni la Sekta ya Madini na Sekta nyingine za uchumi. Mchang'o mdogo wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa ukilinganisha na ukuaji wake, uwezo mdogo wa Serikali kusimamia Sekta ya Madini na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, kuanzia mwaka 2002, Serikali iliunda Kamati mbalimbali kutathmini mwenendo wa Sekta ya Madini kwa ujumla. Mionganoni mwa Kamati hizo ni Kamati ya Kuchunguza Chanzo cha Migogoro baina ya Kampuni iliyokuwa inajulikana kama *AFGEM* na sasa inajulikana kama *Tanzanite One* na wachimbaji wadogo wa Mirerani mwaka 2002. Kamati ya kudurusu Sera ya Madini ya Mwaka 1997 iliyofanya kazi yake mwaka 2004, Kamati ya Kupitia Mikataba na Mfumo wa Kodi katika Sekta ya Madini iliyofanya kazi mwaka 2006, Kamati ya Majadiliano ya Mikataba baina ya Serikali na Kampuni za Madini, iliyofanya kazi mwaka 2006 pia na Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini, iliyofanya kazi yake mwaka 2007. Aidha, katika kuongeza juhudhi za usimamizi wa sekta, Serikali ilianzisha Kitengo cha Ukaguzi wa Uzalishaji na Biashara ya Madini katika migodi mikubwa ya dhahabu. Tathmini hizo zimesababisha kuwepo

umuhimu wa kutunga sheria mpya ya madini, kukidhi matakwa ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na kuzikabili changamoto na kuleta maendeleo endelevu ya Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umeandaliwa baada ya kufanya mashauriano na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais (Mazingira), Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Mipango, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*), Waheshimiwa Wabunge, Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola, Kampuni za Uchimbaji wa Madini, *Chamber of Minerals and Energy*, Wachimbaji Wadogo, Benki Kuu ya Tanzania, Taasisi za Kiraia na zisizo za Kiraia, *NGOs*, Ofisi za Ubalozi za Canada na Afrika ya Kusini na Vyombo vya Habari.

Mchakato wa kuwashirikisha wadau ulifanyika katika kipindi cha kuanzia mwezi Disemba, 2008 hadi jana tarehe 21, Aprili, 2010, ambapo kikao cha mwisho na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kilifanyika. Kimsingi, wadau walikubali kutungwa kwa sheria mpya ya madini.

Pamoja na ushirikishwaji wa wadu hao, utungaji wa sheria ya madini ya mwaka 2010 pia umezingatia uzoefu wa nchi nyingine za Ghana, Botswana, Namibia, Canada, Australia, Marekani na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kufuta Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 na kutunga Sheria mpya ya Madini ya Mwaka 2010, itakayoainisha masharti ya utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, usafishaji na biashara ya madini. Mfumo wa utoaji, uhuishaji na ufutaji wa leseni za madini, ulipaji wa mrabaha na ada mbalimbali na masuala mengine yanayohusika na usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Ushiriki wa Serikali katika shughuli za madini na ushiriki wa wananchi katika kuendeleza Sekta ya Madini pamoja na kumiliki hisa za kampuni zinazochimba madini nchini.

(ii) Mfumo wa uingajji mikataba ya madini kati ya Serikali na kampuni za uwekezaji katika Sekta ya Madini, unaohusisha kipengele cha kupitia utekelezaji wa mikataba kila baada ya kipindi cha miaka mitano na kuboresha kipengele kinachohusu uzuwajji wa mabadiliko ya kodi na ada mbalimbali na kiwango cha uwekezaji kinachoruhusu kuwepo kwa mkataba.

(iii) Kuanzisha makundi ya madini na kuruhusu utoaji wa leseni za uchimbaji mdogo na wa kati ndani ya leseni ya utafutaji mkubwa kwa makundi tofauti.

(iv) Kuzuia utoaji wa leseni ya biashara ya madini ya urani na kutunga kanuni maalumu kusimamia shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini ya mionzi.

(v) Kuondoa baadi ya aina za leseni na kuanzisha aina nyingine ya leseni za *processing, smelting na refining*.

(vi) Kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Madini kwa kubadilisha mamlaka za utoaji wa leseni ili kuhusisha Maafisa Madini wa Kanda katika utoaji wa leseni za uchimbaji mdogo na biashara ya madini.

(vii) Kuweka vifungu vya sheria vinavyosimamia uachiaji wa maeneo ili kuweka mazingira ya kutenga maeneo kwa wachimbaji wadogo na kudhibiti tabia ya kuhodhi maeneo mengi, ikiwa ni pamoja na kuzuia umiliki wa leseni zinazozidi 20 kwa mtu mmoja.

(viii) Kufuta Bodi ya Vito na kuimarisha kazi za Kamati ya Ushauri ya Madini kwa kuanzisha Bodi ya Ushauri.

(ix) Kubadilisha mfumo wa ukokotoaji wa mrabaha na kuongeza viwango kwa aina mbalimbali za madini.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 11 zinazopendekeza mambo mbalimbali kuhusu uendelezaji na usimamizi wa Sekta ya Madini. Sehemu ya kwanza inahusu jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika, matumizi na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya sheria hii inayopendekezwa. Sehemu ya pili inahusu misingi ya jumla. Katika sehemu hii, vifungu vinavyohusu udhibiti wa madini, kibali au ruhusa inayotakiwa kwa ajili ya kutafuta au kuchimba madini, aina ya leseni na masharti ya utoaji wa leseni, uhamishwaji wa leseni ya madini, ada ya leseni, mkataba wa uchimbaji wa madini, uhalali wa mkataba wa uchimbaji wa madini, majukumu ya jumla na ya mmoja mmoja katika umiliki wa leseni; maombi ya leseni ya madini kwa njia ya zabuni na makosa yanayohusu biashara ya madini isiyoruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu namba nane cha sehemu ya pili katika Muswada huu, kinaainisha ushiriki wa Watanzania katika uchimbaji wa madini ya vito kwa kuelekeza kuwa, uchimbaji wa madini ya vito ni kwa ajili ya Watanzania tu na endapo kutakuwa na umuhimu wa kuchimba madini haya kwa ubia na wageni, ubia huo usipungue 50% za Mtanzania au Watanzania na Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana ya madini ambaye ndiye atakayeamu kwa niaba ya Serikali. Umuhimu huo utazingatia teknolojia, utaalamu mahususi na mahitaji ya kutosha. Utaratibu huu ni mpya kwa sababu haumo katika Sheria ya Madini ya sasa. Aidha, utaratibu huu unazingatia matakwa ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009, ambayo tayari imeshaanza kutumika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vifungu namba 10, namba 11 na namba 12 vya sehemu ya pili ya Muswada huu, vinahusu masuala ya mikataba kati ya Serikali na Mwekezaji ambapo kifungu namba 10, kinahusu Serikali kupata hisa zisizolipiwa, yaani *free carried*

*interest*, katika kampuni kubwa za madini kwa kiwango kitakachopangwa na Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana ya Sekta ya Madini kwa mashauriano na mwekezaji. Serikali pia kwa kupitia mashirika yake kama *STAMICO* na Shirika la Maendeleo ya Taifa (*NDC*), itaweza kununua hisa zaidi katika kampuni hizo ikiwa itaona ina manufaa kwa Taifa. Hiyo itakuwa ni nyongeza ya zile *free carried interest*. Suala hili halipo katika mikataba iliyoingiwa chini ya sheria tunayopendekeza kufutwa. Vilevile chini ya kifungu hicho, mikataba itaingiwa endapo uwekezaji utakuwa unafikia kiwango kisichopungua Dola za Marekani milioni 100 atakazowekeza mwekezaji, wakati sheria ya sasa haina sharti la kigezo cha mtaji wa kiwango hiki ili kupata sifa ya kupata mkataba maalum wa uwekezaji, yaani *Mining Development Agreement (MDA)*, ambao huambatana na vivutio kadhaa.

Mheshimiwa Spika, kifungu namba 11 kinahusu uhai wa Mkataba ambao utazingatia uhai wa leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini, yaani *Special Mining License* na kifungu namba 12 kinaelekeza kuwa, mikataba itakuwa inapitiwa kila baada ya miaka mitano. Sehemu ya tatu ya Muswada wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, inahusu uteuzi wa Kamishna wa Madini na Maafisa wengine. Kazi za kukasimu madaraka ya Kamishna wa Madini, uchoraji wa ramani za kijiolojia, uundaji wa Bodi ya Ushauri ya Madini na majukumu yake, Kamati za Wataalamu za Bodi, uanzishaji wa Ofisi za Kanda, makatazo kuhusu utoaji taarifa na haki ya ulinzi wa kisheria kwa wasimamizi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne inahusu leseni za madini kwa kujumuisha masuala ya utoaji, uombaji na masharti ya leseni. Sehemu hii imegawanyika katika maeneo makuu matano, ambayo ni:-

- (a) Leseni za utafutaji mkubwa wa madini.
- (b) Leseni za uchimbaji mkubwa wa madini.
- (c) Leseni za utafutaji na uchimbaji mdogo wa madini.
- (d) Leseni za uchenjuaji na usafishaji wa madini.
- (e) Masharti ya jumla yanayohusu leseni za madini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo (b), kifungu namba 43, kinaelekeza kuwa, leseni za uchimbaji mkubwa wa madini, yaani *special mining license*, sasa zitatolewa kwa kuzingatia kiasi cha mashapo kilichoainishwa kwenye taarifa ya upembusi yakinifu, yaani *feasibility study*. Marekebisho haya yanalenga kurekebisha kasoro zilizokuwepo kwenye sheria ya sasa iliyomruhusu mchimbaji kuweza kupewa leseni kwa muda wa hadi miaka 25, hata kama taarifa ya upembusi yakinifu ingeonesha kuwa madini hayo yanaweza kuchimbwa kwa kipindi cha chini ya miaka 25.

Mheshimiwa Spika, katika eneo (d) linahusu uhamasishaji wa uongezaji thamani kwenye madini. Kifungu namba 59 kinaweka mazingira ya kuiwezesha Serikali, kupitia Waziri mwenye dhamana ya madini kwa kushauriana na mwenye leseni ya uchimbaji wa madini, kupanga kiwango cha madini kinachozalishwa nchini kitakachotengwa kwa ajili ya kuongezwa thamani. Aidha, kifungu cha 60 cha eneo (d), kinahusu uanzishwaji wa

leseni za uchenjuaji na usafishaji wa madini, yaani *processing, smelting and refining*. Hizi ni leseni mpya ambazo hazikuwemo kwenye sheria ya sasa ya madini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masharti ya leseni; baadhi ya leseni isipokuwa leseni za uchimbaji mdogo, biashara, uchenjuaji na usafishaji, zitatakiwa kuwasilisha utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa huduma na bidhaa za ndani na ajira kwa Watanzania, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa wataalamu wa kigeni kupisha wataalamu wa kizalendo kuendesha migodi kupitia utaratibu wa *succession plan and expatriate employees*. Sehemu ya tano inahusu leseni za biashara ya madini; sehemu hii inabainisha vifungu vinavyohusu maombi, masharti na utoaji wa leseni za biashara ya madini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita ya Muswada wa sheria, inahusu mrabaha na utaratibu wa ulipaji, ada ya uchambuzi wa madini ya vito, ada ya mwaka ya leseni na malipo mengineyo. Kifungu cha 87 katika sehemu ya sita ya Muswada, kinapendekeza mambo makuu mawili. Jambo la kwanza linalopendekezwa ni kubadilisha mfumo wa ukokotoaji wa mrabaha kutoka kwenye *netback value* na kuwa *gross value*. Hatua hii itaongeza mapato kwa kudhibiti udanganyifu wa gharama zinazotakiwa kuondolewa wakati wa kukokotoa mrabaha. Jambo la pili ni kuongeza viwango vya mrabaha kwa baadhi ya madini kama vile urani, kwa maana ya *uranium*, kutoka 3% hadi 5%. Dhahabu na madini mengine ya metali ya thamani kutoka 3% ilipo sasa hadi 4% na madini ya vito yaliyoongezwa thamani kutoka 0 hadi 1%.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba inahusu taarifa, usalama wa maeneo ya uchimbaji wa dhahabu na vito na haki ya uingiaji katika maeneo yenye leseni za madini na fidia kwa wanaopisha shughuli za uchimbaji wa madini.

Katika kifungu namba 97(b) cha sehemu hii, kinamtaka mwenye leseni au mwekezaji kutoa fidia stahiki, kujenga makazi mapya mbadala na kuwashamchia wale wanaopisha shughuli za uchimbaji wa madini kwenye makazi mapya yenye hadhi zaidi ya yale waliyokuanayo awali kulingana na Sheria ya Ardhi.

Sehemu ya Nane, inahusu utatuvi wa migogoro ambapo Kamishna wa Madini anaruhusiwa kutatta migogoro na utekelezaji wa maamuzi ya Kamishna.

Sehemu ya Tisa, inahusu masuala ya ujumla kuhusu usajili wa leseni za madini na uwasilishaji wa ushahidi kwa Kamishna wa Madini.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi, inahusu udhibiti wa madini ya mionzi, usajili wa kampuni ya madini katika Soko la Hisa, uhamishaji wa umiliki wa hisa za kampuni na mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya madini kutunga Kanuni. Katika Kifungu Na.109 cha sehemu hii, kinampa Waziri mwenye mamlaka baada ya kushauriana na mwenye leseni kupanga kiwango cha hisa za kampuni zinazotakiwa kuandikishwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa lengo la Watanzania kuweza kununua hisa hizo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja, inahusu kufutwa kwa Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na kuhifadhi maamuzi yaliyofanywa chini ya sheria inayofutwa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya sheria nyingine, kutokana na kutungwa na Sheria mpya ya Madini ya mwaka 2010, itahitajika kufanyika marekebisho katika sheria zingine zinazohusiana na usimamizi wa sekta ya madini nchini. Baadhi ya sheria hizo ni Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ambapo mfumo wa kodi katika sekta ya madini utarekebishesha ili uendane na utekelezaji wa sheria mpya inayopendekezwa, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 itakayoweka masharti ya wanaojenga migodi, kutoa fidia stahiki ikiwa ni pamoja na kujenga makazi mbadala yaliyo bora kwa wananchi wanaopisha shughuli za ujenzi wa migodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingine ni Sheria ya Mazingira, Sura 191, ili kuoanisha Sheria ya Madini na Sheria ya Mazingira itafanyiwa marekebisho ili kuweka mazingira maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Pia Sheria ya Ushuru na Forodha, Sura ya 403 ili kuweka vivutio kwa wawekezaji na kuhamasisha uwekezaji zaidi nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii, kukushukuru wewe binafsi lakini pia kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Shellukindo na Makamu wake Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Bunge lako Tukufu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ofisi yake kwa ujumla, Mwandishi Mkuu wa Sheria (*CPD*), Wizara zote na taasisi zote za Serikali na zisizo za kiserikali na wadau wote kwa ujumla katika sekta ya madini, kwa namna walivyotusaidia kutayarisha Muswada huu. (*Makofi*)

Aidha, nawashukuru wajumbe wote na wale ambao sio wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini lakini wameshiriki nasi kukamilisha matayarisho haya hasa wakati huu wa mkutano wa Bunge unaoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru sana kwa niaba ya wenzangu Wizarani na Serikali kwa ujumla, Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa msaada na mchango wake katika matayarisho haya. (*Makofi*)

Pia nawashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Adam Malima (Mb.), Katibu Mkuu wa Wizara yetu, Ndugu David Jairo ambaye naamini ameshatambulishwa tayari, Kamishna wa Madini, Dr. Dalali Kafumu, wataalam na watumishi wote wa Wizara yetu, kwa kazi kubwa waliyofanya wakati wa maandalizi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa muhimu, nakuomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za pekee, kwa mke wangu Blandina na familia yangu lakini pia waajiri wangu, wapiga kura wa Jimbo la Sengerema, kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada ambao umegawiwa, tunapendekeza kama utaratibu ulivyo, uendelee kusomwa pamoja na jedwali la marekebisho ambalo litawasilishwa kwako.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka katika kuwatambua walioshiriki, nafahamu umuhimu wa Kambi ya Upinzani na hasa Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Cheyo, Mheshimiwa Mnyaa, na Mheshimiwa Halima Mdee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine ni Mheshimiwa Dr. Mzindakaya lakini namkumbuka Mheshimiwa Makwetta, nafasi ulioitumia ya kuwa na sisi wakati wa maandalizi haya, hatutaisahau, tunaamini kwamba Taifa litaendelea kuchota busara na hekima pamoja na ushauri wenu.

Mheshimiwa Spika, haitawezekana kuwataja wote lakini inatosha kusema kwamba Muswada huu, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla umeandaliwa na Watanzania wenyewe kwa manufaa ya Watanzania lakini bila kusahau umuhimu wa wawekezaji. Kwa sababu ili tuendelee kuvuna rasilimali zetu lazima tuendelee kushirikiana. Sisi kama Taifa ambao pamoja na mambo mengine tumebarikiwa kuwa na rasilimali hizi lakini kwa vyovypote vile tunahitaji kushirikiana na wenzenetu ambao wamepiga hatua na hasa wenyе mitaji kuendelea kuvuna rasilimali kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niongee na ulimwengu kwamba sheria hii haikusudii kujenga mazingira ya kutisha kwa wawekezaji wakubwa ambao wanatoka nje ya nchi, ni Muswada endelevu ambao umetokana na kujifunza kwa kasoro ambazo tumezibaini tangu tulivyoanza kutumia Sheria ya mwaka 1998 ambayo ilikuwa imetanguliwa na Sera yake ya mwaka 1997. Kwa sababu tumewashirikisha wadau kwa kiwango kikubwa na kwa sababu pia tumezingatia uzoefu wa sheria zingine na leo kwa kuleta Muswada huu, tukijilinganisha na nchi zingine, bado tunasimama katika mazingira mazuri zaidi ya kuendelea kuwa kivutio. Tunaamini dunia itatuelewa, Watanzania watatuelewa kwa ajili ya uendelevu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa hakika huu ni Muswada wa kihistoria kabisa, narejea pongezi kwenu nyote kupitia kwako, kwa Wizara yako pamoja na Serikali kwa ujumla, ni Muswada wenyе mwelekeo mzuri kwa uchumi wetu. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ili tuweze kupokea maoni ya Kamati, Mheshimiwa William Shellukindo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutumia fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili kwa niaba ya Wajumbe wenzangu, niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010 (*The Mining Act, 2010*).

Mheshimiwa Spika, kuletwa kwa Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu, ni moja ya hatua muhimu ambayo Serikali imepiga katika kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikiikabili sekta ya madini nchini. Changamoto hizo ni pamoa na fungamanisho duni la sekta ya madini na sekta nyingine za uchumi, mchango mdogo wa sekta ya madini katika Pato la Taifa ikilinganishwa na ukuaji wake, uwezo mdogo wa Serikali katika kusimamia sekta ya madini na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba changamoto hizo kwa kiasi kikubwa zimetokana na ugumu uliobainika katika kutekeleza Sera ya Madini ya mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ambavyo kimsingi vyote hivyo vilikuwa vimepitwa na wakati. Hivyo basi, kuletwa kwa Muswada huu ni ishara tosha ya kuleta mapinduzi katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, madhumuni na umuhimu wa Muswada, Muswada huu unakusudia kufuta Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na kutunga Sheria Mpya ya Madini ya mwaka 2010 itakayofafanua masharti ya utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, biashara ya madini, utoaji wa leseni za madini, ulipaji wa mrahaba, kodi na ada mbalimbali na mambo mengine yanayohusu sekta ya madini. Muswada huu unakusudia kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Muswada huu ni muhimu sana kwa Taifa na nchi kwa ujumla na umekuja wakati muafaka na unatarajia kutoa majibu kwa maswali mengi yanayoulizwa na wananchi kuhusiana na mwenendo mzima wa sekta ya madini. Moja ya mambo ambayo yamekuwa yakilalamikiwa katika sekta hii, ni mchango mdogo wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa, (*Growth National Product (GDP)*) na mapato mbalimbali kwa Serikali yatokanayo na sekta hii. Aidha, wananchi wengi wanaozunguka maeneo ya migodi kutonufaika kabisa na uwepo wa rasilimali hiyo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, masuala mengi yaliyoandikwa katika Muswada huu, yamezingatia changamoto na maoni mbalimbali yaliyotolewa kuititia Kamati mbalimbali zilizoundwa kwa lengo la kutoa maoni kuhusu Migogoro, Sera ya Madini, Mikataba, Mfumo wa Kodi, Usimamizi wa Sekta ya Madini, Ushiriki wa Serikali katika Migodi, Umiliki wa Migodi, Mikataba ya Madini, Uharibifu wa Mazingira, Vivutio kwa Wawekezaji, Ulipaji wa Fidia kwa Wananchi wanaopisha migodi, hali ya Wachimbaji Wadogo, Suala la Uchimbaji wa Madini ya Vito n.k.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba Muswada huu umekuja kwa Hati ya Dharura. Pamoja na kuletwa kwa njia hiyo, haukuibana Kamati yangu kushindwa kuwaita wadau muhimu ili kuweza kuujadili na kupata maoni ya kuboresha Muswada huu. Muswada huu ulichambuliwa kwa siku tano katika Vikao vilivyofanyika hapa Dodoma tarehe 16, 18, 19, 20 na 21 Aprili, 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Aprili, 2010, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William M. Ngeleja, aliwasilisha Muswada kwenye Kamati kwa kueleza maudhui ya Muswada na kuchambua maeneo mbalimbali yaliyobainika katika Muswada huu pamoja na jinsi maudhui yalivyoshughulikiwa. Wajumbe walipata fursa ya kutoa maoni ya jumla kuhusiana na Muswada ulio mbele yetu.

Tarehe 18 Aprili, 2010 kilifanyika Kikao cha Kamati, Wizara na Wadau wa Sekta ya Madini. Wadau mbalimbali wapatao 107, walishiriki katika Kikao hicho na walipata fursa ya kutoa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia kuboresha Muswada huu hadi kufikia hatua ulivyo sasa. Tunawashukuru Sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue wadau wote waliofika mbele ya Kamati yangu kama ifuatavyo:-

*Tanzania Chamber of Minerals and Energy; Civil Society Organizations; Legal and Human Rights Centre (LHRC); TAMICO; TAMIDA; Revenue Watch Institute (RWI); Policy Forum; Umoja wa Wachimbaji Wadogo wa Tanzanite Mererani (MAREMA); Watoto/Wajukuu wa Waasisi wa Wachimbaji Wadogo; Asasi za Kidini (FBO); DODEA na Wachimbaji mmoja mmoja hapa nchini. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 19, 20 na 21 Aprili, 2010, Kamati ilikutana na Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Watendaji wa Wizara hii, kwa lengo la kujadili kwa undani vipengele vyote vilivyomo katika Muswada na kuweza kuchambua maoni mbalimbali yaliyopokelewa kutoka kwa wadau. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kiwango kikubwa, maoni yaliyotolewa katika mijadala hiyo yamezingatiwa katika mabadiliko ya Muswada unaowasilishwa Bungeni leo na ndiyo maana hata jedwali la mabadiliko hayo imebidi lichukue muda kilitayarisha kwa sababu kazi hii tuliimaliza jana saa kumi na mbili.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili Muswada huu, Kamati ilihitaji kupata ufanuzi juu ya masuala mbalimbali ambayo Bunge lako Tukufu liliazimia mara baada ya kujadili Taarifa ya Bomani kuhusu Usimamizi Bora wa Sekta ya Madini na ile ya Kamati yangu kuhusiana na hoja hiyo hiyo. Waziri wa Nishati na Madini, alitoa maelezo kwa Kamati yangu kuhusu namna ambavyo hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mijadala wa Taarifa ya Bomani hapa Bungeni zilivyozingatiwa wakati wa mchakato mzima wa maandalizi ya Muswada huu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa hoja hizo zimezingatiwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utafutaji wa madini zimekuwa zikishamiri siku hadi siku kutokana na kukua kwa mahitaji na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kamati

yangu imefarijika na kuridhika kwamba Muswada huu unaolenga kuleta mapinduzi na maendeleo katika sekta ya madini kwa Taifa, sasa unawasilishwa Bungeni. Kulikuwa na malalamiko mengi kwamba unachelewa, unachelewa lakini sasa uko mbele yetu na tunaishukuru Serikali kwa kutumiza haja hii. Kweli Wahenga walisema “hayawi hayawi, sasa yamekuwa”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilitafakari kwa undani Vifungu mbalimbali vilivyomo katika Muswada huu kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 8(2), kinatoa kipaumbele kwa Leseni za Awali (*Primary Mining Licences*) kutolewa kwa Watanzania tu. Kamati imefarijika na kuwepo kwa kipengele hiki kwa kuwa kinatoa fursa pana kwa Watanzania kushiriki vizuri katika uwekezaji ndani ya sekta ya madini bila kuwa na ushindani ambao unawazidi nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tafakari ya undani ilifanyika kwa Kifungu cha 23 kinachopendekeza kuundwa kwa Bodi ya Ushauri ya Madini (*Mining Advisory Board*). Katika hili, Kamati inashauri kuwa Bodi hiyo iwepo kwa sasa lakini kwa hapo baadaye Serikali izingatie kuundwa kwa Mamlaka ya Madini (*Mining Authority*) kama ilivyopendekezwa kwenye Taarifa ya Boman na Kamati yangu, kuhusu kuanzishwa kwa Mamlaka hiyo. Kamati inatambua kwamba uanzishaji wa Mamlaka hiyo unahitaji mchakato wa kuzingatia mambo mengi ya kisera na kiutendaji, kwa hiyo, bado Kamati inashauri kuwa ushauri uliotolewa wa kuanzishwa kwa Mamlaka hiyo, ni muhimu kwa kuwa utasidia kuweka usimamizi bora wa sekta hii pindi itakapoanzishwa. Nashukuru sana kwamba na Mheshimiwa Waziri ametoa maeleo ya kutosha jinsi ambavyo suala hili litashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Madini na Sheria itamke namna ambavyo Mfuko huo utakusanya fedha kwa ajili ya kuchangia Mfuko unaopendekezwa. Kamati inatambua kwamba Mfuko huo ni muhimu hasa katika kuendeleza Wachimbaji Wadogo pamoja na mambo mengine hasa kwa ajili ya kuwapa mafunzo kuwajengea uwezo wa kuandaa miradi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tafakari ya undani ilifanyika kwa Kifungu cha 8(3) kinachopendekeza Uchimbaji wa Madini ya Vito (*Gemstones*) kufanywa na Watanzania tu. Kamati imefarijika na kuwepo kwa Kifungu hiki kwa kuwa pamoja na marekebisho yaliyoletwa kwenye Kifungu hiki na Kifungu cha 8(4), yanatoa fursa pia kwa mzalendo kuingia ubia na asiye raia wa Tanzania kushiriki kuititia leseni za Watanzania kwa ubia. Kipaumbele cha uchimbaji wa madini ya vito kuachwa ufanywe kwa Watanzania tu, kunatekeleza pia matakwa ya Sera mpya ya Madini ambayo imepitishwa na Serikali na hakulengi kuwaondoa Wawekezaji wa Kigeni kuwekeza katika uchimbaji huu, maana wanayofursa kuititia ubia na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijadili kwa upana zaidi suala la umiliki wa eneo la Kilometra za mraba zisizozidi 2000 kwa Mtu Binafsi, Ushirika, Kampuni, Wabia au Wakurugenzi wenye Leseni za utafutaji zisizozidi 20 kama ilivyoelezwa kwenye

Kifungu cha 8(6). Kamati iliridhika na maelezo yaliyotolewa kwamba kuna baadhi ya watafutaji ambao hufanya utafutaji kwa njia za kisasa mfano kutumia ndege na vifaa vingine, hivyo kwa utafutaji wa aina hiyo, Kamati iliafiki eneo kama hilo ni sahihi kuweza kutumika kwa ufanisi zaidi katika utafutaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefarijika na Kifungu cha 29, kinachopendekeza suala la utoaji wa Leseni za Utafutaji wa Madini katika maeneo yatakayotengwa kwa ajili hiyo na kufanyika kwa tenda. Aidha, Kifungu cha 15 pia kinapendekeza maombi ya Haki za Madini (*Mineral Rights*) kufanyika kwa njia ya tenda. Kamati inaamini kuwa hatua hii ni ya kimapinduzi na itaongeza uwazi katika utoaji wa Leseni kwa kutumia njia ya tenda.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imejadili kwa undani suala la Madini ya Vito ya Tanzanite ambayo yanapatikana Tanzania pekee, madini hayo kuwa miongoni mwa madini ambayo kwa mujibu wa Kifungu cha 17 cha Muswada huu kuwa yawe maalum (*specified*). Vilevile, inashauriwa kuwa eneo la Mererani ambako madini haya yanapatikana liwekewe uzio (*fence*) ili kuzuiwa utoroshaji wa madini hayo unaofanyika kwa njia za kificho au njia za panya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 25, kinapendekeza kuzuia utoaji wa taarifa za wamiliki leseni za madini isipokuwa kwa ruksa ya mwenye leseni. Kamati yangu imeridhika na pendekezo hili na kwamba dhana ya kuzuia kutoa taarifa kwa utaratibu wa Sheria ya *Extractive Industry Transparency Initiative (EITI)*, itakayoanzishwa, haitajitokeza kwa kuwa *EITI* itakuwa na sheria yake inayojitegemea. Kifungu hiki kimeipa faraja Kamati na hivyo fursa ya kuanzishwa kwa Sheria ya *EITI* haitakinzana na matakwa ya Kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 23, kinachoainisha idadi ya Wajumbe kwenye Bodi ya Ushauri ya Madini (*MAB*), Kamati imekiboresha Kifungu hiki kwa kuongeza ushiriki wa Mwakilishi wa Wachimbaji Wadogo na Mwakilishi wa Wafanyabiashara ya Madini ya Vito (*TAMIDA*).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umezingatia pia masuala ya mtikisiko wa kiuchumi ambayo yanaweza kutokea wakati mwekezaji yupo katika hatua za kuwekeza katika eneo husika. Hivyo Kifungu cha 38(4), kinampa mamlaka Waziri kuweza kumtaka mwekezaji kuwasilisha ripoti yake ya upembuzi yakinifu na tathimini ya maendeleo ya mradi husika na kuweza kushauriana na Bodi juu ya kutoa bakizo la (*retention*) ya leseni kwa mwekezaji huyo. Kamati imeridhika na angalizo linalopendekezwa katika Kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, utata ulijitokeza pia katika Kifungu cha 10(2), kinachohusu suala la hisa zisizo na malipo (*free carried interest*). Kamati imefarijika na pendekezo la marekebisho yaliyotolewa kwenye Kifungu hiki ya kuruhusu kuwepo kwa majadiliano baina ya pande mbili yaani mwekezaji na Serikali na utazingatia aina ya madini na kiasi cha kuwekeza. Nashukuru Mheshimiwa waziri amelifafanua vizuri hili lilikuwa limeleta utata kwamba pengine sasa ni aina fulani ya ubabe kumlazimisha mtu kwamba utoe *free*

*carried interest* lakini kwa kujadiliana limekaa vizuri sana na itakuwa ni katika masuala ya kuongoza uchumi kwa njia ya demokrasia.

Mheshimiwa Spika, suala la mrahaba (*royalty*) lizingatie mapendekezo yaliyotolewa kwenye Taarifa ya Bomani ambayo imechambua kwa kina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa suala la usimamizi wa mazingira chini ya sheria hii litazingatiwa kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Aidha, Kifungu cha 47(d), kimeboreshwa na kumtaka mwenye leseni kuwa na *Closure Bonds*, hili tumeshindwa kupata neno la Kiswahili na hatimaye kuliacha hivyo hivyo, kabla ya kufunga mgodi. Kamati imefarijika na pendekozo hili kwa kuwa litasaidia urejeshaji wa mazingira pindi mwekezaji atakapokuwa amemaliza shughuli zake za uchimbaji kuliko ikiachwa tu hivi hivi hatimaye atafunga mgodi atatuachia mashimo na kazi hiyo itabidi Serikali ifanye.

Mheshimiwa Spika, vifungu mbalimbali katika Muswada huu vinapendekeza, mwekezaji kuwasilisha mpango wa ununuzi wa bidhaa zinazoweza kupatikana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iwapo vitakidhi ubora na viwango stahili. Kamati imefarijika na kuwepo kwa Kifungu hiki kwa kuwa kinatoa kipaumbele kwa bidhaa za ndani kuuzwa kwa wingi na hivyo kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzishwa kwa Tume Huru ya Usuluhihi (*Independent Mining Appeal Tribunal*), Kamati inashauri kuwa suala hili ni muhimu na Serikali ianze mchakato wa kuanzisha *Tribunal* hiyo kuliko kutegemea busara za Kamishna wa Madini.

Mheshimiwa Spika, suala la utoaji wa leseni chini ya sheria hii inayopendekezwa limeboreshwa na kumwezesha *Zonal Officer* kutoa leseni za awali *Primary Mining Licences* chini ya Kifungu 54 na hivyo kupunguza kazi hii ambayo awali ilikuwa ikifanywa na Kamishna wa Madini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuunda Tume mbalimbali za kushauri kuhusu usimamizi bora wa sekta ya madini, kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zinazohusiana moja kwa moja na sekta hii, kutunga Sera Mpya ya Madini ya mwaka 2009 na hatimaye pendekozo la Sheria Mpya ya Madini ambayo tunaijadili leo hii. Ni matumaini ya Kamati yangu, Bunge lako Tukufu na wananchi wa Tanzania kwa ujumla kuwa, mabadiliko yote haya yatasaidia kuboresha usimamizi wa sekta hii ili iweze kuchangia zaidi katika kukuza uchumi wa Taifa, kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Nitumie fursa hii kumshukuru pia Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William M. Ngeleja (Mb) na Naibu wake Mheshimiwa Adam K. Malima (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu David K. Jairo, Kamishna wa Madini, Dr. Peter Kafumu na Watendaji wote wa Wizara

ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukijadili Muswada huu. Napenda kuwashukuru pia Waandishi wa Sheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa msaada wa kisheria walioutoa katika kutoa ufanuzi na marekebisho ya vifungu vilivyokuwa na utata katika Muswada huu na ninaamini kwamba kazi hiyo itafanyika vilevile kwa ufanisi ili Waheshimiwa Wabunge nao waweze kuelewa vizuri marekebisho ambayo tumefanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuchambua Muswada huu na kwa ushirikiano wao walioutoa wakati wa kuandaa maoni haya. Napenda kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti na Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Faida M. Bakar, Mheshimiwa Lolesia J.M. Bukwimba, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Yahya K. Issa, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Rita Louis Mlaki, Mheshimiwa Mohammed H.J. Mnyaa, Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mheshimiwa Dk. James A. Msekela, Mheshimiwa Omar Shekha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Charles N. Mwera, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Christopher O. Ole Sendeka na Mheshimiwa Mohammed S. Sinani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Andrew Chenge (Mb), kwa kukaa na Kamati yangu muda wote kuanzia siku ya kwanza mpaka siku ya tano, napenda kumshukuru sana, mchango wake umekuwa wa manufaa makubwa sana. Vilevile Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto (Mb) ambaye kwa bahati nzuri alishiriki kwenye Kamati ya Mheshimiwa Jaji Mstaafu Bomani, naye michango yake imetusaidia sana kurejea mambo ambayo yalitolewa kwenye taarifa ile. Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, (Mb), Mheshimiwa Halima Mdee (Mb), Mheshimiwa John Cheyo (Mb), Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya (Mb), Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu (Mb), Mheshimiwa George Simbachawene (Mb), Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni (Mb), Mheshimiwa Charles M. Kajege (Mb), Mheshimiwa Siraju J. kaboyonga (Mb) na Mheshimiwa Jackson Makweta (Mb) na wengine wote ambao nimewasahau, kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukijadili Muswada ulio mbele yetu leo. Shukrani za pekee pia ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wengine wakiwemo Mawaziri kwa kututia nia na kutuhimiza kwamba tufanye kazi hiyo kwa umakini na tumejitahidi kuzingatia ushauri wao, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati, kwa Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashililah, pamoja na makatibu wa Kamati hii Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Stella S. Bwimbo, kwa kuihudumia Kamati kwa ufanisi wakati wote na kuandaa Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba Bunge lako Tukufu lijadili na likubali kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti William Shellukindo, sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika masuala haya ya Nishati na Madini ambaye atakuwa ni Mbunge Ismail Jussa Ladhu.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU (K.n.y. MHE. MOHAMED HABIB MNYAA, MSEMAJI MKUU WA UPINZANI, WIZARA YA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Madini wa mwaka 2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007. Nafanya hivi kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa ambaye amepata dharura.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini pamoja na wajumbe wake wote, kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya katika kuhakikisha kuwa Muswada wa Sheria Mpya ya Madini, unakamilika na kuletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa nimetenda haki kama sitotambua kazi iliyofanywa na Mheshimiwa William Ngeleja (Mb), Waziri, Mheshimiwa Adam Malima (Mb), Naibu Waziri, Ndugu David Jairo, Katibu Mkuu na Dr. Peter Kafumu, Kamishna wa Madini pamoja na timu nzima ya watendaji katika Wizara kwa kazi kubwa waliyoifanya kuandaa Muswada huu. Natambua pia mchango wa wadau wote walioshiriki kwa njia moja au nytingine katika kufanikisha kuwepo kwa Muswada huu katika sura hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa kauli hapa Bungeni juu ya umuhimu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli zote rasmi za Kiserikali. Hata hivyo, ni masikitiko ya Kambi ya Upinzani kwamba pamoja na umuhimu mkubwa wa Muswada huu wa madini kwa wachimbaji wadogo ambao idadi kubwa hawaielewi vizuri lugha ya Kiingereza, Serikali haikufanya juhudzi zozote za kuhakikisha Muswada huu unatolewa pia katika lugha ya Kiswahili. Hili linaonyesha tu kuwa matamko kama haya yanayohusu matumizi na ukuzaji wa lugha hii ya Taifa yanaishia kuwa ya kisiasa zaidi kuliko ya kisera yanayolenga utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kabla ya kupitia vifungu, nieleze mambo ya jumla kwanza.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini hapa nchini imegubikwa na changamoto kubwa tatu. Changamoto hizi ndiyo chanzo cha kelele nyingi sana na malalamiko ya wananchi kuhusu Sekta ya Madini. Malalamiko na kelele hizi ndiyo yalipelekea kuundwa kwa Kamati mbalimbali za kuishughulikia sekta hii. Miiongoni mwetu kuna Wabunge

ambao siku zote wamekuwa wakisimama kidete kutaka changamoto hizi ziangaliwe. Kambi ya Upinzani katika Bunge hili la Tisa, imekuwa ikieleza kuhusu changamoto hizi. Serikali nayo katika madhumuni na sababu za kuleta Muswada huu wa sheria, imerejea changamoto hizi. Changamoto hizi ni:-

- Kwamba Sekta ya Madini haina mahusiano ya kutosha na sekta nydingine za uchumi (*forwards and backwards linkages*) na hivyo kupelekea kutochochea ukuaji wa sekta nydingine (*low integration to the economy*). Madhara makubwa ya changamoto hii ni kwamba, sekta inakuwa *enclave* na uwekezaji wote unakuwa hauna maana kubwa katika uchumi wa Taifa na hivyo kupunguza umasikini;

- Kwamba Sekta ya Madini imekuwa na mchango mdogo sana katika Pato la Taifa (*GDP*) ukilinganisha na kasi ya ukuaji wa sekta yenye na hata mchango wa sekta katika mauzo ya nje (*exports*). Madhara ya hali hii ni kuwa uchumi unabaki kukua hewani lakini hauwafikii wala hauwanufaishi wananchi wetu walio wengi. Sekta ya Madini ilichangia 3.8% ya Pato la Taifa (*GDP*) mwaka 2008 ilihali inachangia 40% ya mauzo ya nje na inakuwa kwa wastani wa 10% tokea mwaka 2000; na

- Kwamba Sekta ya Madini haina usimamizi mzuri, hali ambayo inapelekea kuingia mikataba ambayo haina maslahi kwa Taifa, kushindwa kusimamia mikataba hiyo na hata kushindwa kutatua migogoro ndani ya sekta yenye. Madhara ya changamoto hii ni hisia za ufisadi na mapato ya nchi kupotea.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Madini itakayotungwa na Bunge lako Tukufu utakuwa wa maana iwapo tu utakuwa umejibu changamoto hizi kikamilifu. Muswada huu ulio mbele yetu tunaupima kwa vigezo vya changamoto hizi. Uamuza wa kukubali ama kukataa Muswada huu, unapaswa kutokana na vigezo hivi vya changamoto ya sekta.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba tuuchambue Muswada huu kwa vigezo hivi kama ifuatavyo. Kwanza, fungamano na sekta nydingine za uchumi. Changamoto hii siyo rahisi kuonekana waziwazi katika Muswada wa Sheria hii. Hii ni changamoto inayoelezwa vizuri zaidi na sera za Serikali na mikakati ya kuendeleza sekta. Hata hivyo, Muswada unapaswa kuonyesha ni jinsi gani sekta ya madini itaungana na sekta nydingine za uchumi. Hapa tunazungumzia zaidi upande wa ununuzi unaofanywa na makampuni ya madini kwa vifaa vya ndani ya nchi. Muswada (kufuatia marekebisho yaliyowasilishwa) umeweka vipengele vya kuhakikisha ununuzi unafanyika hapa nchini. Imekuwa ni jambo la kawaida sasa kusikia kwamba makampuni ya madini yananunua bidhaa kutoka nje ya nchi ilihali bidhaa hizo zinapatikana hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunapenda kuwakumbusha Watazania kwamba fursa zilizopo zinapaswa zitumike ipasavyo maana kuna fursa nyingi ambazo zinapotea bure. Kwa mfano, kuna sababu gani kwa Kampuni ya *Geita Gold Mine (GGM)* kununua nyama kutoka Kenya wakati ng'ombe wanatoka Geita? Hivi kweli hakuna mjasiriamali wa Tanzania anayeweza kuwekeza katika machinjio pale Geita ili kupata soko hili? Kwa nini Serikali haiielekezi wananchi kuona fursa hizi? Hili ni kosa la wawekezaji au kutojiandaa kwetu mpaka jirani zetu wanachukua fursa hizi.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la vivutio vinavyotolewa katika sekta ya madini kubagua makampuni ya ndani yanayofanya kazi ya kuchimba madini (*local contractors*). Hii hupelekeea makampuni mengi kuchimba madini wao wenyewe (*owner mining*) na hivyo kuzuia fungamano katika uchumi kwani iwapo kampuni zitatumia kampuni za ndani kuchimba, fedha inabaki ndani na hivyo kuchochaea uchumi wetu na wakichimba wenyewe, fedha hizo hurudi kwao. Kambi ya Upinzani, inashauri kuwa iwapo kuna motisha (*incentives*) zozote ambazo Serikali itatoa kwa wawekezaji, basi motisha hizo zinapaswa ziende pia kwa wakandarasi wa ndani ili kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji kutumia wakandarasi hao wa ndani.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la kuzingatia ni uzalishaji wa umeme katika migodi. Makampuni mengi hutumia umeme wao wenyewe kwa kuwa *TANESCO* bado hajawenza kuzalisha umeme na kuuza kwenye migodi. Hili nalo linapunguza fungamano na sekta nyingine za uchumi. *TANESCO* wanapoteza soko la zaidi ya shilingi 150 bilioni kwa kushindwa kusambaza umeme wa kutosha na wa uhakika kwenye migodi yote nchini. Kwa kuwa umeme unatumika katika mchakato mzima wa uzalishaji kwenye migodi unatokana na majenereta, ambapo mafuta ya kusukuma mitambo hiyo yanapatiwa msamaha wa ushuru, sasa basi ni kwa vipi *TANESCO* itasaidiwa ili iwe ndiyo msambazaji mkuu wa umeme unaotakiwa katika uzalishaji? Kambi ya Upinzani, inadhani hili linaweza kufanyika sasa kupitia mikataba ya uendelezaji madini yaani *MDAs* inayotakiwa kuingiwa kati ya makampuni na Serikali. Kambi ya Upinzani inaihimiza Serikali kuhakikisha kuwa migodi yote iliyopo inatumia umeme kutoka *TANESCO* na vile vile kwa migodi mipyä itakayoanza moja ya sharti la kufunguliwa kwa mgodi liwe ni mgodi huo kuwa na umeme kutoka Shirika la *TANESCO* hata kama itabidi kuingia mikataba maalumu kuwezesha hili kati ya *TANESCO* na makampuni hayo ya madini.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya sekta kuchangia katika ukuaji wa pato la Taifa. Changamoto ya pili juu ya uchangiaji katika *GDP* inajibiwa na changamoto nyingine mbili. Sekta ikiwa na mahusiano mazuri na sekta nyingine basi hupelekeea mchango wake katika uchumi kukua. Vile vile sekta ikisimamiwa vizuri, hupelekeea mchango mkubwa katika Pato la Taifa. Hivyo ili sekta ya madini iweze kufikia lengo la kuchangia 10% katika pato la Taifa kama ilivyo katika *VISION 2025*, ni muhimu sana vipengele vya sheria vinavyohakikisha changamoto ya kwanza na ya tatu vipewe uzito unaostahili katika sheria hii tunayoelkea kuitunga.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya uwezo wa Serikali kusimamia sekta. Changamoto ya tatu ni kuongeza uwezo wa Serikali katika kusimamia sekta ya madini. Hili kwa kweli Muswada huu umeshindwa kulizingatia kwani badala ya kuunda na kuiimarisha taasisi ya kusimamia sekta, Serikali imetunga sheria ya kumuimarisha mtu ambaye ni Kamishna na Waziri mwenye dhamana. Hapa dhana nzima ya kuiwezesha Serikali kuwa na uwezo wa kusimamia na kuiendeleza sekta inaondoka na hivyo inaweza kuturudisha nyuma kama ilivyo kuwa kwa mamlaka aliyokuwa amepewa Mkurugenzi wa Wanyamaporí wakati ule. Bunge lako Tukufu linakumbuka kuwa, tulipokuwa tunatunga Sheria ya Wanyamaporí ya mwaka 2009, tuliweza kuondoa tabia hii ya kurundika

mamlaka kwa mtu mmoja na badala yake tukaweka Mamlaka ya Wanyamaporini nchini. Kambi ya Upinzani inarejea kutaka suala hili lizingatiwe pia katika Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni, inapenda kuwakumbusha Wabunge na Watanzania kwa ujumla ya kwamba hata kama sekta inafungamana namna gani na uchumi, kama usimamizi wake ni mbovu ni chanzo cha rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na hata kudumaa kwa sekta. Hivyo, tunasisitiza umuhimu wa kuanzisha Mamlaka ya Madini nchini yenye nguvu ya kusimamia sekta, kusimamia mikataba (*contracts management*) na kuendeleza sekta.

Mheshimiwa Spika, Tanzania haiwezi kuendelea kwa kujenga watu wenyewe nguvu, bali itaendelea kwa kujenga taasisi zenyewe nguvu. Muswada huu unamjenga Waziri mwenye nguvu na Kamishna mwenye nguvu na hiyo inaweza kuwa chanzo kikubwa cha ufisadi kwani kama alivyowahi kusema Lord Acton wa Uingereza, '*Absolute power tends to corrupt absolutely*' yaani madaraka yasiyo na kikomo hufisadi bila ya kikomo. Kambi ya Upinzani inataka Taasisi yenye nguvu kusimamia sekta ya Madini kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Rais ya kupitia Sekta ya Madini yaani (Kamati ya Bomani).

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani hivi sasa zimeanzisha Mifuko ya Utajiri wa Dola (*Sovereign Wealth Funds*) kutokana na sekta zao za rasilimali. Kamati ya Bomani pia ilipendekeza hili katika Taarifa yake. Kwa jinsi Muswada ulivyoletwa, inaonekana wazi Serikali imekataa kulitekeleza pendekezo hili. Hii inaonyesha dhahiri jinsi ambavyo Serikali haina nia ya kuhakikisha utajiri wetu unatumika vizuri kwa manufaa ya Taifa. Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Madini ambao ungeundwa kutokana na mapato yanayotokana na fedha za mrahaba ungeweza kusaidia sana kuwekeza katika miradi mikubwa ya maendeleo. Kambi ya Upinzani inataka Serikali kulikubali pendekezo hili kwani ni jambo jema.

Mheshimiwa Spika, sasa nikigeukia baadhi ya vifungu vya Muswada huu ambavyo Kambi ya Upinzani inapenda kuvitolea maoni mahsus, naomba nianze na kifungu kipyaa cha 10(2) kilichopo katika jedwali la marekebisho kinachosema na nanukuu "*The level of free carried interest and public equity participation in any mining operations under special mining license shall be negotiated upon between the Government and mineral right holder...*".

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashindwa kuamini kama kweli Serikali itaweza kuendesha majadiliano na mwekezaji bila ya kuwepo kwa mamlaka maalum husika. Hii inatokana na ukweli kuwa wale wote wanaoendesha majadiliano huteuliwa maalum kwa kazi hiyo na kazi ikimalizika na timu ya majadiliano inavunjwa. Tumejionea yaliyotokea katika majadiliano na *IPTL*, *SONGAS*, *RICHMOND* na kadhalika. Hii inawafanya Watanzania kwa ujumla kuwa na hisia mbaya (*bad feelings*) kuhusiana na timu za majadiliano za Serikali (*Government Negotiating Teams*) zinazoundwa. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa ni lazima kuwepo na mamlaka iliyoundwa kisheria ambayo itafanya kazi hiyo kwani mamlaka hiyo itabeba

dhamana kwa niaba ya Watanzania kuhoji yale ambayo wawekezaji watakuwa wamekwenda kinyume na hata kuweza kuwashitaki.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19(3) kinazungumzia Waziri kwa kushauriana na Kamishna wa Madini kufanya uteuzi wa Watendaji. Hapa jambo ambalo tunaona limesahafulika ni nafasi ya Katibu Mkuu wa Wizara. Kambi ya Upinzani, inauliza nafasi ya Katibu Mkuu katika kadhia nzima ya kiutendaji itakuwa wapi? Inaonyesha kuwa majukumu yote yamechukuliwa na Waziri pamoja na Kamishna wa Madini. Hii ni kukiuka ngazi za madaraka katika mlolongo mzima wa kiutendaji na inaweza kuleta mivutano Wizarani inayoweza kuepukwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla vifungu vingi vimempa Kamishna wa Madini nguvu kubwa sana, jambo ambalo ni hatari. Hii ni moja ya sababu ambazo tunaona zinahitaji kuwepo kwa Mamlaka ya Udhibiti (*Regulatory Authority*) ya sekta ya madini. Katika dhana nzima ya utawala bora na uwajibikaji inatakiwa kuiimarisha Taasisi iwe na nguvu na siyo kumuimarisha mtu kama Muswada huu unavyofanya. Hii ni hatari kwa Bunge kutunga sheria ya kujenga watu badala ya kutunga sheria ya kujenga Taasisi.

Mheshimiwa Spika, haya yanatokana na ukweli kwamba katika Kifungu cha 103 na naomba kunukuu:-

*“The Commissioner may send a copy, certified under his hand, of any order made by him to any civil court with the local limits of whose jurisdiction the subject matter of the order is situated, and the civil court shall enforce the order of the Commissioner in the same manner in which it would enforce its own order”.*

Mheshimiwa Spika, nguvu hii ya hadi Kamishna kuingia katika mamlaka ya Mahakama ya kutoa amri kwa Mahakama kuitaka ikubali kutekeleza/kuidhinisha maamuzi ambayo yeye ameyachukua kama vile yametolewa na Mahakama hiyo yanakiuka kabisa misingi ya utawala wa sheria. Kambi ya Upinzani, inaomba tupatiwe ufanuzi kuhusu nguvu hii ya ajabu ambayo anakusudiwa kupewa Kamishna.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 21 kinaelezea kazi za wakala wa *geological survey* kwa kirefu, lakini kitu cha kushangaza Muswada hausemi lolote kuhusiana na majukumu ya Wakala wa Ukaguzi wa Madini nchini (*TMAA*) ambao wametajwa katika Sera ya Madini ya mwaka 2009. Kambi ya Upinzani inataki sheria hii tunayoipitisha itambue kuwepo kwa Wakala huyu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 23(3) kinahusu muundo wa Bodi ya Ushauri. Bodi inaundwa na Wajumbe tisa akiwemo, baada ya marekebisho yaliyoletwa, mwakilishi wa jumuiya za wachimbaji wadogo, lakini kati ya hao wote hakuna hata mmoja anayetoka katika Mashirika yasiyo ya Kiserikali na asasi na watu ambao wamekuwa katika harakati za kuifanya sekta ya madini ilete manufaa kwa nchi na wananchi wote. Wajumbe sita waliobaki ni watumishi wa Serikali. Kambi ya Upinzani kwa hili inaona kuwa uwakilishi huu unaifanya Bodi ya Ushauri kuwa ni tegemezi na hivyo haiwezi kufanya kazi yake ya kutoa ushauri kikamilifu kuhusiana na tasnia nzima

ya madini. Huu ni udhaifu wa wazi na iwapo tutauacha bila ya kuurekebisha, Watanzania watahoji Bunge lilipitishaje uanzishwaji wa Bodi hii? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 23(7) kinasema kuwa na nanukuu:-

*“The Minister may amend any provision of the Schedule”.*

Mheshimiwa Spika, jedwali linalozungumziwa ni jedwali la kwanza ambalo linatoa taratibu na miongozo jinsi Bodi ya Ushauri itakavyofanya kazi kwa ujumla. Hivyo basi, kifungu kinachotajwa kinasema kuwa Waziri anaweza kubadilisha kifungu chochote katika jedwali kadri anavyoona yeye inafaa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kifungu hiki kinaweza kutumiwa vibaya na kusababisha madhara makubwa kwa nchi na pia kinadhalilisha kuwepo kwa Bodi nzima ya Ushauri. Tunaitaka Serikali ikifute Kifungu hiki cha 23(7) kwani kinatoa madaraka ya kudhalilisha Wajumbe wa Bodi ya Ushauri inayoundwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 23(8) kinachosema kuwa Bodi ya Ushauri lazima iwasilishe ushauri wake kwa Waziri na Waziri anaweza kutozingatia ushauri huo, lakini kabla ya kuachana na ushauri huo kwanza autangaze katika magazeti. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa Bodi inaundwa na timu ya wataalamu mbalimbali na ushauri wanaoutoa ni dhahiri unakuwa umefanyiwa utafiti wa kutosha. Hivyo basi, sheria kutamka kuwa Waziri anaweza kutokuzingatia ushauri huo, ni njia nyingine ya kuonyesha kuwa Bunge linatunga sheria ya kutothamini ushauri wa mamlaka ambayo inaundwa kwa sheria. Tukiridhia hili, itakuwa ni aibu kwa upande wa Bunge na Serikali iliyouleta Muswada huu. Kambi ya Upinzani inauliza ni kwa nini Waziri asitoe sababu za kukataa ushauri huo na pia kwa nini atumie fedha za walipa kodi kutangaza ushauri huo wakati hautatumiwa?

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 25 kinazungumzia usiri wa kutoa taarifa zinazohusiana na shughuli za madini na kinaendana na kifungu cha 100 ambacho kinaelekeza aina ya taarifa zinazotakiwa kuwa ni siri kwa kampuni, ambazo ni zile taarifa za wataalamu kama jedwali la pili linavyooleza. Lakini kifungu hicho kimekuwa na maelezo mengi kiasi kwamba kinaweza kutumika kuficha mambo hata yale yanayotakiwa kuwekwa wazi kwa umma.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaungana na wadau kuhusiana na mkakati wa kuweka uwazi kwenye kile ambacho kampuni inazalisha na kuilipa Serikali na Serikali kuweka wazi kile inachopokea (*Extractive Industries Transparency Initiative - EITI*) ili kuondosha dhana au hisia za kuwepo malipo yasiyokubalika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 28 kinahusiana na maombi ya leseni za utafutaji (*application for prospecting licence*), kifungu kidogo cha (1), kuna aina tofauti za madini kama vile kifungu (a), (b).... hadi (f), suala kama lilivyotolewa na wadau linabaki kuwa ikitokea Makampuni tofauti yenye leseni tofauti za madini tofauti lakini eneo ni moja, hapo itakuwaje? Nani atakuwa na haki? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kukiangalia

kwa makini kifungu hiki kwani kinaweza kuleta mtafaruku mkubwa sana mionganoni mwa Makampuni yenyenye leseni za utafutaji kwa aina tofauti za madini.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 87 kinahusu masuala ya mrabaha ambapo kinataka msingi wa malipo ya mrabaha utokane na “*gross value*” ya madini husika. Kambi ya Upinzani, inakubali kuwa mabadiliko haya yataongeza mapato kiasi fulani kwa Serikali lakini tunaamini hilo pekee halipaswi kuwa msingi wa mabadiliko. Ni maoni yetu kwamba mbali na kuongeza mapato lakini msingi wa utozaji mirabaha unapaswa pia uwe ulio rahisi kwa mamlaka zinazoratibu sekta hii kupanga viwango halisi vinyavyopaswa kulipwa na pia usiota mwanya kwa wahusika kudanganya au kupotosha juu ya thamani halisi. Kwa msingi huo, Kambi ya Upinzani inapendekeza “*gross value*” hiyo ifanyiwe marejeo kwa kutumia “*published reference price*” kama zile zinazotangazwa na *London Metal Exchange (LME)* ambazo zitaondoa mzigo kwa Serikali katika kujua thamani halisi inayopaswa kutozwa mrabaha.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 101, kinazungumzia uwezo wa Kamishna na Afisa mwengine aliyeruhusiwa kuingia (*authorized officer*) kwenye migodi na kupata nyaraka zinazohitajika yaani *power of entry*. Ukiangalia kazi zilizoainishwa hapa kufanywa na Kamishna au Afisa mwengine aliyeruhusiwa kuingia, ni zile zinazotakiwa kufanywa na Wakala wa Ukaguzi wa Madini nchini (*TMAA*), lakini wakala hakutajwa katika kifungu hiki. Kambi ya Upinzani, inauliza kweli kulikuwa na haja ya kuunda Wakala huyu kama anashindwa kupewa nguvu hizi kisheria? Tunamtaka Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili kwa makini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapendekezo hayo kuhusu vifungu mahsusini, Kambi ya Upinzani pia inapendekeza mambo mawili ya jumla ambayo inapendekeza yaingizwe katika Sheria Mpya ya Madini. Kwanza ni haja ya kutenga 20% ya mrabaha kwa ajili ya kurudishwa katika Halmashauri za Wilaya ambako madini husika yamechimbwa ili kusaidia maendeleo ya maeneo hayo na hivyo kunyanya hali za maisha ya wananchi wake. Pili ni kuwepo kwa sharti linalomtaka Waziri kwa niaba ya Serikali kutoa na kuchapisha Taarifa ya Hali Halisi ya Madini katika nchi au kwa lugha nyingine *Statement of Mineral Reserves in the Country* kwa kila mwaka kama inavyofanyika India ili kujua hali ilivyo kutokana na madini yaliyokwishachimbwa na mengine yaliyovumbuliwa kadri shughuli hizo zinavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nihitimishe kwa kusema kwamba katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, Taifa letu limekumbana na mijadala mikali na hata mizozano kuhusiana na kutofaidika kwake na rasilimali ya madini. Tunadhani mojawapo ya mafanikio ya Bunge hili yanapaswa kuwa ni kutunga sheria inayowajali Watanzania lakini pia inayotoa motisha za kutosha kwa wawekezaji kuja kuwekeza katika sekta hii na hivyo kutoa ajira kwa watu wetu na kukuza uchumi wa nchi yetu. Tukifanya hivyo, tutaweza kujenga jamii inayozingatia na kujali haki sawa kwa wote na yenyenye uchumi imara unaotoa ajira na tija kwa wote. Kambi ya Upinzani inawaomba Waheshimiwa Wabunge kuzingatia haja ya uwiano huu katika kujadili na hatimaye kupitisha Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, kwa kuwasilisha kwa ufasaha kabisa maoni ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ndio tutaingia katika mjadala. Orodha yangu hadi sasa ina wachangiaji 20 na nitawatamka Wabunge wasiozidi wanne, wa kwanza ambao ndio pengine watapata nafasi ya kuchangia, kama kawaida dakika 15, ni Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Halima Mdee, sasa namwita Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwamba nimepata nafasi hii ya kuichangia Muswada huu wakati ambapo moyo wangu una furaha kubwa sana kutokana na usikivu wa Serikali ya Chama chetu ya kutekeleza ahadi ya Rais ya nchi yetu na kusikiliza kilio cha Watanzania cha muda mrefu. Siwezi kueleza sana furaha yangu niliyonayo kutokana na Muswada huu ambao unajibu kiu ya wananchi wa Jimbo langu la Simanjiro na kiu ya Watanzania hasa wale waliopata fursa ya kutoa maoni yao kwa muda tofauti kwa Kamati mbalimbali zilizokuwa zimeundwa kwa nia ya kuboresha sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Serikali ilikwishaunda Tume nyingi za kupitia masuala haya ya madini. Naikumbuka sana taarifa ya Jaji Mark Bomani ambayo ilifanya kazi nzuri, kazi ya kihistoria, imechambua mambo ya msingi yanayostahili kupewa kipaumbele katika Muswada huu na nawahakikishieni kwamba taarifa ya Jaji Bomani itakuwa ni dira kubwa sana kwangu na kwa Wabunge wengi watakaochangia Muswada huu wa Madini. Wananchi wa Jimbo langu hususan wananchi wachimbaji wa *Tanzanite* pale Mererani, watakumbuka taarifa ya Kamati ya Jenerali Mboma ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa inashughulikia mgogoro kati ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo wa madini ya vito vya *Tanzanite* pale Mererani. Mapendekezo ya Tume ya Jenerali Mboma, ni matarajio yangu kwamba tutakapomaliza kupitisha Muswada huu yatakuwa yamepata majibu.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanasubiri kuona Muswada tunaopitisha hapa kama utaonyesha sura halisi ya kwamba Bunge hili ni Bunge la watoto wa wakulima na wafanyakazi maskini ambao watahakikisha kwamba Muswada huu unaweka mazingira mazuri sana kwa Watanzania kufaidi rasilimali za nchi yao. Leo baada ya marekebisho ambayo natarajia Waziri atayaleta na kukamilisha Muswada au vifungu fulani vya Muswada kuhusu uchimbaji wa madini ya vito, kwa mara ya kwanza madini ya vito yatakuwa yamekabitihwa yachimbwe na Watanzania kwa asilimia mia moja. Napenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Ngeleja, Naibu wake, Mheshimiwa Malima na wataalamu wake, kwa uamuzi huu wa busara ambao leo Serikali yetu imeufanya katika Muswada huu. Imani yangu ni kwamba, Bunge hili litaridhia marekebisho tutakayoyaleta sisi na yale ambayo Waziri atayawasilisha ili vito vibaki kwa ajili ya Watanzania na hivi ni vito kwa ujumla wake kwa migodi midogo na mikubwa.

Mheshimwa Spika, kwa muda mrefu nilipokuwa nimeingia kwenye Bunge hili, sasa ni miaka minne na zaidi, nimejaribu sana kulishawishi Bunge hili na kuishawishi Serikali ikubaliane na kilio cha Watanzania kuhakikisha kwamba madini ya vito yanabaki kwa ajili yetu. Ni imani yangu, leo hili litatimia na wananchi wa Mererani na Tanzania nzima, watafurahi kwa uamuzi huo wa busara. Ninachotaka kutahadharisha tu ni kwamba pasiletwe *miscellaneous amendments* zingine za mlango wa nyuma zitakazobadilisha sheria ili kuweka uwezekano wa kuruhusu uchimbaji wa madini ya vito kwa wageni. Muswada huu uhakikishe madini ya vito yanachimbwa na Watanzania, leseni zitolewe kwa Watanzania na pale ambapo teknolojia na mitaji zaidi inahitajika leseni hiyo apewe Mtanzania, Mtanzania amkaribishe mgeni, aseme huyu awekeze kwa kiwango ambacho hakitamnyima Mtanzania huyu uhuru wa kuhakikisha kwamba yeye ndiyo anamiliki zaidi ya asilimia 50 katika mgodi huo hata uwekezaji ungekuwa umefanywa wa kiasi gani.

Mheshimwa Spika, ninapenda pia kuchukua nafasi hii, kuikumbusha Serikali au kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha kwamba Leseni ya Wachimbaji Wadogo Wadogo (*The Primary Mining Licence*) iongezewe muda kutoka muda wa miaka mitano na kuwa miaka saba ili kuhakikisha kwamba mchimbaji huyo anayepewa leseni anapata muda mwingine tena wa kufanya utafiti wa madini haya katika leseni hiyo hiyo ya uchimbaji madini ya *Primary Mining Licence*. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewajengea wachimbaji wetu wadogo wadogo mazingira ya kuhakikisha kwamba wanapata muda wa kutosha wa kuchimba madini yale na kuweza kuyauza. Ni kwa minajili hiyo hiyo, ninapenda kuishauri Serikali ihakikishe kwamba mara tu baada ya Muswada huu, wanatangaza tangazo la Serikali la kuzuia usafirishaji wa madini ghafi ya vito ili kuhakikisha kwamba usanifu na uongezaji thamani wa madini haya unafanyika hapa hapa nchini. Faida ya kukata au kusanifu madini ya vito hapa nchini ni nyingi sana, lakini nitataja faida mbili kubwa. Moja, itakuwa ni fursa ya kutoa ajira kwa Watanzania lakini fursa nyingine ni kukaribisha teknolojia kutoka nje iweze kupata nafasi hapa nchini kwa watu wetu na kwa maana hiyo thamani ya madini itakuwa imeongezeka na mapato ya Serikali ya Watanzania yatakuwa yameongezeka kwa kiasi kikubwa.

Mheshimwa Spika, Muswada wa leo pia utazungumzia uchimbaji wa madini yenye thamani kubwa sana na madini yale ambayo ni *strategic minerals* ambayo yanachimbwa kwa uwekezaji mkubwa. Bado ningendelea kuishauri Serikali, kama alivyosema Waziri, tuhakikishe kwamba Serikali inapata hisa katika migodi hiyo mikubwa ili tuwe na jicho katika uwekezaji huu na tuweze kujua nini kinazalishwa, kinauzwa wapi, kwa thamani gani na kwa maana hiyo, tutajua kwamba mapato ya Serikali yatakuwa kiasi gani. Kwa maana hiyo, pia ninapenda kuikumbusha Serikali hasa Waziri atakayetunga Kanuni baada ya Muswada huu kupita na nina hakika Muswada huu utapita vizuri sana kwa sababu ni Muswada wenye tija kwa nchi nzima, kwa Watanzania na nitauunga mkono kwa nguvu zote lakini ahakikishe kwamba katika Kanuni atakazoziaandaa, anaweka *component* ya *cooperative social responsibility* kwa upande wa wawekezaji wale ili wahakikishe kwamba sio tu wanavuna rasilimali hizi na kutuachia mashimo tunataka wananchi wanaozunguka katika maeneo yale ya uwekezaji, waweze kunufaika na uwekezaji uliko katika maeneo yao kutokana na wao kupewa wajibu wa kuchangia miradi ya maendeleo na isiwe ni hisani. Iwe ni wajibu kwa wawekezaji

kuchangia miradi ya maendeleo. Lakini pia katika kodi itakayokusanya, ni vizuri ukawekwa utaratibu wa kuhakikisha kwamba sehemu fulani ya mapato hayo yanarudi katika maeneo yale ili wananchi waone faida ya kutoa ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kugusia suala zima la wawekezaji hawa kurejesha ardhi au mazingira mara tu baada ya uchimbaji katika hali waliyoikuta. Imekuwa ni utamaduni sasa katika uchimbaji wa dhahabu yanaacha mahandaki makubwa, wawekeze na werejeshe mazingira kama walivyoyakuta, tutaachiwa mashimo makubwa, tutaachiwa sumu katika mashimo hayo, Watanzania watakuja kupata hasara tu na wakubwa watakuwa wameondoka kuyapeleka nje. Ndiyo maana napendekeza juu ya ubia wa Serikali kwamba Serikali ihakikishe kwa kila mgodi mkubwa, jicho la Serikali linakuwepo kwa kuwa ina hisa za kutosha, Serikali iendelee kununua hisa ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na jicho letu katika mchakato mzima wa uchimbaji madini. Lakini pia Serikali haiwezi ikategemea *loyalty*, mkakaa mnategemea kale kaasilimia tano kanaweza kubadilisha nchi, haiwezekeni! Ni lazima Serikali iwekeze ili iweze kupata kodi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na wenzangu waliokuwa wametangulia, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa kupendekeza juu ya umuhimu wa kuundwa kwa Mamlaka. Ni muhimu tuwe na Mamlaka itakayopunguza madaraka ya Waziri. Kwa mujibu wa Sheria hii, Waziri amepewa madaraka makubwa mno. Amepewa Bodi ya kumshauri na Bodi ambayo ni lazima kwa wakati huu iendelee kuboreshwa kwa kuweka wawakilishi wa *Tanzania Minerals Dealers Association* na hizi *Regional Associations* ambazo zina uwakilishi halali na wadau halisi katika eneo hilo pamoja na Asasi za kiraia. Kwa maana hiyo, nasema ni muhimu sana katika siku za usoni, Serikali iharakishe kuleta mabadiliko ili kuunda Mamlaka ya Madini. Lakini pia kuweka Kifungu cha kuunda *An Independent Mining Tribunal* kutokana na migogoro iliyoko. Kwa sababu kwa mujibu wa Sheria hii, katika *Section 102*, Kamishna atakuwa na jukumu la kusuluhiha migogoro. Migogoro hii mingine Kamishna atakuwa na maslahi nayo ukizingatia na yeye yumo kwenye mchakato wa utoaji leseni. Kwa maana hiyo, tunahitaji kuwa na chombo ambacho kiko huru, kitakachowenza kushughulikia migogoro itakayokuwa imetokea na uamuzi wa Waziri au Kamishna mwenyewe ili pia kuwapunguzia wananchi mzigo wa kukimbia kila wakati kwenda kwenye Mahakama Kuu kwa mujibu wa matakwa ya sehemu ya 104. Ni vizuri Bodi hiyo ishughulikie madini yote ikiwemo na madini vito.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nigosie suala la *cooperate social responsibility*. Ni vizuri migodi yote hii ikatimiza wajibu huo. Leo ukienda kwenye maeneo ya malisho ya kijiji cha Naisinyai, Losoit, Langasiti na kijiji cha Nomiuti, yamechukuliwa na migodi ya Tanzanite na leo wafugaji maeneo yao hayapo yamekuwa ni maeneo ya migodi. Ni vizuri basi hao wanaonufaika na madini hayo, wasiendelee kuyahamisha kuyapeleka huko wanakopeleka halafu wananchi wanaachwa watupu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri baadaye atusaidie, atoe maeleo ni namna gani tumeamua madini ya vito yabaki kwa Watanzania mara baada ya leseni zote za

wageni wanaochimba vito kwisha. Tuhakikishiwe kwamba leseni hizo na maeneo hayo yanabaki kwa ajili ya kukidhi matakwa ya Sheria mpya na pasiwekwe Kanuni nyingine yoyote itakayoruhusu kwa mlango wa nyuma kuwarudisha wawekezaji hawa wa nje katika sekta ya madini ya vito. Vito kwa Watanzania, Sheria hii inatungwa na Bunge la Tanzania na watoto wa wakulima na wafanyakazi maskini, ni lazima ioneshe dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba Watanzania wananaufaika na rasilimali hii. Tutaweka mazingira mazuri kwa uwekezaji mkubwa unaohitaji teknolojia na mitaji mikubwa na tutawatengenezea mazingira makubwa katika madini yale ambayo ni *strategic minerals*, twende kwenye dhahabu, twende kwenye chuma, twende popote tutakapokwenda lakini ni vizuri pia huko tunakokwenda tuhakikishe jicho la Serikali na hisa za Serikali ziko pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kutizama sehemu ya 43, inayotoa muda usio na ukomo kwa *Special Mining Licence*, kwa wawekezaji hawa wakubwa. Wakati uliopita au kwa Sheria iliyopo sasa, *Special Mining Licence*, ina ukomo wa miaka 25, hata leo napendekeza uwekwe ukomo, ukomo wake usiwe ni mpaka mwekezaji amalize rasilimali iliyoko katika eneo hilo. Tukiacha Sheria iruhusu uvunaji mpaka mashapo yaishe au kwa jinsi mwekezaji atakavyoomba, tutakuwa tumeuza nchi kwa watu wachache wenyе mitaji mikubwa na kuzingatia kwamba wakati mwingine mashapo yaliyoko yanaweza kuchukua miaka 50 hadi 100 au hata kama sio hiyo lakini ni vizuri sana Mheshimiwa Waziri akaangalia kifungo hicho.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kwa marekebisho haya na kwa niaba ya wananchi wa Simanjiro, napenda kuishukuru Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuwa *flexible* katika marekebisho haya na mimi niseme nimefurahi vito kwa Watanzania na ninaunga mkono hoja hii na ninaomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba *Special Mining Licence* haichimbi madini ya vito, tuendelee kuchimba madini ya vito kwa kutumia Primary Mining Licence. Sina mashaka na *commitment* ya Mheshimiwa Ngeleja, sina tatizo na Kamishna wako na Naibu wako na Katibu Mkuu kwamba ninyi ni wasikivu na mtazingatia Sheria hii mara tutakapoipitisha. Tunaomba marekebisho machache tutakayoyawasilisha baadaye wote tusaidiane ili tuweze kuhakikisha kwamba Watanzania wananaufaika, leseni hatutoi ya muda mrefu kupita kiasi na baada ya hapo Watanzania watafarijika na Muswada huu. Nawahakikishieni kwamba Muswada huu umejibu kilio cha muda mrefu cha Watanzania. Ninawapongeza na narudia kuwapongeza, Ndugu General Mboma, Tume ya Bomani na Wajumbe wake wote wakiwemo akina Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, akiwemo Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Cheyo na wengine wote walioshiriki, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, ni furaha tu, ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kukushukuru wewe mwenyewe, kwa kunipa nafasi ya pili, ili niweze kutoa mawazo yangu kuhusu Muswada huu wa Sheria Mpya ya Madini wa mwaka 2010. Kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati na mimi napenda kumshukuru Mheshimiwa Shellukindo na Kamati yao, kwanza kwa imani walivoonesha kwetu na namna walivyotushirikisha katika kutoa mawazo katika ile Kamati. Nafurahi na mimi

nimeshuhudia mwenyewe mabadiliko makubwa na mazuri ambayo yametokana na mchango wa Kamati ile na ninahakika mabadiliko yatakayoletwa, hayo machache, kwa kweli yametokana na kazi nzuri ya ile Kamati na usikivu wa Serikali yenyewe, chini ya uongozi wa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba niipongeze Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba kuletwa kwa Sheria hii, kumezingatia maslahi ya nchi. Duniani kote kitu kinaitwa kutunga Sheria, lazima kitokane na utashi wa kisiasa. Utashi wa kisiasa ndiyo kitu kinachoweza kuongoza na kuleta Sheria nzuri kama hii. Kwa hiyo, mimi naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, ninataka kutoa mawazo yangu katika mambo ambayo ni ya msingi. La kwanza, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia kuhusu mambo ya vito na madini, kwa kweli katika historia Muswada huu umezingatia sana maslahi ya wachimbaji wadogo kwa aina zote ya madini, kwa kuwa tangu mwanzo tulikuwa tunapiga kelele kuhusu vito, imezingatiwa pia. Uzuri ni kwamba katika Sheria hii, Waziri anapewa madaraka ya kuweza kuelekeza mwenye kiwanda au mwenye mgodi kwa kumwambia kwamba asilimia fulani ya madini lazima yasafishwe hapa hapa nchini na huu ndiyo uhai na maendeleo yetu kwa sababu sisi tumekuwa watumwa, pamba tunauza ghafi, madini tunauza ghafi kila kitu kinakwenda hivyo hivyo. Sasa mimi na wezangu tumefurahia sana Muswada huu kwamba sasa itakuwa ni hatua ya kwanza kuweza kusindika mazao yetu hapa hapa.

Mheshimiwa Spika, ila jambo ambalo napenda tulifanye kama tunavyofanya kwa wakulima wadogo, naomba Serikali iangalie utaratibu wa kuanzisha mikopo kwa wachimbaji wadogo na namna ya kununua madini ya wachimbaji wadogo. Kwa mfano, kuna wakati ambapo Serikali iliwhahi kuanzisha utaratibu kupitia Benki, kwa wakati ule ni Benki Kuu, walianzisha utaratibu wa kununua dhahabu kwa wachimbaji wadogo. Uzuri wa utaratibu wa sasa, ni kwamba ukiamka asubuhi kwenye *internet* unaweza ukajua bei ya dhahabu. Kwa hiyo, kuandaa wachimbaji wadogo hawa wakapata namna ya kuweza kuuza hata kama ni kwenye migodi. Kwa mfano, kama Mgodi wa Bulyankhulu unawachimbaji wadogo, Serikali inaweza ikazungumza na hawa wenyе migodi, tukakubaliana watawalipa kiasi gani hawa wachimbaji wadogo, ijulikane maana hawa wanachimba, wanakwenda kuuza usiku kwa magendo wala hatujui wanamuuzia nani na nina hakika wanaibiwa, natoa tu ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tulizungumza jana na ninapenda kulirudia na ninahakika Serikali wamelizingatia na nadhani wanaandaa *amendments*, nilielezee kidogo kwa sababu ninau zoefu nalo. Duniani kote, madini ya msingi yanayoweza kuwa ndiyo chanzo ya kuleta mapinduzi ya viwanda na viwanda mama, kwa Kingereza yanaitwa *industrial base minerals*, ndiyo madini ya msingi ya kuleta mapinduzi ya viwanda. Sasa kwa nchi kama yetu, nashauri Serikali isikubali kutoa *PL* na *Mining Licence* kwa watu ambao watafanya *speculation*, kwa sababu madini haya ni ya msingi. Kwa mfano, mnaweza kuwa mnampa mtu kwa mfano *PL* ya kumiliki chuma, sasa asipoiendeleza mnafanyaje? Maana atakayetafuta *investor*, ni ye ye hata kama Sheria

inataka Waziri kusema, kwenye kile Kifungu cha 10, ambacho kinampa Waziri madaraka ya kuweza kuingilia madaraka ya *development* lakini mwenye mali au mmiliki ndio atakuwa anaisimamia hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tukubaliane kwamba katika Muswada huu, tuweke eneo ambalo litalinda maslahi ya nchi. Chuma, Mkaa wa Makaa ya Mawe, Soda-Ash, vitu kama hivi vikubwa, mmiliki wa maeneo hayo iwe ni Serikali. Serikali ndiyo ina nafasi ya kuagiza vyombo vyake kuingia *joint venture* na wale wawekezaji. Hiyo itaondoa watu kumiliki na kuhodhi maeneo na vilevile itatupa nafasi sisi ya kusimamia uchumi. Chuma ndiyo maendeleo ya dunia na inavyoonekana ingawa utafiti haujakamilika lakini upo uwezekano wa Tanzania kuwa ya tatu au ya nne kwa kuwa na *deposit* nyingi ya chuma. Kwa makaa ya mawe, ukichukua kwa mfano Liganga, ukienda Rukwa, ukienda Mbeya, sisi ni matajiri wakubwa sana wa makaa ya mawe. Sasa mkaa huu hatuwezi kuwapa *PL* watu binafsi, *PL* hizo ziwe mali ya nchi na nchi itaagiza vyombo vyake kutafuta wawekezaji. Hii ndiyo itaweza ikatusaidia namna ya kusimamia uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, labda niseme pia kidogo, Wachina ni *Ma-socialist* Mabepari. Wachina wamefungua mlango kwa akili kweli, sisi tulifungua mlango na panya wakaingia, ndiyo, mimi nataka niseme jambo moja ambalo si zuri. Wawekezaji wote kuna *guidelines* za dunia lakini *investors* wanatujua, wanasema ukienda Tanzania, utakwenda kuwalalia kwenye mikataba, wanatujua, wakienda nchi nyingine, wanafuata kama vile nchi inavyotaka. Hivi tunavyozungumza kuna mtu anasema wawekezaji hawatakuja, watakuja kwa sababu wewe una rasilimali na hata ile *viability* wanaposema machimbo yanatosha kiuchumi, ni rasilimali yetu, unaweza kwenda duniani kote ukununua teknolojia na ukakopa fedha, msingi ni rasilimali na mimi nashauri katika Ilani ya CCM, kwa kuwa najua CCM itarudi madarakani, katika Ilani naomba tuweke mkakati wa suala la kuendeleza madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iimarishe vyombo vyake vitakavyofanya kazi za upembuzi ili sisi wenyewe ndiyo tujue Liganga tuna chuma kiasi gani na aina yote ya madini, ndiyo tunawaalika wawekezaji, tunawaambia hii ndio rasilimali iliyopo. Kwa hiyo, kinachotuumiza ni kusema sisi wanyonge acha waje, wakija ndiyo wenyе kauli, sisi hatuna kauli katika mali yetu, haiwezekani kuwa hamna kauli kwenye mali yenu. Makampuni yote ya Kichina mnayoona yanakuja kujenga barabara hapa, ni Makampuni ya Serikali ya China, ya Mikoa ama ya Serikali Kuu, sisi tumekubali kuachia kila kitu. Tunasema unajua bwana tukigusa huko, watatunyima misaada, Tanzania si nchi ya kuomba misaada na naomba pia sisi Bunge la CCM, tuombe Chama chetu kwenye Ilani, safari hii tuweke kifungu kinachosema mwisho wa kuwa ombaomba ni huu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tuweke mwisho wa kuwa ombaomba kwa sababu ndicho kinachotufanya tunyanyasike katika nchi hii. Sisi ni matajiri hapa Afrika Mashariki na Kanda hii matajiri tuko wawili, Congo DRC na Tanzania, ndiyo matajiri wa rasilimali nyingi. Sasa Mungu akupe nini. Hatuna sababu ya kuwa wanyonge, Chama chetu ni imara, Rais wetu ni imara, tukatae mambo ambayo hayafai. Mimi napendekeza mali ibaki

kuwa ya Serikali sio kwa wawekezaji. Mimi najua kuna watu wanauzwa viwanja, sasa kama Serikali haiwezi kufanya *exploration*, huyu mtu binafsi mnampa, yeze ana hela gani ya kufanya *exploration*? Ana nguvu kuliko Serikali? Haiwezekani na ni mapema mno kusema lakini tutakuja kueleza uzoefu wetu unatupeleka wapi. Tunafanya majaribio mahali, sitaki kutoa siri na ikifanikiwa mimi nitakuja kuwaambia Waheshimiwa Wabunge inawezekana kufanya hivyo. Tunaogopa bure tu, akili nyingi tunazo, tungekuwa maskini wa akili, mimi ningeogopa na utajiri wa kwanza ni akili na tumepewa, sasa tatizo liko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Wabunge hatuna tabia ya kujibizana yaani huwezi kumjibu Mbunge mwanzako lakini nataka nielezee kile Kifungu cha 43, hakikuweka muda wa mwisho kwa maana ya miaka kwa sababu tunazungumzia madini ya aina nyingi, hatuzungumzii madini ya miaka mitano, kumi au 25, hapa kinachotafutwa ni *feasibility study* inayoonesha *viability* ya huo mgodi unaochimba. Kwa hiyo, huwezi kuunganisha *feasibility study* na miaka maana nyingine itasema miaka kumi na nyingine miaka kumi na tano. Sasa utachanganyaje kuweka *limit* ya miaka wakati mradi ndiyo unajiamulia miaka na mkopo wa *investor*, utategemea miaka ambayo atakuwa amelipa fedha yake. Kwa hiyo, nashauri tukubaliane na Serikali, hakuna haja ya kuweka muda, si sawa, watu watatucheka, utawekaje muda? Tunachoweka muda ni *feasibility study* na uhai wa mali iliyopo pale ambayo unataka kuchimba.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Senetor Mzindakaya, huo ndiyo mchango unaofanana na watu wenye uzoefu. Tunaendelea na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, kwa kuwa Mheshimiwa Halima Mdee hayupo na nimepokea ombi la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa heshima, nadhani nitampa yeze ikiwa kutakuwa na muda na vinginevyo ataanza jioni.

**MHE. LOLESLIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada huu amba o uko mbele yetu, Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka kabisa ambapo wananchi hasa hasa wachimbaji wadogo walikuwa katika hali ngumu. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu wakati huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi ninatoka katika sehemu ambayo ni ya uchimbaji. Nimekua na nimesoma kutokana na fedha zinazotokana na uchimbaji. Kwa hiyo, ndiyo maana nimefarijika sana na Muswada huu kwa sababu umegusa hasa wachimbaji wadogo wadogo. Muswada huu umeweza kuwataja wachimbaji wadogo wadogo katika Sheria hii na umezungumzia jinsi ambavyo wachimbaji wadogo wadogo wamepewa haki ndani ya nchi yao. Kwa hiyo, niseme kwamba Muswada huu umewatambua wachimbaji hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuwatambua wachimbaji wadogo, mimi mawazo yangu, ninaiomba Serikali iweke mfumo mzuri wa kuwawezesha wachimbaji hawa kwa sababu wachimbaji wadogo wanachimba katika mazingira magumu sana. Hawana zana za kuchimbia, hawana mitaji na matokeo yake wanajikuta kwamba kwa kutumia zana duni walizonazo wanachimba kwa kuteseka sana na matokeo yake wengine wanaangukiwa na migodi kama jinsi ilivyotokea katika kijiji cha Sabora kule Kasemi. Kwa hiyo basi, ninaiomba Serikali kwa vile imeamua kuwajali kabisa wachimbaji wadogo, basi iendelee kuwapa kipaumbele hasa hasa kwa kuwapa mitaji ili waweze kunufaika na kuweza kuimarisha uchumi wao kwa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, naiomba Serikali iendelee kuwaelimisha wachimbaji hawa. Kutokuwa na elimu ya uchimbaji wa madini kunasababisha athari kubwa sana kwa wachimbaji hawa. Unakuta watu wengi wanaposikia mahali fulani kuna madini, watu wanaingia kuchimba kule kwa wingi, kwa sababu ya kukosa elimu ndiyo maana kunasababisha wachimbaji hawa kuathirika hasa kwa kuangukiwa na migodi hii na inaleta shida sana na kuweza kupoteza maisha ya wananchi. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwa kweli pamoja na Muswada huu, lakini pia tutoe elimu kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili waweze kunufaika zaidi, waweze kuchimba kwa teknolojia nzuri kabisa ili waweze kupata matunda ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuzungumzia habari ya hii migodi mikubwa ambapo kuna vijiji ambavyo vimezunguka migodi hii, naishukuru sana Serikali kwa kuongeza asilimia ya mrahaba lakini niseme tu kwamba mrahaba huu hautoshi kwa ajili ya maendeleo au huduma za jamii katika maeneo husika. Nikitolea mfano tu kwa ule mgodi wa *GGM* ambapo kwa kila mwaka Halmashauri ya Wilaya inapokea kama kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya huduma za jamii mahali pale. Kiwango hiki ni kidogo sana, hakitoshelezi kiasi kwamba hata unapofika katika maeneo husika ya vijiji vilivyo jirani na migodi, kwa kweli wananchi wanaishi katika maisha duni sana. Kwa hiyo, kwa ushauri wangu, pamoja na ongezeko la mrahaba, ninaomba sana Serikali ijaribu kuangalia pia utaratibu mpya wa kuweza kutenga *percent* fulani ya mapato yatokanayo na migodi hii ili yaweze kunufaisha vile vijiji vilivyo kandokando ya migodi hii. Hii itawezesha vijiji hivi kuweza kunufaika zaidi na kuweza kupata huduma bora hasa hasa tukizingatia kwamba ni muhimu kwa kweli vijiji hivi au wananchi hawa waweze kuishi maisha bora kwa sababu Mwenyezi Mungu ameweza kutoa rasilimali hii kwa ajili yao.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali ni hilo hasa ukizingatia nilivyotangulia kusema, natokea katika Jimbo la Busanda, kuna vijiji ambavyo viko jirani kabisa na migodi. Kuna vijiji kama cha Nyakagwe, ambacho kiko jirani, kilomita mbili tu kutoka katika mgodi wa *Barrick* wa *Kahama Gold Mine* lakini eneo hili kwa kweli huduma za jamii, inasikitisha. Ukifika katika eneo hilo, hakuna maji, huduma za afya, zipo kwa kiasi ambacho kwa kweli hakiridhishi. Kwa hiyo, Serikali itakapoona kwamba kuna umuhimu huu wa kuweza kuangalia kwa upya kwamba kiasi fulani au *percent* ya mapato irudi katika vile vijiji ambavyo viko karibu na migodi hii. Nitoe tu mfano, tunashukuru kwamba mwaka jana ilipitishwa sheria kwa sekta ya maliasili ambapo vijiji vilivyo kandokando ya migodi hii ili yoweze kunufaika zaidi na kuweza kupata huduma bora hasa hasa tukizingatia kwamba ni muhimu kwa kweli vijiji hivi au wananchi hawa waweze kuishi maisha bora kwa sababu Mwenyezi Mungu ameweza kutoa rasilimali hii kwa ajili yao.

kwa ajili ya huduma za jamii. Kwa hiyo, niombe basi hata katika sekta ya madini tujaribu kufanya hivyo ili kuweza kuimarisha na kuwezesha vijihi hivi vilivyoko karibu na machimbo vione kwamba Mungu amewajalia na amewawezesha kuwepo katika maeneo yale. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kuongezea ni kwamba; naishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeamua kushiriki kikamilifu katika uchimbaji wa madini au katika kuendeleza sekta ya madini. Naomba basi Serikali hii iongeze zaidi usimamizi wa rasilimali katika maeneo husika ya uchimbaji ili kuweza kuona kwamba kile kiwango kinachotakiwa au kinachozalishwa pia hata sisi wenyewe au Taifa zima tuweze kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kuishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeleta Muswada huu, kwa kweli ni Muswada mzuri ambao una manufaa kwa wananchi wetu hasa hasa wale wachimbaji wadogo ambao ni kipaumbele kwa sababu tukiwajali hawa wachimbaji wadogo, maana yake tumejali jamii nzima. Kwa hiyo, niendelee tu kuomba Serikali pia ijaribu kutoa elimu basi kwa hawa wachimbaji wadogo ili waweze kujua sheria hii mpya. Kwa sababu ni sheria mpya, unakuta watu wengi wanakuwa hawana elimu hii. Kwa hiyo, niiombe Serikali, kupitia Muswada huu, iweze kutoa elimu kwa hawa wachimbaji wadogo ili waweze kufahamu zaidi kwamba ni haki zipi za msingi ambazo wanatakiwa kufanyiwa na Serikali yao lakini pia, waweze kunufaika zaidi na Muswada huu au Sheria hii Mpya ili waweze kunufaisha pia familia na maisha kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, niwaombe pia wananchi kwa ujumla wanaotoka katika maeneo ya uchimbaji, wawe tayari kusikia na kuelimika kupitia Sheria Mpya hii ya Madini na kuweza kuitumia kwa ufasaha zaidi ili waweze kunufaika zaidi na kuweza kuimarisha maisha yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nichukue nafasi hii kusema kwamba nashukuru sana kwa Muswada huu na nashukuru sana Serikali jinsi ambavyo imeweza kuuleta kwa wakati mzuri na muafaka na kwa sababu imekubali kabisa kubadilisha sheria. Nina imani kubwa kwamba itaweza pia kuzingatia yale yote ambayo tumeiomba katika kuwawezesha wachimbaji wadogo ili iweze kuimarisha maisha yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kuunga mkono hoja hii, nashukuru sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda huu uliosalia wa dakika 10, hauwezeshi uchangiaji wa haki kama inavyotakiwa wa dakika 15. Lakini la pili, pia nisingependa saa 11.00 kuanza na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa sababu wote tunaelewa saa 11.00 huwa tuko wachache mno na huyu ni mtu mzito anatakiwa azungumze watu wametulia. Kwa hiyo, nitaanza na Mheshimiwa Kabwe Zitto saa 11.00, ingawa anaitwa Zitto, lakini mwepesi tu! Baada yake yeye, atafuata Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, halafu Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Dora Mushi, wameongezeka wengine wawili, Mheshimiwa Shibuda na Mheshimiwa Janet Mbene, lakini kwa kuwa

tunatarajia kumaliza shughuli za Muswada huu asubuhi, basi nitatoa nafasi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa yale yote atakayoyasikia leo kwa Wabunge, kwa kawaida, kwa muda kama huu, atapata kusikia Wabunge 14, ili Wizara ijiandae vizuri, basi tutamalizia wale wanne kesho asubuhi, ndiyo tuhitimishe hoja hii.

Kwa hiyo, kwa sababu muda hauruhusu kuendelea na shughuli nyingine, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.52 mchana Bunge lilahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyotangaziwa saa 7.00, orodha bado ni ndefu na sasa siwezi kupokea majina tena zaidi kwa sababu nitaharibu ratiba. Lakini nadhani ningewataja wale wanne wa kwanza ambao watachangia kama ifuatavyo:- Tutaanza na Mheshimiwa Kabwe Zitto, atafuatiwa na Proffesor Raphael Mwalyosi ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya na baada ya hapo nitamwita Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kushiriki katika kuchangia Muswada huu kama jinsi mwenyewe ulivyoita kwamba ni Muswada wa kihistoria kwa sababu inachukua muda kwa nchi kukaa na kutunga Sheria ya Madini. Tutakumbuka kwamba tulikuwa na Sheria ya mwaka 1979 tukatunga nyingine mwaka 1998 na sasa hivi mwaka 2010 ndiyo tunatunga Sheria nyingine, kwa hiyo, inaweza ikachukua miaka na inategemea na jinsi Sheria hii itakavyokuwa inaweza ikachukua muda mrefu zaidi hata kwa kipindi cha kati ya sasa na Sheria ambayo inatumika sasa kuweza kuwa na Sheria nyingine ya Madini.

Mheshimiwa Spika, mimi nitapita pale ambapo Kambi ya Upinzani Bungeni imepita asubuhi wakati tunatoa maoni yetu kama jinsi ambavyo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Jussa kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Mnyaa, kwamba Sheria hii mpya tunaitarjia iweze kujibu zile changamoto tatu ambazo tumeziainisha na tumeweza kuonyesha ni maeneo gani ambayo tunadhani bado Sheria hii haijaweza kuyaelezea kama jinsi ambavyo inavyotakiwa. Lakini napenda nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na Wabunge wote ambao walishiriki katika kuipitia Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, tunavyopitisha Sheria hii leo ni tofauti kabisa na ilivyokuja mwanzo. Kuna mambo mengi sana ambayo tumefanikiwa kuyaongeza katika ngazi ya Kamati na katika hili pia napenda kuwapongeza kabisa Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Ngeleja na Naibu wake Mheshimiwa Malima kwa kuwa wasikivu na kupokea maoni mbalimbali ya Kamati na kuweza kuyafanyia marekebisho. Hawakuwa wabishi na hii inaonyesha ni jinsi ambavyo Wizara ambazo tunawakabidhi vijana zinavyokuwa na utendaji ulio imara, imara zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze kwa dhati kabisa vijana wenzangu kwa jinsi ambavyo waliweza kupokea na tulikaa sana toka siku ya Ijumaa, Kamati ya Nishati na Madini inashughulikia Muswada huu na tulikuwa tunakaa mpaka usiku! Tulikuwa hatukai Bungeni kabisa! Kwa kweli Wajumbe wote walioshiriki walifanya kazi nzuri sana. Ni masikitiko yangu tu kuwa baadhi ya Wabunge amba wanatoka maeneo ambayo yana migodi na wamekuwa wakilalamika sana kuhusiana na masuala ya rasilimali hii ya madini hatukuwaona kabisa kwenye Kamati na hatujawaona kabisa hata hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, inaweza ikaja baadaye watu hao hao ndiyo wakaanza kulalamika kwamba Sheria ni mbaya ama ni nini wakati fursa ya kushiriki katika utungaji wa Sheria walikuwa nayo. Katika hili napenda kwa dhati kabisa nimpongeze sana Mbunge wa Simanjiro - Mheshimiwa Ole-Sendeka pamoja na kwamba alikuwa ana Miswada miwili, ule wa Mifugo na Madini, lakini bado alihakikisha anakuwepo mara zote kuhakikisha kwamba analinda maslahi ya wapigakura wake. Vilevile nampongeza Mbunge wa Busanda - Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, naye pia alishiriki muda wote. Sasa natarajia kabisa kuwa wale amba hawakushiriki wasije kurutudisha nyuma, wakubaliane na yale ambayo wenzao wameweza kushiriki na kuweza kuyapitisha.

Mheshimiwa Spika, licha ya yale ambayo tumekubaliana, kuna mambo ambayo hatukukubaliana ambayo tukasema kuwa tutakuja kuyazungumza ndani ya Bunge. Yale ambayo tunadhani kuwa hii ndiyo fursa ya kuweza kuyazungumza, mengine yameshazungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, la Kwanza alizungumza Mheshimiwa Ole-Sendeka kuhusiana na kutoa leseni kutokana na Mashapo, leseni za uchimbaji mkubwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka amezungumza hapa kwamba ye ye *report* ya Bomani ndiyo Msahafu. Lakini nilikuwa naomba nirejee *report* ya Bomani ilisema nini kuhusiana na utoaji wa leseni za uchimbaji mkubwa *SML*, maana yake kulikuwa kuna malalamiko makubwa sana kama mnakumbuka.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba *MDA* tulizokuwa tunazitoa kwa muda wa miaka 25 ni nyingi sana na bahati nzuri mimi nilishiriki kwenye Kamati ya Bomani. Tukapata maoni mengi sana ya wadau wanaosema kwamba miaka 25 ni mingi sana, haiwezekani kutoa leseni au kuwa na *MDA* kwa miaka 25 ni mingi mno irekebishwe na mapendekezo mengi yaliyokuja ni kwamba leseni zitolewe kutokana na Mashapo ambayo yanapatikana katika lile eneo. Sasa pendekezo letu la 4.1.3 ninasema kuhusu mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Madini ya Kamati ya Bomani inasema: “Leseni za Uchimbaji mkubwa *SML* zitolewe kulingana na Mashapo.”

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali yenye imetekeleza hilo, imetekeleza uamuza wa Bomani. Kwa hiyo, wale waumini wa *Report* ya Bomani labda inabidi turudi tena kwa Bomani tumwambie Rais atuunde kwa siku chache, tunaweza kulirekebisha hili, lakini kwa kweli kwa hili Serikali imehamisha kama jinsi ilivyopendekezwa kwenye *report* ya Bomani. Kwa hiyo, nilikuwa ninapenda niwaelimishe wenzangu hivyo na kwamba kwa vyovypote vile katika utungaji wa Sheria kuna *compromise* kama nilivyosema kuna mambo ambayo Serikali ilikuja nayo, tukawakatalia tukayarekebisha. Kuna mambo ambayo sisi tumekuja nayo wakayakubali, kuna mambo ambayo

hatujakubaliana lakini kwa hili tukiwanig’niza tunakuwa tunawaonea kwa sababu wamelitoa katika taarifa ya Bomani kama jinsi ambavyo tuliwaomba na tulivyowataka watekeleze taarifa ya Bomani.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo hatujakubaliana ni suala zima la jinsi gani ambavyo tunahakikisha kwamba rasilimali za madini zinafaidisha wale watu ambao rasilimali ile imepatikana kwao. Msemaji wa Kambi ya Upinzani amezungumza na nilikuwa naomba nichangie hili pia kwamba Kamati ya Bomani ilipendekeza kwamba sehemu fulani ya mrahaba irudi katika maeneo ambayo yana migodi na tulipendekeza asilimia 20 ya mirahaba hii. Serikali imelikataa, lakini haina maelezo ya kina ya kwa nini imelikataa. Sisi tunadhani hili ni jambo jema na jambo hili litapunguza sana kelele za wananchi kwa sababu wataweza kuona kwamba sehemu ya rasilimali inachimbwa katika maeneo yao, inarudi. Tulikuwa tumependekeza kwamba asilimia 20 ya mapato yanayotokana na madini yarudi kwenye Halmashauri za Wilaya kule madini yanapopatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba hili Serikali iendelee kulifirkiria na ililetie katika Muswada huu. Jambo la msingi hapa ambalo ni *conception* ni kwamba hatutaki asilimia 20 ya mapato yanayokusanywa kama kodi. Kama kodi ya mapato, *revenues* na *charges* nyingine, tunachokitaka ni asilimia 20 ya mrahaba kwa sababu mrahaba siyo kodi, kimsingi mrahaba ni *compansation* ya unyonyaji wa yale madini kule chini siyo kodi. Kwa hiyo, hii inaweza ikarudi kule, na hairudi kwenda kuagawia watu waende wakazitumie, inarudi kwa ajili ya kwenda kwenye Halmashauri, kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano mzuri sana. Ni kwamba eneo lolote ambalo madini yanapatikana, Halmashauri za Wilaya zinapata taabu sana kwa sababu idadi ya watu katika yale maeneo inaongezeka. Maana yake ni kwamba idadi za hospitali zitaongezeka, idadi ya mashule itaongezeka na idadi ya huduma za maji itaongezeka. Kwa hiyo, leo huwezi kupanga bajeti ya Wilaya ya Kahama sawa sawa na Wilaya ya Kigoma. Haiwezekani kwa sababu Wilaya ya Kahama mahitaji ya watu wa Kahama ni kubwa zaidi kuliko ya watu wa Kigoma kutokana na upatikaji wa ile rasilimali pale na watu kuongezeka zaidi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema kwamba sehemu hii iweze kwenda, na wala hii haitakuwa mara ya kwanza. Watu wote ambao wana vitalu vya uwindaji asilimia 25 ya mapato yanayotokana na vitalu yanarudi kule ambako rasilimali ile inapatikana. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba hili liweze kuangaliwa ili kuhakikisha kwamba watu wetu wanafaidika. Hili hatukukubaliana katika Kamati, ndiyo maana tumelileta hapa ili Bunge zima liweze kutafakari na kuona ni jinsi gani tunaweza kulifanya.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo hatukuweza kukubaliana ni suala la uanzishwaji wa *Mineral Development Fund*. Waziri amelieleza pamoja na lile la Mamlaka, lakini alivyolieze ni tofauti na jinsi ambavyo Serikali iliji-*commit* kwenye Kamati kwa sababu ninayo nakala hapa ya Serikali inasema kwamba “*on establishment of Mineral Development Fund the Government will make a commitment to establish the*

*Fund in the future.*" Katika maelezo ya Waziri wa Nishati na Madini alipokuwa anazungumza hapa, leo amegusiagusia *Mineral Development Fund* hakutoa *commitment* ambayo aliiyahidi kwenye Kamati, kwa hiyo, tunachokitaka tunajua kwamba uanzishwaji wa *sovereign Wealthy Fund* siyo kitu kidogo. Kama Serikali ingekuwa imejiandaa toka mapema miaka miwili iliyopita toka *report* ya Bomani imewasilishwa, leo tungeweza kuwa na Muswada ambao umehusisha uanzishwaji *Sovereign Wealth Fund*, lakini angalau Serikali ingeweka *commitment* ndani ya Bunge hapa kusema kwamba *Sovereign Wealth Fund* ni jambo ambalo linakubalika.

Serikali italifanya kwa hatua hizi na hizi na faida ya *Sovereign Wealth Fund* ni kuweza kusaidia kuwekeza katika maeneo ambayo labda ni magumu kuweza kuwekeza, inaweza ikajenga ma- *university* ambayo yanatasaidia kujenga uwezo wa Watanzania. Inaweza ikajenga mabarabara, inaweza ikapeleka huduma za maendeleo katika maeneo ambayo yapo kule, lakini pia fedha ambayo inatokana na hii *Sovereign Wealth Fund* inaweza kutumika kuwekeza kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri tulionao na nilizungumza na *Governor* wa Benki Kuu kwamba wakati Kampuni ya *African Barrick Gold* imetangaza kuuza hisa zake katika soko la hisa la London, kama tungekuwa na *Sovereign Wealth Fund* yetu, tungeweza kushiriki katika ununuzi ule moja kwa moja kutokana na *Sovereign Wealth Fund* yetu. Tungekuja huku zile *free carried interest* zingeongeza katika zile ambazo tayari tunazo na zile za *negotiation* na Serikali na wenyewe leseni zingeongeza zaidi, kwa hiyo, tungeweza kumiliki sehemu kubwa sana ya migodi ambayo inamiliikiwa na hiyo kampuni ya *African Barrick Gold*. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu sana Serikali iangalie uwezekano huu na itoe *commitment* kama ilivyoahidi kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwenye Kamati ilisemwa very *firmly* ilivyofika hapa Bungeni wakaizungumza juu juu, kwa hiyo, tunataraja Waziri atawezza kutoa hiyo *commitment*.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninadhani litakuwa la mwisho, kutokana na muda ni suala la *section 25* inayohusiana na *prohibition*. *To prohibit access to information*, sasa kama Taifa tumeshaji- *commit* kwenye *transparency* kwenye *sector* ya *exertive industry*, tunafahamu kwamba Serikali ipo katika utaratibu au mchakato wa kuleta Sheria kwa ajili ya kuiweka Kisheria ile *exertive Industry transparency initiative* kama jinsi ambavyo Msemaji wa Upinzani alivyozungumza hapa asubuhi. Lakini tayari ile *section 25* itaweza kubana hata hiyo Sheria tutakayoitunga kwa sababu ile inakataza katakata *information* zozote kuweza kutolewa. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kui-*relax* ile *section 25* ili isiweze kutuletea taabu wakati tunafanya utekelezaji wa *exertive Industry to transparency initiative* ambapo tayari Kamati imeshaundwa na Mheshimiwa *Judge* Bomani ameshateuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Kwa hiyo, kwa heshima ya *Judge* Bomani Serikali ingeweza ku-*relax* kile kipengele kuhakikisha kwamba hatutapata matatizo katika uanzishwaji wa hii *IT*.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kuna wakala wa Serikali ambao tumeuanzisha baada ya matatizo ya Alex Stuart, gharama ambazo tulikuwa tunalipa kwa Alex Stuart.

Lakini taarifa ambazo Alex Stuart waliweza kuzitoa, tumeanzisha wakala wa Ukaguzi wa Migodi lakini wakala huu katika Sheria nzima hakuna hata sehemu moja ambayo wakala huu unatajwa kama jinsi ambavyo Msemaji wa Upinzani alisema. Kwa hiyo, tulikuwa tunahitaji mabadiliko mahususi ya maeneo mahususi yafanyike na hasa pale kwenye ruhusa ya kuingia kwenye migodi siyo watu wa *TRA* tu, siyo Kamisha wa madini tu na watu wake bali pia na watu wa wakala hii.

Mheshimiwa Spika, kama wakala wa jiolojia ametajwa kwenye Sheria, kipi ambacho kinazuia wakala hii ya kukagua migodi hii kuweza kutajwa kwenye Sheria? Masuala ya Mamlaka yameelezewa vizuri sana na Msemaji wa Upinzani Bungeni. Hili ni suala ambalo halijawa *addressed* kabisa, ndiyo suala ambalo lingeweza kutusaidia kuhakikisha kwamba sekta hii inasimamiwa vizuri. Lakini mabadiliko makubwa ambayo tumeyafanya kwenye Muswada na usikivu wa Wizara ya Nishati na Madini, Waziri pamoja na Watendaji wake wote ambao tulikuwa nao, tulikuwa tunakesha nao kwa kazi hii. Imeonyesha ni jinsi gani ambavyo kwa pamoja Bunge, Kamati ya Nishati na Madini pamoja na Serikali tumeweza kuhakikisha kwamba tumeboresha Muswada huu na iwapo mambo haya ambayo tumeyazungumza na kuona kwamba bado hatujakubaliana nayo, bado yale yanayohitaji *commitment* ikatolewa *commitment*, yale yanayohitaji mabadiliko ya Kisheria yakafanyiwa mabadiliko ya Sheria ya sasa, kwa kweli tutakuwa na Muswada mzuri sana ambao utasababisha tuweze kumiliki vizuri rasilimali zetu za madini na kama mabadiliko haya yakifanyika hatutakuwa na sababu ya kukataa Sheria hii. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kuchangia Katika Muswada huu wa Kihistoria na ninataka niseme ni Muswada ambao umekuja wakati muafaka. Wakati Watanzania tumetoka kwenye lindi la uelewa mdogo wa masuala ya madini na sekta nzima ya uchimbaji madini tumpata wasomi, watu wameelimika, ni tofauti kabisa na mwaka 1979 na 1998 leo kuna uelewa mkubwa. Kwa hiyo, Muswada huu unapoletwa leo, ninaamini kwamba tunazalisha Muswada au Sheria ambayo itakuwa na tija kuliko Miswada iliyopita.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo sababu kubwa ya kuunga mkono, lakini vilevile ninaunga mkono kwa sababu imekuja wakati muafaka ambapo Wilaya zilizokuwa nyuma zikiwa na madini kama Ludewa ni wakati huu ambapo uwekezaji na uchimbaji madini katika Wilaya hizo hususan Ludewa umeanza. Kwa hiyo, tukiamini, tutaweza kushiriki vizuri katika maendeleo ya sekta hii na kwenda sambamba na wananchi wa Tanzania wenzetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri Ngeleja, Naibu wake na Watendaji wote. Ninatoka kwenye madini lakini sikushiriki sana kwa sababu nilikuwa kwenye shughuli nyingine, ila nilikjua kwamba wenzetu walioko watafanya kazi nzuri sana. Niliamini kwamba Mheshimiwa Ngeleja na wenzake ni wasikivu, lazima watasikiliza na tutatoka na Muswada na Sheria nzuri kama inavyoelekea kuwa sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kusema mambo machache kama ifuatavyo:- Kwanza nilitaka nizungumzie kuhusu usimamizi wa madini ya viwanda (*industrial Minerals*) kama vile chuma, *soda ash* na makaa ya mawe kwamba ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Mzindakaya yakiachiwa holela inaleta matatizo sana.

Mheshimiwa Spika, awali mradi wa kuzalisha chuma ghafi, mradi wa kasi mpya ilikuwa tutumie milima inayoitwa midogo midogo ya chuma nje ya maeneo ya *NDC* nje ya Liganga na maeneo hayo yapo karibu manne, lakini tulipokwenda kuangalia, uwezekano wa kutumia maeneo hayo iligundulika kwamba yote yalikuwa na makampuni yanayo-*prospect for minerals other than chuma*. Ni maeneo ya *deposit* za chuma lakini wanatafuta madini mengine kama *platinum* na maeneo mengine *platinum* iko *associated* na chuma, wao wanachotafuta ni *platinum* siyo chuma. Kwa hiyo, hatuwezi kutumia chuma kile kwa sababu kuna watu wamepewa leseni za *ku-prospect* madini mengine. Kwa hiyo, tulishindwa na ikabidi turudi Liganga kumega milima michache au mmoja kwa ajili wa mradi wa *sponge iron*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nami naungana mkono na Mheshimiwa Dr. Mzindakaya kwamba Madini ya thamani kubwa na siyo ya thamani kubwa, *Industrial Minerals* kama haya niliyoyataja ni vyema yote hayo kama ni *major deposit* yawe chini ya usimamizi moja kwa moja wa Serikali kupitia kwa mfano *NDC*.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nilitaka nizungumzie ni suala la ukomo wa leseni za uchimbaji madini haya ya Mashapo, uchimbaji mkubwa, nakubali kwamba hakuna sababu ya kuwa na ukomo miaka 25, kama tuna uwezo wa kushiriki au kufanya tathmini kujua kiasi cha mashapo na thamani yake ni kiasi gani, kuweza kufanya *feasibility study* itakayofanywa na sisi tunalewa na tunajua hapa kuna madini yanayoweza kuchimbwa kwa miaka 10 hadi 20 na kwamba hatuwezi kudanganywa, kama uwezo huo tunao mimi sina matatizo. Hakuna sababu ya kuweka muda wa kuchimba madini haya.

Mheshimiwa Spika, nitakachotaka Waziri anisaidie ufanuzi huo, maana yake Mwalimu Nyerere alisema kwamba tusichimbe madini kama hatuna uwezo na tumejifunza kwamba hapo nyuma miaka karibu kumi iliyopita, tumejiingiza kwenye sekta hii, imetuletea matatizo kwa sababu pengine uzoefu wetu ni mdogo. Je, kwa utaratibu huu, tukipitia *feasibility study* ambayo tutajua madini haya, *deposit* hii inatupeleka kwenye uchimbaji wa miaka kadhaa, ndiyo muda ule utakuwa *minimum* kwa ajili ya kumwezesha Mwekezaji achimbe hapo. Kama hivyo ndivyo utalaamu huu tunao? Kama hatuna tutaupata kwa utaratibu upi?

Mheshimiwa Spika, napenda Waziri atueleze mchakato au utaratibu utakaotumia kuhakikisha kwamba utalaamu huu Watanzania tunakuwa nao ili kuanza kushiriki mara moja katika utaratibu huu unaozungumzwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu nilitaka kuchangia kuhusu haki za wananchi wanaoishi maeneo ya machimbo au migodi. Narudia kusema, natoka kwenye Wilaya

ambayo imebakia nyuma kwa miaka mingi sana licha ya kuwa tajiri, kila tulipoomba jamani mtupe angalau barabara nzuri tunaambiwa mgoje *development fund* za barabara, zina uhusiano na mradi mkubwa wa Mchuchuma au wa Liganga. Matokeo yake tumebakia nyuma mpaka leo. Sasa tunasema wananchi hawa lazima wafaidi tunapoanza kuchimba madini haya.

Mheshimiwa Spika, naona kuna namna nyingi za kuwawezesha wananchi. Moja ni *empowerment*. Wananchi hawa wapewe mafunzo ya kuwawezesha kushiriki katika uchimbaji na uwekezaji, kwa kutumia fursa zinazotokana na uchimbaji madini, kuwa-*empower* wananchi hawa ili waweze kushiriki, lakini pia waweze kupata *revenue* kutokana na *activities* nyingine kama vile viwanda vidogo vidogo, kilimo, uzalishaji wa mifugo kwa ajili ya kulisha watu watakaokuwa kwenye migodi hiyo, watapata fedha na hii inawezekana.

Mheshimiwa Spika, lakini kupata gawio, tumeambiwa hapa habari ya mrahaba na mimi nadhani ni haki. Ni lazima wananchi hao wapate kidogo kutokana na mapato hayo, lakini hata upande wa hisa za Serikali, kwa sababu tumekubaliana kwamba Serikali ni lazima iwe na hisa kwenye miradi hiyo mikubwa, sasa kwenye hisa hizo hasa wakati wa *operation* kwanini Halmashauri zisipate mgawo wa hisa hizo, lakini hata fidia ya haki. Kwa vile mchakato wa kupata fidia unachukua hata zaidi ya mwaka mmoja, ni vema wenzetu hawa wa Wizara wakawa wanatueleza mchakato wa fidia unaonaokwenda sambamba na mchakato wa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunaambiwa fidia itatolewa na Mwekezaji mwenyewe, na mchakato mzima ni juu ya mwekezaji: Je, tuna uhakika gani kwamba fidia itakuwa imekamilika kabla ya uwekezaji? Sheria inasema, kabla ya uwekezaji, fidia iwe imetekelizwa. Je, utaratibu huo ukoje?

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana kama Waziri atatoa ufanuzi huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie masuala mawili ya kimazingira. Pamoja na kwamba sheria hii itazingatia sheria mama, masuala ya mazingira yatasimamiwa na sheria mama ya mazingira, lakini nilipenda katika kifungu cha 41 na 49, kinasema kwamba haitoshi kuzungumzia kwamba sharti moja la kumpa mtu leseni ya uwekezaji, uchimbaji madini iwe ni kuzingatia *Environmental Management Plan*. Uzoefu wetu North Mara umeonesha kwamba hiyo haitoshi, matatizo ya North Mara ilikuwa ni kutokuwepo na *monitoring*, hakuna mtu aliyejewa anafuatilia mambo yaliviyotakiwa kutekelezwa katika mgodi ule, matokeo yake tuliposhtukia kuna matatizo, ndiyo wote tunakurupuka, tunashangaa.

Kwa hiyo, siyo suala la *Environmental Management Plan* kuifuatilia, haitoshi. Lakini *Environmental Monitoring* ni muhimu sana na lenyewe lingezingatiwa na nitapenda kujua kama Waziri analitambua hilo na analainisha katika *Environmental Management Plan*, au hilo limeachwa nje?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni sharti la kuhusu muda wa *abandonment*. Kama tunafikia mwisho au mwekezaji anaamua tu kwamba sasa basi, siwezi kuendelea, wakati mgodini kuna mashimo na kadhalika. Tunazungumza kuwa na *closure bond*. *Closure bond* ni kitu kinachotakiwa kifanyiwe mwisho, lakini tumtake Mwekezaji yeote iwe ni lazima afanye *rehabilitation* ya *area* ile, irudie hali yake ilivyokuwa mwanzo. Suala la *closure bond* iwe ni *option* ya mwisho kwamba tutatumia hela yake yeye iliyowekwa kama *bond* kurekebisha eneo ambalo ameliharibu endapo yeye ataamua kuondoka na kuacha mgodi ule. Lakini isisitizwe kwamba ni lazima afanye *rehabilitation* ya *site* ile kabla hajaondoka.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ulikuwa ni mdogo kwa namna hiyo, nashukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Prof. Mwalyosi. Nimemwona Mheshimiwa Halima Mdee ndiye atakayefuata, na katika orodha hii sasa nitamwita baada yake Mheshimiwa Dora Mushi ambaye atafuatiwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi. Asubuhi uliponitaja sikuwepo kwa sababu nilikwenda hospitali, kichwa changu hakijakaa vizuri kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaumwa. Kichwa kinauma. Nimeambiwa nitumie lugha iliyo sahihi. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Endelea tu Mheshimiwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyofanya, nachukue fursa hii kwa dhati kabisa kuipongeza Wizara kutokana na kuleta Muswada huu muhimu ambao tunaamini baadaye utakuwa sheria, na vile vile kwa suala kubwa muhimu sana ambalo amelifanya la kuhakikisha kwamba madini ya vito yanachimbwa na Watanzania peke yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio makubwa sana. Hali kadhalika, naipongeza ile dhana ya pili kwamba pale ambapo itaonekana kwamba Watanzania hawana uwezo wa kuchimba hivyo vito, wao ndiyo watapewa leseni ili washirikiane na Mwekezaji wa nje ili sasa baadaye maisha yao yaweze kubadilika kutoka na kuwepo kwa madini. Matumaini yangu ni kwamba kwa sababu tuna makampuni makubwa ya madini na katika kipengele cha 16 cha sheria hii, kinatoa mazingira ambayo kwa sasa hivi *off course* lazima mikataba yao itakuwepo mpaka pale itakapoisha *then* tukiwa tuna-review tutahakikisha kwamba matakwa ya sheria hii sasa yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa tu kusisitiza kwamba tusije tukajisahau tukajikuta tuna *review* na matokeo yake hata madhumuni mazima ya sheria hii yasiwepo. Kwa hiyo, pale ambapo tuta-review mkataba kama ambavyo kipengele kinasema, kama mkataba ukiisha muda wake ama ukiwa *terminated of which* mimi sitegemei, tuhakikishe kwamba haya matakwa ya sheria hii yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, wakati naendelea, niungane kabisa na hoja ya *Agency* ambayo ameizungumza Mheshimiwa Zitto, kwa kupitia *order* ambayo ilitolewa na Waziri, kupitia *Executive Agencies Act* ilianzishwa kitu kinachoitwa Tanzania *Mineral Audit Agency*. Hii ilianzishwa na *GN Na.362*. Ukiangalia huu Muswada hakuna mahali popote ambapo wamezungumzia uwepo wa hii *agency*. Mimi ninayo hii sheria hapa, ukiangalia kazi ambazo hii *agency* imepewa kimamlaka inasema *Role* ya kwanza ni: “*To monitor and audit quality and quantity of mineral produced and exported by large, medium and small scale miners.*” Ukiangalia kazi ya pili inazungumzia: “*To audit capital investment and operating expenditure.*”

Mheshimiwa Spika, labda nikizungumza kwa lugha ya Kiswahili, kwanza ni kufanya ukaguzi wa ubora na wingi wa madini tulio nayo, na pili ni ku-*audit* uwekezaji ama kufanya ukaguzi wa uwekezaji uliopo na gharama ambazo wanazitumia katika kuendesha migodi yao ili baadaye sasa kuiwezesha nchi iweze kujuua katika hivi vitu viwili inapata kiasi gani baada ya kuondoa yale mahitaji ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa uwepo wa Tanzania *Mineral Audit Agency* kwa kipindi cha kifupi kuanzia mwaka 2000-2009, wameweza kufanya kazi ambayo ilikuwa inafanywa na *Alex Stewart* kwa shilingi zaidi ya bilioni 20 kwa mwaka, wao wanafanya kwa bilioni tano tu.

Pamoja na mambo mengine, katika kufanya kazi kwao kwa muda huu mfupi, wameweza kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 21 ambazo kwa makosa tu, kampuni ya *Barrick* ama kwa bahati mbaya ama kwa makusudi iliweka katika *expenditure* za uzalishaji, lakini wao walipokwenda kule na kuchunguza katika dhana nzima ya kufanya *auditing* wakakuta wameweka katika maeneo ambayo wanatakiwa wasamehewe kodi. *Barrick* ikakiri kwa maandishi kwamba tumekosea, tutarudisha kama kodi ama fedha ambayo inatakiwa kupelekwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, hii *agency* ambayo leo hii haipo hapa kwenye sheria lakini ukiangalia kazi zake kwa mapana, kwa sababu nikianza kutaja kazi zote hapa sitamaliza, ndiyo kazi ambazo hii sheria ina dhamira ya kuzitekeleza. Kwa sababu mwisho wa siku tunachoangalia ni kwa kiasi gani tunafaidi ama tunanufaika kutokana na migodi yetu. Kwa hiyo, kama sheria inatoa mazingira mazuri, lakini hatuna chombo cha kizalendo ambacho kitakwenda kufanya ukaguzi kule kwenye migodi kwa sababu hiki chombo kina wakala wake katika kila mgodi katika migodi nane. Wakala wao kila wanachofanya ni kuangalia kwa siku kimepatikana nini na kutoa ripoti.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lazima tunapotunga sheria tuangalie ni namna gani tutaweza kuitekeleza hii sheria kikamilifu. Kutokana na kazi ya hii *agency* yetu ambayo ni ya wazalendo, wala siyo ya watu wa nje, ni ya wazalendo na ambao wanatumia fedha ndogo sana, tumejikuta kwamba *GGM* ambayo inasemekana kwamba ilikuwa hailip*cooperate tax* ikaweza kulipa *tax* ya shilingi bilioni 2.5 *last year*. Kwa hiyo, hivi ni vitu ambavyo lazima tuvikuze.

Mheshimiwa Spika, naambiwa katika michakato ya Baraza la Mawaziri, hiki kitu kilikuwepo, kwa sababu ukiangalia hii sheria yake ambayo imeitunga inasema kwamba,

*“The Chief Executive Officer will exercise statutory powers as per the mining Act Cap 1,2,3”* ambayo leo hii ndiyo tunaibadilisha ama tunaifuta na kuileta sheria hii nyingine. Iweje katika ile sheria iliyopita huyu *CEO* alikuwa anatambulika kwamba *statutory power* zake atazipata kutoka kwenye sheria, sasa leo tunatunga sheria huyu *CEO* hayupo kwenye sheria kazi yake itakuwa nini? Kwa hiyo, ni lazima tu-*balance* mambo hapa. Tuangalie hiki chombo kazi yake ina manufaa ama haina manufaa? Kama mnadhani haina manufaa, sidhani kama leo hii mngewajengea maabara ya kisasa ambayo inawawezesha wao kupima hili jiwe la dhahabu ili kuweza kujua dhahabu ni ipi, *silver* ni ipi ili baadaye wawekezaji wakipeleka huko nje wasije wakadanganya kwamba katika jiwe hili labda dhahabu ilikuwa asilimia kadhaa na *silver* ilikuwa asilimia kadhaa ama shaba kwa mantiki nyingine.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani Waziri ni muhimu kama alivyopendekeza Mheshimiwa Kabwe hapa, kwamba bado tuna nafasi ya kuleta mabadiliko. Kama tumeweza kuweka agency nyingine huku ni kitu gani kinachotuzuia sisi tusiweke hii *agency* ambapo sheria iliyokuwepo zamani ilikuwa inamtambua *CEO* wake?

Mheshimiwa Spika, inawezekana labda Mheshimiwa Waziri alipotoshwa akajikuta kifungu kinatoka kiaina, lakini ana dhamira njema kama ambavyo tunaamini sisi hapa, nadhani anaweza akaleta mabadiliko ili hatimaye hii dhana nzima ya kuboresha sekta yetu ya madini mwisho wa siku ifaidishe Watanzania Wazalendo tutakuwa tumefanya jambo la busara sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ninalotaka kuzungumzia ni sheria hii kwa ujumla wake. Kimsingi kama ambavyo alizungumza Mheshimiwa Kabwe ni kwamba kuna masuala ambayo tulikubaliana, lakini kuna masuala ambayo tulijikuta hatukubaliani, tukakubaliana kwamba tuje tuyazungumze Bungeni tutajua hatua ambazo tunaweza tukazichukua.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo mimi linanitia mashata katika Muswada huu ni mamlaka makubwa aliopewa Waziri wa Nishati na Madini. Ukiangalia Muswada huu *ume-establish board* ambayo ina watalamu lukuki, lakini ukija kuangalia *board role* yake ni nini katika Muswada huu mzima ni *advisory* tu, na ushauri Waziri halazimiki kuufuata hata kidogo. Sheria inachomwambia ni kwamba kama *Board* imekushauri na hutaki kufuatana na ushauri wake unachotakiwa ni *kui-publish report* ya *Board*. Sasa unapokuwa na sheria ambayo inaunda Bodi pamoja na *committee* ya kutosha, lakini haiipi *power* siyo ya kugongana na mamlaka ya Waziri, lakini *at least* kungekuwa kuna mlango amba unamtaka Waziri kama akikataa kukubaliana na maamuzi ya Bodi atoe sababu, tukiacha hivi, siyo kila Waziri atakuwa na dhamira njema, siyo kila Waziri atakuwa kama Mheshimiwa Ngeleja au wengine, inawezekana akatoka Waziri huko anajifahamu mwenyewe ‘chizi’, akaamua kupindisha mambo kama anavyotaka yeye. Kwa hiyo, ni lazima tutunge sheria kwa kutokumwangalia mtu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mamlaka ya Waziri, kwa mfano, kuna kipengele kinachohusiana na *amendment of development agreement*, katika hiyo *amendment* inampa fursa mwekezaji kufanya mabadiliko ya mkataba, yaani kuna masuala ambayo yanaweza yakawa kwenye leseni halafu Mwekezaji akapewa hayo mamlaka ya kufanya

mabadiliko kadhaa. Vile vile inampa mamlaka mwekezaji katika suala zima la kuratibu ajira za watu, kuangalia ni namna gani anaweza akabadilisha huo mchakato.

Mheshimiwa Spika, mtu ambaye ana mamlaka ya kutoa ruhusa kwa mwekezaji kufanya hayo mabadiliko ni Waziri. Sasa unapokuwa na Waziri anayepewa mamlaka ya aina hiyo ambayo mengine ukiangalia kwa undani yanaweza yakaathiri mkataba mzima kwa sababu mkataba unaundwa na leseni, kwa hiyo, kama huyu akiruhusiwa kufanya mabadiliko kadhaa kwenye leseni inawezekana kabisa ikaathiri ile dhamira nzima. Sasa Bodi inapokuwa haina mamlaka, Waziri anaamua mwenyewe anasikiliza tu ushauri halafu hana ulazima wa kufuata, nadhani hapa kunaweza kuwa na tatizo na tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunarekebisha ili basi kila mtu aridhike kwa upande wake.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nina machache tu ya kuzungumza, lakini ninachotaka kusisitiza ni kwamba hii *agency* yetu ambayo imetungwa kisheria tuhakikishe kwamba tunafanya mabadiliko kidogo kwenye huu Muswada ili tuweze kuupitisha hasa tukizingatia kwamba kuna fedha tayari imewekezwa pale na hasa tukizingatia kwamba ina wawakilishi sasa hivi katika kila eneo na hasa ukizingatia kwamba Sheria ya Madini iliyopita imeitambua na inawatambua. Sasa inakuwa ni kitu cha kushangaza kama Sheria hii ambayo inabadilisha ile Sheria nyingine haitambui hiki kitu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima J. Mdee, na pole sana kwa kuumwa kichwa. Tunaendelea. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dorah Mushi atafuatiwa na Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani humu Bungeni na wakati huo huo ...

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana ...

**SPIKA:** Subiri kwanza Mheshimiwa Dorah, najua una haraka na Mererani, lakini baada ya Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani nitamwita Mheshimiwa Gosbert B. Blandes ambaye naye hayupo, basi tutaona hapo mbele.

Mheshimiwa Dorah H. Mushi, karibu!

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada huu uliopo mbele yetu.

Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema hata nikaweza kuwepo hapa Bungeni leo na mimi niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu ambaao ni wa muhimu sana. Kipekee namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusikia kilio cha wananchi wachimbaji wa Tanzania. Pia nampongeza sana Mheshimiwa William Ngeleja - Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Mkwe wangu - Mheshimiwa Adamu K. Malima, pamoja na Kamishna wa Madini na Wataalamu wote ambaao wamefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba Muswada huu unatosheleza matakwa ya Watanzania hasa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na kuipongeza pia sheria hii ambayo imeruhusu Madini ya vito kuchimbwa na Watanzania au na wachimbaji wadogo wadogo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Madini ya vito hasa ya *Tanzanite* yalikuwa hayahitaji wala uchimbaji mkubwa sana au mitambo mikubwa sana. Hii ilikuwa ni uoga tu hadi tukaenda kutafuta Wazungu wa kuja kutusaidia kuchimba Madini yetu ambapo Watanzania wenyewe walikuwa wameshaanza kuchimba Madini haya na hata sasa ninaamini kabisa wanawenza kuchimba na wakaleta mabadiliko makubwa katika nchi yetu, yaani wakapata ajira na tukaijenga nchi yetu kama vile ilivyojengwa *South Africa*.

Mheshimiwa Spika, nathubutu kusema kwamba Sekta ya Madini ikiweza kuweka Sheria nzuri ya kukusanya mapato ni wazi kwamba sasa Pato la Taifa litaweza kukua kwa asilimia nyangi tu kuliko ilivyo sasa hivi na pia tutaona Watanzania wakifurahia Madini katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba ikiwa sheria hii itasimamiwa vizuri, basi Serikali itafute namna nzuri ambayo itasaidia kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, niendelee pia kuipongeza Sheria hii kuteua madini ya *Tanzanite* kuwa madini maalum na ya pekee duniani. Hii tutajivunia sana kwa sababu madini haya ni maalum kwa sababu hayapatikani mahali pengine popote duniani. Kwa hiyo, naipongeza sana Sheria hii kwa kupitisha Madini ya *Tanzanite* kuwa maalum na yatangazwe duniani kote.

Lakini ninachoogopa ni kwamba kuna haja basi ya kutafuta namna ya kuyalinda Madini haya, iwepo basi Sheria inayoitwa *Export Warrant* ambayo itaweza kuyapa ulinzi madini haya kuanzia yanakochimbwa kwenye mgodi yanakozalishwa hadi kupeleka kiwandani na hadi kwenye masoko.

Nasema hivyo kwa sababu gani? Lazima Madini haya yawe na ulinzi wa kutosha na madhubuti kwa sababu watainuka watu wasiotutakia mema, watakapojuwa kwamba ni Watanzania na ni wachimbaji wadogo wadogo wanaochimba Madini haya, basi watatafuta njia nyngine ya kuweza kutengeneza Madini yanayofanana na *Tanzanite* ambayo yatakuwa ni *synthetic* na baadaye madini haya yatauzwa kwa bei kubwa huko kwenye soko la nje. Lakini baadaye utakuta wanunuzi wetu wanalamika kwamba siyo *genuine*. Kwa hiyo, itakuja kuharibu soko la Madini yetu. Naomba sana Sheria hii waangalie namna ya kuweka Sheria ya kulinda Madini haya kwa kuweka hiyo Sheria ya *Export Warrant* ambayo ni kibali maalum kwa sababu kibali hiki kitakuwa na jina la mwenye mgodi na *clean title* ya ule mgodi. Hivyo basi, kama Madini yataolewa pale mpaka kwenye soko itajulikana hata kama kutatokea watu watakaobadilisha itaonekana kwamba madini haya yametoka kwenye mgodi fulani. Hivyo, ninaomba sana hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naipongeze pia Serikali kwa kuweka mipango mizuri kwa kuliteua eneo la Mererani, yaani mji mdogo wa Mererani kuwa eneo maalum kwa ajili ya

viwanda. Sio viwanda kwa ajili ya *Tanzanite* tu, bali ni viwanda kwa ajili ya biashara nyingine. Hivyo basi, kwa *EPZ - Export Processing Zone* kuwepo Mererani itasaidia pia wakati wa kudhibiti Madini yetu haya kuyapitishia kwenye *Export Processing Zone* na kuyakata kama Sheria hii inavyosema kwamba madini yetu ni lazima yathaminishwe, yakatwe na kusanifiwa vizuri na baadaye yapelekwe kwenye masoko ya dunia.

Mheshimiwa Spika, naomba ile mamlaka sasa inayoshughulikia umiliki au kutoa hati kwa ajili ya *ku-register EPZ* Mererani ifanyiwe haraka sana ili tuanze kuwakaribisha wawekezaji waje waweke viwanda tayari kwa ajili ya kuanza kukata madini yetu na ya kuyasanifu.

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii napendekeza kwamba Kamishna hataweza kufanya kazi ya kutatua migogoro kwa sababu tunayo migodi mingi sana Tanzania na sidhani kama Kamishna atafanya kazi ya kuzunguka Tanzania nzima kwa ajili ya kutatua migogoro ya wachimbaji wakubwa na wadogo. Mimi nafikiri ingekuwa vyema kama kingeundwa chombo maalum ambacho kitashughulikia migogoro kama hii labda Mahakama maalum kama ile ya ardhi, nafikiri labda ingesaidia kuliko kumwachia Kamishna afanye kazi ya kutatua migogoro. Mimi naamini kwamba haitakuwa rahisi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie pia suala la akina mama ambao wanapewa migodi kwa ajili ya uchimbaji hasa kwenye migodi yetu ya Mererani. Kuna akina mama wengi sana wana migodi yao, lakini akina mama hawajaruhusiwa kuingia kwenye migodi. Inapotokea uzalishaji yule mama anatakiwa akae pale juu na Meneja ndiye atakwenda chini kwenye uzalishaji hatimaye kinacholetwa pale juu hakionekani.

Kwa hiyo, utakuta yule mama haendelei kabisa. Madini yatakuwa yanapita tu yanakwenda na watu wengine na yeze hatakuwa anafaidi. Mimi ninaomba kwamba Sheria hii iweke Sheria ya Wanawake waende kule chini wakadhibiti madini yao wenye kwa sababu ile migodi sasa hivi imetengenezwa vizuri, ina ngazi na ninaamini kabisa Watanzania wameshapata teknolojia nzuri ya uchimbaji na ninaamini kabisa ile migodi sasa hivi hata mimi ninaweza nikaingia mpaka kule chini nikadhibiti madini yangu. Kwa hiyo, ninaomba Sheria hii imwangalie mwanamke ambaye amemilikishwa mgodi apewe haki yake ya kudhibiti madini yake mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie habari za ushirikishwaji wa wawekezaji wanaoletwa baina ya wawekezaji na wanakijji wanaishi kandokando ya machimbo. Ni mara nyingi kumetokea minong'ono kwamba hatushirikishwi, hatujui ni nini kinaendelea na kweli ukiangalia ni kwamba wageni wanapelekwa katika eneo husika na wenyeji wako pale pale, hawajui ni kitu gani kinachoendelea. Mimi nafikiri sio haki na ndiyo maana utakuta wageni wanapokuja hawajali wale wenyeji waliowakuta. Ni kama mtu anakuingilia kwenye eneo lako kwa kweli huwezi kufurahi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuanzia sasa wawekezaji au mgeni ye yeyote anayeletwa kwenye eneo husika akutanishwe na mwenyeji na wawe *transparent*

kuwaeleza wenyeji kwamba ni kitu gani sasa kinachoendelea hapa ili mwenyeji naye aridhike.

Mheshimiwa Spika, ninaomba eneo hilo walizingatie kabisa kuona kwamba wale wananchi au wanakijiji wanaoishi katika maeneo yale wapewe nao heshima yao na vile vile wale wawekezaji wanapochimba mrahaba, ule mrahaba urudi kwenye jamii ili uweze kuleta maendeleo katika kile Kijiji husika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nizungumzie suala la yale mazingira ambayo tayari yameshaharibika sana. Mimi ningombwa kuwa sheria hii itakapopita na kuwa Watanzania watachimba madini yao wenye basi na wale waliopo wawekezaji wasije wakaibomoa ile migodi na kuiharibu na kuiweka katika mazingira ambayo wakati wachimbaji wadogo wadogo watakapokuja kuingia kuwa tena ndiyo kiama chao wafe wote, halafu baadaye tutasema ya nini basi tuliwanyang'anya tukawapa wachimbaji wadogo wadogo wakati tunapowapoteza watu wetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba eneo hilo liangaliwe na waombwe sana kwamba wasiharibu hayo mazingira zaidi wayaweke vizuri watuachie ili na sisi tuje tufaidi kama nao walivyoyafaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie *Special Mining Licence*. Ninaomba hii *Special Mining Licence* isichimbe Madini ya vito kabisa, hiyo ipelekwe kwenye mambo ya *Uranium*, Madini ya viwandani, *Iron* na *Continuum* ya madini mengine ambayo ndiyo ambayo watayawekea muda maalum. Kwa mfano, ninapozungumzia kwamba wasichimbe madini ya vito, madini ya vito yana muda. Kwa mfano, kama hawa waliochimba tuseme miaka 20, lakini hata wachimbaji wadogo wadogo wanawenza wakachimba kuanzia miaka mitano, kumi mpaka ishirini, pato la Taifa likaonekana kabisa. Kwa hiyo, ningelekeza *Special Mining Licence* ilekeze kwenye madini ya viwandani.

Mheshimiwa Spika, mimi napongeza tu na kwamba ninamshukuru Mwenyezi Mungu... (*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili hiyo!

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja. (*Makofî*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninao wajibu wa kuwaarifu kwamba mwenzetu Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro - Mbunge wa Vunjo aliishiwa nguvu, jana hali yake ikawa mbaya kutokana na msongo wa damu. Tumemfikisha Muhimbili leo asubuhi na imegundulika kwamba ana kiharusi chepesi (*mild stroke*). Hali yake ni kwamba anazungumza, na Madaktari wanaendelea kumhudumia. Nilikuwa napata vikaratasi hapa

watu wakionyesha wasiwasi mkubwa lakini nadhani Mwenyezi Mungu amemvusha katika magumu na sasa anaendelea vizuri na anaongea.

Taarifa ya pili ni kwamba, jedwali la marekebisho au mapendekezo ya marekebisho kutoka Serikalini la kurasa kumi nadhani mmekwishagawiwa. Kwa hiyo, unapousoma huu Muswada wa Sheria ya Madini huna budi kutazama na jedwali hili la kurasa kumi. Hii inadhihirisha kazi kubwa iliyofanyika baina ya Kamati na Serikali. (*Makofi*)

Mwisho, nafurahi sana kumkaribisha rafiki yangu Prof. Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, ambaye hakuwepo hapa Bungeni. Kwa hali ya kawaida unaweza kusema Waziri asipokuwepo labda yuko nje ya nchi, lakini kwa hali ya sasa fununu zinaniambia kwamba alikuwa anazima mioto pale Mwanga. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji anayefuata, ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes na wakati huo huo Mheshimiwa Job Y. Ndugai ajiandae.

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza nami nakushukuru kwa kunipa fursa hii, pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kurudi safari salama na niseme kwamba wakati nikiwa Canada nilipata fursa kupita katika Wizara ya Mambo ya Nje na kuonana na wawekezaji wakubwa wa madini wakiwa wana wasiwasi sana na Sheria hii tunayoileta sasa Bungeni. Lakini niliwatoa wasiwasi nikawaambia kwamba tunachokifanya ni kimoja tu, tugawane kile kidogo mnachokipata ninyi kwani sio mnasema mnakipata kidogo, basi angalau tugawane, ndiyo tunachokifanya kwenye sheria. Kwa hiyo, nafurahi hiyo meseji imefika na nikawaambia watutakie heri na baraka katika kuitisha sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili, ninapenda kusema kwamba nchi yetu imebarikiwa kuwa na madini mengi ya aina nyingi, lakini kwa bahati mbaya sana hatuna taarifa sahihi za wingi, aina na maeneo ambayo yana madini hayo. Taarifa zilizopo, wanazo watu wa nje zaidi kuliko tulizonazo sisi ndani ya nchi na kwa sababu hiyo, basi hata kifungu hiki cha 29 cha Sheria kinachosema kwamba tutangaze *tender*, basi *tender* inataka utangaze kwa kitu unachokijua kilipo, wingi wake, aina yake na thamani yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu la kwanza ni usimamizi wa utekelezaji wa Sheria hii. Hii sheria ni nzito, ni muhimu kwa uchumi wa Taifa letu, lakini ili isimamiwe vizuri na Serikali iwajibike vizuri kwa umma kwamba wanasmamia raslimali za nchi, Serikali lazima iwe na taarifa sahihi ya raslimali tulizonazo. Kwa hiyo, ushauri wangu kwanza, kazi ya kwanza ya Serikali ni kufanya *mapping* na inahitaji shilingi bilioni 15. Kwa teknolojia ya sasa haiwezi kuchukua zaidi ya miezi mitatu mtapata taarifa ya raslimali nchini zilizopo. Mkitaka utaalamu huu tutawaelezeni unapopatikana.

Mheshimiwa Spika, ukishatoka hatua hiyo, hatua ya pili ni kuainisha maeneo ambayo au madini yatakuwa ni raslimali ya Taifa. Kwa mfano huwezi ukaichukua *Uranium* ukampa mtu ye yeyote, ina madhara ya aina nyingi. Kwanza umuhimu wake katika kuitumia katika Taifa, lakini vile vile na mtu anavyoweza kuitumia. Kuna madini kama

ya *copper*, ambayo ni mali sana; kuna *nickel* ambayo ni mali sana kwa hiyo, kuna madini ambayo ni lazima zimilikiwe kwa kiasi kikubwa na Taifa lenyewe na ndivyo wenzetu wengi waliofanikiwa walivyofanya.

Mheshimiwa Spika, nina ushahidi wa wazi, shirika letu moja hapa liliingia ubia na kampuni moja wakielewa wao kwamba wanayo *coal* tani milioni tisini. Wageni walipofanya *exploration* kwa kutumia milioni tano wakagundua tuna tani zaidi ya milioni mia tatu. Sasa unapoingia ubia kwa asilimia thelathini ukielewa wewe una tani milioni tisini ukajajikuta kumbe baada ya *exploration* mwenzako ana tani milioni mia tatu unajikuta umeingia ubia kwa rasilimali ambayo hata wewe mwenyewe hukuijua thamani yake na wingi wake. Ndio maana nasisitiza sana ili tuweze kuingia kwenye ubia katika *fair hands*. Ni vizuri tukajua tuka-*own our products*. Tatizo letu hatuzi-*own* hizi *product* kwa sababu hatuzijui zilipo. Kwa hiyo, kazi ya kwanza naiomba Serikali katika sheria hii isimamie kujua rasilimali zetu zilipo, wingi wake na aina yake.

Mheshimiwa Spika, pili tumewaambia wachimbaji wadogo wadogo sasa mambo yao yatakuwa mazuri. Wachimbaji wadogo wadogo sheria hii hajawasaidia, imewasaidia kwa namna moja tu kwamba sasa wanatambuliwa na sheria. Lakini watafaidikaje katika sheria hii? Bado hakuna *infrastructure* ya kusema mimi nikishapata mali yangu, nakwenda kuiiza mahali fulani. Hakuna *infrastructure* ya kusema kama mimi ninao mgodi, nahitaji fedha za kuuendeleza mgodi huu. Kwa hiyo, tumepitisha sheria ya kuwaambia kwamba sasa tunawarithisha rasilimali lakini rasilimali ambayo hawawezi kuitumia kwa sababu hatujaweka *infrastructure* na ndio maana tukasema katika Kambi ya Upinzani na Wabunge wengine wote ile mamlaka inayohusika ipewe mamlaka ya kuweza kusimamia pamoja, namna gani wachimbaji hawa sio tu watakaoratibiwa, lakini watakaowezeshwa kuuza bidhaa zao ili waweze kuzitumia na kupata faida.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo tutakuwa tunaona mali, mgodi lakini umekaa nao huwezi kufanya chochote kwa sababu huna soko na hasa kwa sababu sasa wale wageni tuliowaondoa ni dhahiri unaliondoa soko. Unapowaondoa wageni, unaliondoa soko. Ukishaliondoa soko unabakisha huyu na mali yake. Kwa hiyo, yatakayotokea ni nini? Ni kuziiza kwa njia ya panya na Serikali itakosa mapato. Kwa hiyo, lazima uweke *infrastructure* itakayosaidia sio tu kama na *own money* lakini ninalo soko, ninayo teknolojia, ninao mtaji. Watanzania hatuwezi kuridhishwa mali wakati hatuna mitaji ya kufanya *investment* katika nchi yetu na ndio tatizo kubwa la Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tatu sasa nilitegemea kwamba Serikali inajenga kada ya Watanzania kuwa sio tu kwa wachimbaji wadogo wadogo angalau iwe kwenye *middle class* ya wachimbaji. Leo hapa maneno yote tunayozungumza ni kutegemea *investors* kutoka nje. Lakini hatuna promosheni ya Watanzania ku-*own* na kuwa wachimbaji wakubwa, hakuna. *South Africa* walipoanzisha utaratibu wa kusema kwanza mwaafrika apewe nafasi. Leo kuna makampuni manne yanayoongozwa na wanawake *South Africa*, wanawake, makampuni makubwa ya madini *South Africa* yanaongozwa na wanawake, kwa sababu kulikuwa na *infrastructure* ya kuwasaidia wale wanawake waweze kumiliki na kutumia rasilimali za nchi kupata mali.

Mheshimiwa Spika, sasa ili mgodi usaidie, kuna mambo manne lazima yawepo. Kwanza kama mgodi nchini upo, mgodi huo ili nchi ifaidike sio ile *reality* ya asilimia tatu, hapana. Kwanza, anapoingia yule mtu ajue kwamba nyie Serikali mnajua thamani ya mgodi wenu, kwamba huu mgodi amba tunataka kuingia ubia na wewe sisi tuna *estimate* tunazo tani milioni tatu, hatua ya kwanza.

Hatua ya pili, ni kwamba atakapoanza kuchimba zile fedha anazotaka kuchimbia zinatoka ndani ya nchi. Kwa hiyo, lazima muwe na *strong financial institutions* zitakazosaidia kuwakopesha wale, vinginevyo, atakopa nje kama wanavyofanya sasa. Watakwambia tumekopa shilingi milioni 100 kumbe walizotumia pale ni shilingi milioni 50 wataendelea wao kila siku kuchukua *dividend* kwa *amount* ambayo ni hewa.

Mheshimiwa Spika, tatu, lazima uwe na *supplies* za kusaidia. Ile *paper* ya *URE*, hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani kwamba lazima uwe na vitu vyta *ku-supply*, kama huna hivyo, maana yake watu wataagizia vitu nje ndio maana wenzetu wanachukua nyama kutoka Kenya na mahali pengine. Lakini nne, muhimu sana, lazima uwe na viwanda vinavyotoa mashine zinazohitajika katika ile *minning*. Kwa hiyo, kama huna hivyo utabaki na *reality* yako wewe ya dola tatu, dola tano, asilimia tatu, basi. Vitu vyote vingine vinakuwa vinatoka nje kila siku. Kwa hiyo, kufaidika kama Taifa, hatufaidiki.

Kwa hiyo, nasema *the whole programme* ya kufaidika katika madini hatujaipanga. Hatujaipanga hata kidogo! Kwa hiyo, tutaendelea kufikiria tu kwamba sheria hii itatusaidia, mimi nasema bado kazi kubwa tunayo ya kuifanya sheria hii bado iwafaidishe Watanzania. Hii sheria bado ina kazi kubwa ya kufanyiwa. Sina hakika kama Wizara ina *capacity* hiyo. Ndio maana tunashauri taasisi nyingine ziundwe ili kusaidia hii Wizara iweze kufanya kazi.

Unapomwingiza na Kamishna naye akatatue mgogoro atakaa saa ngapi ofisini kushughulikia mambo mazito? Unapomwambia Waziri kwamba kama kitu uamue wewe atakuwa atakuwa na muda gani Waziri wa *ku-sign* mikataba mizito mizito? Kwa hiyo, tunahitaji kuunda *institutions* za kuweza kusimamia hii sheria. Hii ni *industry* kubwa, sio *industry* ndogo. Juzi Canada wamepitisha sheria, Kambi ya Upinzani pale Canada wamepeleka Muswada wa sheria kuomba kwamba makampuni yao yote yaliyoko nje lazima vile vile ya-*invest* katika *social sector* katika nchi hizo, wamefanya wenzetu wa *Canada*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kugundua kwamba makampuni yao yanatengeneza hela nyingi, lakinivile kuna migogoro huko wanakotoka, sasa sisi hapa tunakataa kutoa asilimia ishirini ya *reality* kuwapa Kahama ambapo wataachiwa maradhi ya vifua vikuu. Wataachiwa mashimo, hawaachiwi kitu chochote pale zaidi ya hicho. Mimi nasema bado hatujatengeneza *infrastructure* ya kuitumia *minning industry* ikakuza uchumi wa nchi. Kwa hiyo, nahitaji Waziri asipende sana kuchukua madaraka mengi katika hii sheria wala Kamishna, tujenge taasisi zitakazosaidia kusimamia hii migodi. Tuna *STAMICO*, tuipe jukumu *STAMICO* kusimamia wachimbaji wadogo wadogo, wana *technical know how*. Sasa hivi *STAMICO* wanazo *drilling machines* nzuri, wanawenza

wakasimamia vizuri *STAMICO* wachimbaji wadogo wadogo na wakapata ujuzi ndani yao.

Mheshimiwa Spika, tunayo *MBC*, tuirithishe maeneo makubwa ya migodi yetu kama *uranium* na kadhalika ili wawekezaji watakopokuja, Serikali nayo iwe na *stake* ndani yake. Mimi nashangaa Ghana ukienda huwezi kampuni ye yote kuingia pale kama haina angalau asilimia tano au kumi ya Serikali na huwezi kuingia kama huna Mghana vile vile. Lakini sisi sasa tumeachia kila kitu holela tu, hatufiki huko. Hatutafika huko, tunahitaji kuwarithisha Watanzania mali zao ama kwa kupitia wao wenyewe au kwa kupitia taasisi zao. Kwa hiyo, ushauri wangu sheria hii ni nzuri na marekebisho tuliyoyapendekeza naamini yatapita. Ninachoomba tujenge taasisi za kusaidia utekelezaji wa sheria hii. Tusitoe madaraka kwa mtu mmoja mmoja, hatasaidia.

Mheshimiwa Spika, pili, lazima tutengeneze *infrastructure* na Waziri tunategemea katika bajeti hii atatueleza wachimbaji hawa wadogo wadogo watapata wapi mitaji ya kufanya shughuli zao. *STAMICO* watawapa elimu ya aina gani? Soko lao la bidhaa litakuwa wapi? Hapo ndio tutaona kweli wachimbaji wadogo wadogo watakuwa wamefaidika. Ahsante sana.

**MHE.GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi binafsi nimesimama hapa, nitakuwa na machache sana ya kuzungumza. Lakini kwanza kubwa kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri ambaye ameleta sheria hii. Yeye binafsi Mheshimiwa Ngeleja pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Adam Malima, kusema ukweli kazi hii haikuwa ndogo mpaka imefika hapa, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wameileta hapa mbele yetu. Siku zote huwa nasema navutiwa sana na utendaji wa Mawaziri wetu hawa wawili, Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Adam Malima. Kwa kweli kazi zao zinakwenda vizuri sana, nawapongeza sana. Kasoro ndogo ni pale wanaponinyima umeme vijiji kwangu tu.

Mheshimiwa Spika, sheria hii ambayo ipo mbele yetu kwa kweli ni nzuri na kama kuna mapungufu ni ya kawaida yanaweza kurekebishwa, kwa lugha ya Kiingereza tunasema kwamba ni *curable*. Lakini pia ni sheria nzuri sana katika historia ya nchi yetu. Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia sheria hii imejaribu kutatua matatizo mengi ambayo tumekuwa nayo huko nyuma, kuna vipengele ambavyo mimi binafsi nimevutiwa sana. Kwa kuanzia, kuna kipengele Na. 109, kipengele hiki kinazungumzia ku-*list shares* kwenye *stock exchange*. Maana yake ni nini?

Ni kwamba kwa kipengele hiki kwa sheria hii kama tutapitisha leo ni kwamba, kuanzia kupita kwa sheria hii, wananchi wetu, Watanzania, wazawa pamoja na Serikali kwa ujumla watakuwa na uwezo, watawezesha na wenyewe kumiliki hisa katika sekta ya madini. Hii ndio mwanzo wa Watanzania na wenyewe kufaidi rasilimali yao ambayo wamepewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, binafsi kwa kweli naipongeza sana, hatukuwa nayo hii na mimi ninadhani itawasaidia Watanzania walio wengi. Lingine ambalo nimevutiwa ni kwamba sheria kabla ya kuletwa hapa ni kwamba siku za nyuma katika migodi mingi ambayo inachimba dhahabu na madini mengine, tumekuwa tukishuhudia kwamba tunapoteza mapato yetu kama nchi. Utakuta kwenye migodi mbalimbali vyakula vinatoka nje ya nchi, hata ndizi ambazo zinalimwa pale Karagwe wanaagiza pengine kutoka *South Africa*, kutoka Ulaya na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa sheria hii, kama itapita nimefurahishwa sana na kipengele ambacho kipo ndani ya sheria kwamba vyakula vitakuwa vinatoka kwenye nchi yetu, vinakwenda kwenye migodi ili na wananchi wetu waweze kupata vipato. Nimefurahi sana kwa sababu wananchi wetu ni wakulima ni wazalishaji wa mazao ya vyakula, nyama , maziwa na mengineyo.

Kwa hiyo, nina imani itasaidia sana kuongeza kipato cha wananchi. Lakini pia nimefurahishwa sana na kipengele cha kuonesha kwamba Serikali na yenyewe inaweza ikamiliki ikawa na masilahi katika migodi hii kwa kununua hisa katika makampuni ya madini. Lakini lingine ambalo ni muhimu sana ukisoma kipengele Na. 108, kipengele hiki kinahusiana na madini ya aina ya mionzi na madeni haya yamewekewa utaratibu mzuri mno ndio maana nikaanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwamba wameweka utaratibu kwamba madini ya namna hii, yenyе mionzi hayataweza kuchimbwa kiholela, hataweza kuingizwa, hayataweza kusafirishwa bila kupata *consent* au kibali cha Tume ya mionzi ya *atomic commission* ambayo iko Arusha.

Mheshimiwa Spika, hili jambo zuri sana kwa ajili ya usalama wa wananchi wetu. Lakini lingine katika sheria hii kuna mapungufu madogo mimi nimeyaona. Upungufu ambao umezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni ule upande wa utatuza wa migogoro. Migogoro inapozuka kati ya wachimbaji labda na mchimbaji mwenzake, migogoro inapozuka kati ya mchimbaji na wananchi wanaomzunguka pale, hapa bado sheria haijaka vizuri. Nami nilitaka kupendekeza kwamba kifungu hiki kwa busara ya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kama nilivyoanza kuzungumza watumie busara wakifute kabisa wala sio ku-*amend*.

Kwa sababu kifungu hiki kwa kweli hakileti *mantic*, kinajaribu kuiharibu sheria nzima. Kwa sababu unapochukua majukumu ya kutatua migogoro mizito ya madini ukamkabidhi mtu mmoja ambaye ana *title* ya Kamishna, kwanza Kamishna ameajiriwa kufanya kazi ya Kamishna, anayo *job description* yake ambayo inahusiana na kazi zake. Huyu Kamishna ni mtu mmoja na sio mtaalamu wa sheria, hana kabisa taaluma ya sheria. Kamishna huyu ni mtu anachoka. Siku moja niliwahi kufika kwenye ofisi ya Kamishna tukiwa na matatizo ya migogoro ya wachimbaji wadogo wadogo, tuliingia mle kuanzia saa 10.00 Kamishna ameanza kutusikiliza kwa sababu kesi ilikuwa ndefu amesikiliza mwisho akaanza kusinzia pale kwenye Kiti. Sasa tukawa tunamwamsha tunamwambia Kamishna tunaomba utusikilize. Lakini huyu mtu unamwonea kwa sababu anachoka na ana kazi nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema hiki kipengele hakina maana hata kidogo na kama tukiacha hapa, *mantic* yote ambayo imetunga hii sheria, itakuwa imepotea. Nilikuwa napendekeza kama walivyozungumza Waheshimiwa wenzangu kwamba Mheshimiwa Dorah Mushi amezungumza kwamba pengine tuwe na *minning tribunal*.

Wengine wamezungumza kwamba tuwe na taasisi mbalimbali, lakini nilikuwa napendekeza kwamba hili sheria iweze kukaa vizuri. Tunataka, tusitake lazima tuwe na *authority*. Mining *authority* hiyo ni lazima.

Kama ambavyo tumekuwa na *authorities* mbalimbali na tunaona zinafanya vizuri, mfano mzuri ni wa *TICLA*, tunaona inafanya vizuri mno katika industry ya mawasiliano. Sasa tukitaka mabadiliko, mapinduzi katika masuala ya madini, lazima tuwe na *mining authority* ambayo yenyewe itashughulikia masuala yote ya madini. Lakini kumuachia Kamishna afanye kazi hizi, kwa kweli naomba kusema kwamba tutakuwa tunampa mzigo ambaio sio wake na mwisho wa siku atachemsha, kesi zitalundikana, itakuwa mgogoro juu ya mgogoro.

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Waziri atanielewa katika hili. Lakini pia haya sio maneno yangu mimi kama Blandes. Hata ukisoma, Tume ya Bomani ilipendekeza kwamba tunapopendekeza kuwa na Kamishna wa Madini kusikiliza migogoro, ni jambo ambalo linachelewesa kabisa kwanza haki, lakini pia linaharibu kabisa taswira nzima ya kitu tunachotaka kukifanya hapa. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba kwa kuzingatia Tume ya Bomani na ushauri ninaoutoa ni vizuri kabisa kifungu hiki tukifute na tuweke kifungu kingine ambacho kina *establish authority*.

Mheshimiwa Spika, ukisoma kifungu cha 105 ambacho kinazungumzia ni vipi Kamishna atawenza kutengeneza utaratibu wa kuwasilisha malalamiko. Kifungu hiki kinasema hivi: “*The Commissioner may make rules providing for the initiation and conduct of proceedings*”.

Sasa hapa ukiangalia kifungu hiki, sina uhakika kwenye *amendments* sikuangalia vizuri, lakini kama kitabaki hivi kwamba Kamishna anaweza akafanya au asiweke *rules*, sasa akikataa tunafanyaje? Sasa mimi nilikuwa napendekeza kwamba iwe ni lazima, iwe ni *mandatory* kwamba lazima Kamishna atengeneze utaratibu kama kifungu hiki kitakuwa kimepita. Vinginevyo, kuacha hivi tunawenza tukapata Kamishna mzembe sana asitengeneze utaratibu na ikawa ni *chaos*, mtu asijue kwamba anadai haki yake, lakini utaratibu wa kudai haki yake ukoje?

Mheshimiwa Spika, wamezungumza wenzangu kuhusiana na masuala mazima ya *tanzanite*, nilibahatiwa kuishi pale Arusha. Nimekuwa nikiona wachimbaji wa *tanzanite* jinsi wanavyoathirika. Wale vijana wanatumukia shimoni, wanachimba *tanzanite* yao, haina soko, lakini mimi katika hili nimefurahishwa na jambo moja kwamba tumetunga sheria ya kulinda vitu vyetu kwamba vichimbwe na Watanzania peke yao.

Hili jambo mimi limenivutia sana, kwamba *tanzanite* na madini mengine kama rubi na mengine yachimbwe iwe ni kwa faida ya Watanzania. Hii ni sahihi kabisa, lakini pia nikavutiwa kwamba kama mtanzania atakuwa amepata leseni ya kuchimba vitu vya

thamani na kwa bahati mbaya akawa hawezi anataka kuingia ubia, nimeona ndani ya sheria hii kwamba, Mtanzania anaweza kuingia ubia na mwekezaji kutoka nje ili mradi asizidi asilimia hamsini.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo, kwa nini huyu mtu anaanza kutafuta mbia kutoka nje? Kwa nini mtu huyu asiende benki akapata mikopo, akawenza kuchimba vizuri na akapata faida kubwa? Ndio hiyo amesema mwenzangu aliyemaliza kuchangia, ni vizuri hawa watu tukawawekea utaratibu wa kupata mikopo katika benki na wenyewe waweze kuchimba na kuweza kufaidika.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nilitaka nizungumzie ni kile ambacho kinahusiana na *Advisory Board*, nimeiona, nimeisoma nimeielewa kwa makini. Ni vizuri hawa watu tukawawekea utaratibu wa kupata mikopo katika benki na wenyewe waweze kuchimba na kuweza kufaidika.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nizungumzie ni kile kipengele kinachohusiana na *Advisory Board*. Nimeiona nimeisoma, nimeielewa kwa makini, lakini nimeshindwa kuelewa umuhimu hasa ni upi. Kitu kinashauri tu kwamba kumshauri Waziri na wanasma Waziri anaweza akapokea au asipokee. Sasa kazi yake ni nini? Mimi nilidhani *Advisory Board* kama tunataka iwepo, basi tuipe majukumu mengine ya msingi, yaeleweke, lakini siyo ushauri tu peke yake. Nadhani kuwa na *Advisory Board* ambayo haina majukumu ya msingi na yenye siyo busara.

Mheshimiwa Spika, lingine nimevutiwa na kipengele cha 43 ambacho kinazungumzia muda wa kuchimba madini. Nashukuru kwamba Sheria hii imekiweka vizuri sana na wananchi wasiwe na wasiwasi. Wametueleza muda wa kuchimba madini kutegemea na yale madini ambayo yatakuwa kwenye kishapu. Kwa hili limekaa vizuri na ninakubaliana nalo kabisa wala hakuna tatizo na baada ya *feasibility study* kufanyika ni kwamba muda utaonyeshwa. Nashukuru mno.

Mheshimiwa Spika, siku zote wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakipata shida. Kwa mfano, kule Geita kuna wachimbaji wako Mgusu, ni karibu mwaka wamesimamishwa kuchimba madini kule Mgusu, na hawajui hatima yao, wanashindwa kupeleka watoto shule.

Hawa wachimbaji wadogo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, tena huko ndio Mkoani kwake, awaangalie wale wachimbaji wadogo wadogo wale wa Mgusu, wamefungiwa muda mrefu, basi aone uwezekano wa kuwafungulia awape leseni ikiwezekana wiki ijayo na wenyewe waweze kufaidika na rasilimali za nchi yao.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Karagwe. Wananchi wa Karagwe siku zote wananiuliza wanasma, Mheshimiwa Mbunge, mbona madini yetu sisi hatusikii fununu kwamba madini yetu yatachimbwa lini? Mimi binafsi sina elimu ya kutosha kuhusiana na madini. Pengine ningependa Mheshimiwa Waziri anaposimama akaeleza sisi Karagwe madini tulionayo ni yapi na kwa nini wawekezaji hawaji kuchimba huko na sisi wananchi wangu waweze kupata mikopo, waje wachimbe madini huko jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa wananchi inatakiwa sana. Suala la madini ni geni kwa nchi yetu, na siyo kwa wananchi wa hali ya chini hata wale wakubwa. Tunahitaji kupata elimu kuitia vyombo vya habari, magazeti, redio na kadhalika ili tujue kwamba madini yenye we yako wapi. Ukimchukua mtu wa Kigoma, ukimchukua mtu wa Tanga hawezi kujua kwamba hata kama anataka kuchimba madini, hana elimu ya kutosha katika hii *industry*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana hata baada ya Sheria hii kupita, wale *Zonal Managers* na Wizara ijipange vizuri. Watu waelimishwe, wajue madini gani tunayo hapa nchini na wanafanyaje kuweza kuyavuna.

Mwisho, kama nilivyosema niendelee kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, niwapongeze. Kama nilivyosema, ni kati ya Mawaziri ambao kwa kweli wananiutia sana katika utendaji wao wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Gosbert Blandes. Sasa namwita Mheshimiwa Job Ndugai, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na Mheshimiwa Yono Kevela ajiandae.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kumshukuru Mheshimiwa Waziri Ngeleja, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Kamishna wa Madini na Wataalam wao wote kwa kazi kubwa walioifanya kutuletea Muswada huu ambao kwa miaka takriban minne na kitu tumekuwa tukipiga kelele kwamba tunauhitaji kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasema sana nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa jinsi mliviyoshirikiana nami katika msiba ulionipata wa kufiwa na mama yangu mzazi, Mdala Zaina Chonya kule Kongwa, ilikuwa tarehe 5 Aprili na tukamzika tarehe 8 Aprili, 2010. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote. Namshukuru Baba Askofu Chimeledya kwa kushiriki, Viongozi wote wa Serikali Mkoani Dodoma, Viongozi wa Chama ambao tulishirikiana nao, bila kuwasahau wananchi wa Kongwa ambao kwa kweli walijitokeza kwa wingi sana. Sina cha kuwapa, nasema ahsante sana. Mwisho, niseme kwamba Mwenyezi Mungu tunakuomba uiweke roho ya Marehemu mama yangu mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati akiwasilisha Sheria yake kwetu amefanya hivyo kwa ufundi mkubwa sana. Kwa kweli jambo hili gumu amelirahisisha kwa kulieleza kwa mapana na marefu na kwa usikivu wake wa kazi kubwa ambayo imefanyika katika ngazi ya Kamati ambayo inashuhudiwa na marekebisho mengi ambayo Serikali imeyakubali, inaonyesha nia njema ambayo kwa kweli Serikali yetu inayo katika kuhakikisha kwamba tunafaidika na rasilimali hii ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu katika nchi yetu. Amesema kwamba sheria, kanuni na taratibu ambazo tunazo na

marekebisho tunayafanya yanatufanya Tanzania tuwe ni moja ya vivutio vikubwa kabisa katika Afrika kwa uwekezaji katika Sekta ya Madini. Hili ni jambo jema la kujivunia.

Lakini nikumbushe tu kwamba cha muhimu pamoja na kwamba sisi ni *destination* mzuri sana kwa ajili ya wawezekaji, lakini pia niulize swali ambalo hata Kamati imeuliza kwamba ni mchango kiasi gani ambao Sekta hii inachangia katika uchumi wa nchi yetu na kwa maana hiyo katika maendeleo yetu? Kwa hiyo, ni jambo hata baada ya Sheria hii lazima tuendelee kujiuliza mara kwa mara: Kukua kwa haraka kwa Sekta hii kunachangia nini katika uchumi wa nchi yetu? Kwa hisia zangu na Watanzania wengi ni kwamba mchango wake ni kidogo sana, haiwagusi sawasawa, fungamanisho lake ni duni ukilinganisha na sekta hii na sekta nyingine ambazo zinapaswa kwenda kwa pamoja na kwa haraka na mchango wake bado ni duni.

Mheshimiwa Spika, naamini katika eneo hili litafanyiwa kazi ili na lenyewe liweze kuboreka vizuri. Ramani nyingi katika nchi yetu kwa maana ya *geological survey* na *mapping* ambazo zimefanyika za masuala ya madini baadhi yake zimefanywa na Warusi watu wa kutoka nchi ya Russia na kwa hiyo, maandishi yake mengi yako katika *Russian*. Sisi Chuo Kikuu cha Dodoma kama nilivyosema asubuhi mwakilishi wenu yuko pale, tumeanzisha *Centre of Excellency* ambayo tunaianzisha hivi sasa ya Afrika Mashiriki mzima kwa ajili pamoja na mambo mengine kufundisha Kirusi. Lengo letu mojawapo ni kufikia mahali ambapo wenzetu wa mataifa haya wanapofanya kazi za namna hii za kitaalam za kuweza kupima utajiri wetu tulionao, basi tuweze kuwa na Watanzania wanaoweza kutafsiri *information* hizo ili ziweze kufaidia Taifa letu kwa kiwango kikubwa.

Naamini Mheshimiwa Waziri katika kushirikiana ku-up grade Chuo chetu Madini cha Dodoma tutashirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma katika jambo hilo ili tuhakikishe kwamba ramani tulizonazo katika nchi yetu ziwe zimefanywa na Wajerumani, ziwe zimefanywa na Warusi iwe ni Waarabu au mataifa mengine yoyote tunao Watanzania amba ni wataalam kabisa katika lugha hizo ili tuweze kufaidika na rasilimali tulizonazo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 37 wa Sheria hii na hasa fungu 43 linalozungumzia habari ya kutoa leseni *special mining licence* kwamba itatolewa kwa *applicant* kutegemeana kwa lugha iliyoko katika Sheria hapa kutegemea na *estimated life of the Board*, kutegemea na mali iko kiasi gani katika eneo lile. Jambo hili linanipa mashaka makubwa kwa sababu kwa vyovyyote vile makampuni makubwa yataweka *consultancies*, yataweka wataalam watakaowaambia mali iko kiasi gani.

Uzoefu unaonyesha, Kamati yangu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira tulipotembelea kwa mfano *Geita Gold Mine*, tulikuta kulikuwa na makadirio ya kwamba iko dhahabu kiasi gani wakati ule walipokuwa wanapewa leseni. Lakini wanapopata leseni siyo kwamba wanaacha kuendelea kutafiti, wanaendelea na utafiti, *exploration* na wanagudua mali nyingine. Kwa hiyo, uko uwezekano mkubwa sana kama sisi hatuna wataalam wetu wenyewe au hatuna *system* ya kuweza kujuu kama hiki walichosema *consultant* wa mwekezaji ndicho kitu halisi, tutajikuta katika eneo hili tunababaika

kidogo. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali ijizatiti katika eneo hili la kujua wapi iko mali, iko mali kiasi gani, sisi wenyewe tuweze kufahamu jambo hili. Vinginevyo litatusumbua sana hili jambo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, ningependa kuzungumzia vile vile kutokana na uzoefu wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira tulipotembelea Mgodi wa North Mara, Mgodi wa Buzwagi na Mgodi wa Geita, migodi yote ni ya dhahabu kwa Kampuni mbili tofauti. Ni kwamba tulikuta malalamiko mengi sana kwa wananchi. Mengi sana! Malalamiko haya yako katika migodi mingine pia. Malalamiko haya yako kwenye sehemu mbili kubwa. Sehemu moja ilikuwa ni uharibifu wa mazingira. Sasa kweli iko Sheria ya Mazingira. Lakini Sheria ile ya mazingira ilipotungwa mwaka 2004 haikuwa *ime-capture* sawasawa changamoto mbalimbali zinazotokana na athari za mazingira katika zoezi la uchimbaji wa madini.

Kwa hiyo, ningetarajia hapa pangekuwa na kifungu ambacho angalau kinashughulika na masuala haya ya kuzingatia hifadhi ya mazingira. Lakini bahati mbaya sijakiona. Kwa mfano mabwawa ambayo yanabeba sumu baada ya matumizi ya mgodi, wao wanayaita *TSF*. Mabwawa yale kwa migodi ya kisasa ni lazima yawe na *lining* yawe na mikeka ambayo inahakikisha au mazulia ambayo yanahakikisha kwamba yale maji ya sumu hayavuki kwenda katika ardhi na kwa maana hiyo kuingia katika *system* ya maji yanayopita chini ya ardhi na kwa hiyo, kuchafua vyanzo vya maji na kuleta hatari kwa maisha ya wananchi, mifugo yao, mimea yao na kwa ujumla viumbe hai. Sasa nilitarajia kabisa katika Sheria hii pangekuwepo angalau na kifungu kinacholazimisha jambo hili la mabwawa ya sumu yote katika nchi yetu kuhakikisha kwamba yanawekewa mazulia ya aina hiyo ya kuzuia maji yasiweze kupenya kwa sababu hilo halipo katika Sheria ile ya Mazingira ya mwaka 2004 na kwa sababu sio *requirement* ya Sheria ya Mazingira kwa sasa.

Kwa hiyo, kuna hiyo *leeway* ya mwekezaji ama kuweka, ama kutokuweka na kwa sehemu kubwa kwa mfano mgodi wa North Mara tatizo lile la mazingira lilitokana na kwamba mabwawa yake yale ya sumu hayana mazulia hayo. Kwa hiyo, natarajia kwa sababu muda bado tunao, Mheshimiwa Waziri kama kuna mahali tunaweza tukaweka jambo hili tuliweke. Kwa sababu ni muhimu sana katika Hifadhi ya Mazingira. Cha pili kutokana na uzoefu wa wananchi wa maeneo hayo, yako mengi. Lakini mawili haya ni makubwa. Ni malalamiko makubwa kwamba wananchi hawafaidiki na kuwepo na uwekezaji mkubwa wa madini wa kiwango hicho katika maeneo hayo, hawafaidi vya kutosha. Sasa hili tumewaachia wawekezaji kufanya wanavyoona wao kama hisani hivi. Nilidhani jambo hili lisiwe hisani moja kwa moja. Tuwabane kidogo wawekezaji, wawajibike kwa namna moja au nyingine na maendeleo ya maeneo ambayo wanayafanya kazi ili pawe na mabadiliko yanayoleta tija kwa wananchi wale.

Lakini vile vile fidia ambayo inatolewa kwa wananchi ambao inabidi wahamishwe kwa sehemu kubwa fidia hizi zinatawaliwa na Sheria ambayo iko kwenye Wizara ya Ardhi, Sheria ya Fidia kwa ujumla kwa mwananchi anayeondolewa mahali kwenda pengine. Suala la Sheria hii moja kwa moja kwamba kwa kweli uko umuhimu basi wa Sheria hiyo ambayo iko chini ya Wizara ya Ardhi na yenyewe ikaja kwa haraka.

Wananchi wetu wanaondolewa kwa fidia ndogo ndogo sana. Kule tulikokwenda angalau zile kampuni zinajaribu kufanya *top up* zenyewe, kwa kuwaonea huruma wananchi wale kwa kuona jinsi ambavyo wanapata kitu kidogo sana. Kwa hiyo, Sheria ya Fidia ambayo inalalamikiwa sana na yenyewe ni vizuri ikaja haraka ili tuweze kuirekebisha.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo la utoaji wa leseni za masuala ya madini, iwe *prospecting*, iwe ni *mining* na kadhalika zile leseni zinapotolewa na Kamishna wa Madini au mahali fulani, Makao Makuu ya Wizara hakuna *consultation* na Halmashauri ya Wilaya wala Kijiji husika, wala eneo husika. Wao wanatoa tu kama Dodoma, kama ni Dar es Salaam, popote pale nchi hii. Kwa hiyo, unaweza ukakuta una nyumba yako huko sijui wapi, wenzako wameshatoa eneo hilo ni la kuchimba madini. Sasa Serikali za Vijiji hazihusiki chochote, Halmashauri ya Wilaya haihusiki chochote. Wanaona tu mtu anakuja, anaanza shughuli zake, wakati katika maeneo mengine yote ya kiserikali kunakuwa na *consultation* fulani, hapawi na maamuzi tu ya Serikali Kuu moja kwa moja halafu basi, ndiyo *final*. Sasa nilidhani katika Sheria hii iko haja kwa kweli ya kuwa na mawasiliano na kuonekena uwajibikaji wa huyo aliyepewa leseni kwa kijiji husika, anawajibika vipi kwa Halmashauri husika? *Unlike* hali ilivyo sasa hili linapaswa litazamwe na ikiwezekana lifanyiwe mabadiliko tuwe na *consultation*.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 109, mimi nimefurahia sana, linahusu masuala ya *listing* kwenye *stock exchange* kwamba Waziri atapewa madaraka na wataweka *regulations* kuhusu masuala yanayohusu *minimum share holding* kwenye masuala ya *ku-list* kwenye *capital markets* na *securities*, lakini vile vile kwenye *stock exchange*. Lakini kinachonikwaza kwenye kifungu cha 109, kinasema: “*the Minister shall in consultation with holders or special mining license,*” sijui *consultation* ile ya nini? Nashauri ile *consultation* iondoke, Waziri awe na mamlaka kamili. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Namwita sasa Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, atafuatiwa na Mheshimiwa Yono Kevela, ajiandae Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi nichangie kidogo kuhusu Muswada huu. Nimefarijika kidogo kutokana na *Schedule of Amendments* ambapo mengi nilikuwa nieleze, lakini kwa bahati yamekuwa *captured humu*. Lakini mbali na hayo, katika ibara ya pili ambayo nafurahi kwamba imerekebishiwa, lakini hii ibara ya pili ukiisoma pamoja na ibara ya tano katika ukurasa wa 12 nafikiri pia ibara ya tano nayo inahitaji marekebisho. Inahitaji marekebisho kwa sababu kama ilivyo ibara ya pili kwamba madini sio suala la Muungano na katika ibara ya tano imeelezea wazo kwamba, wamesema hapa kwamba *subject to the provisions of this Act the entire property and control of the minerals or in or under the land to this Act applies as vested in the United Republic.*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa nahisi kuna tatizo kwa sababu kwa mfano unapokuta madini kama *diamond* ambayo yako chini ya bahari na utaikuta hii iko katika Mashariki ya Chwaka kwa mfano katika Kisiwa cha Zanzibar, sasa kwa mujibu wa ibara

ya tano inaweza ikaleta matatizo. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri ibara ya tano pia ajaribu kuirekebisha ili iende sambamba na ibara ya pili.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya tisa ukurasa wa 15, hapa wanasema kwamba hizi *mineral rights* ambazo zinawekwa hapa zinaweza zikatolewa, lakini *subject to subsection two, no special mining license, or any divided proportion net part of shall be assigned to another person without a written consent of the Licensing Authority*. Sasa wasiwaso wangu ni kwamba hii *consent* ya *Licensing Authority*, inaweza ikawa na matatizo kwa sababu anaweza akatoa au akasaini hii leseni kwa njia nyingine ambazo sio halali. Sasa je, kuna ulazima wowote wa *ku-assign* hizi *mineral rights*? Mimi nilikuwa nafikiria utaratibu huu wa *ku-assign* labda pengine ungelikeweka masharti mengine ambayo yatahakikisha *Licensing Authority* hawezi akaisaini kwa utaratibu ambao anataka yeze.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 14 katika Ibara ndogo (2), hapa anasema kwamba wale watu ambao wanaomba au *wame-tender* katika suala la kuchimba madini, ikiwa kuna watu wawili ambao wamepeleka tenda zao siku moja, basi anayehusika yaani *Licensing Authority*, yeze ndio ataamua ni nani wa kumpa kati ya wawili wale.

Mheshimiwa Spika, nafikiri huu sio utaratibu mzuri kwa sababu, katika watu wawili wale ni lazima kuna mmoja ambaye ametangulia kwa masaa. Sasa nafikiri sheria ingeweka utaratibu kwamba yule ambaye anakwenda mwanzo, hata kama wote wawili wamekwenda katika siku moja lakini yule anayekwenda mwanzo ndio afikiriwe. Kwa maana hiyo, kuna utaratibu ambapo mtu ambaye ana-tender anapeleka tenda yake na anaweka muda ambao ameweke ile tenda. Sasa kwa maana hiyo, atajulikana ni yupi aliyekwenda mwanzo. Kwa hiyo, napendekeza kwamba watu wa aina hii watazamwe kwa mujibu wa muda ambao wamekwenda.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 23 hapa inasema kwamba *Minister may amend any provisions of this schedule*, lakini haikueleza ni *schedule* gani. Kwa sababu katika sheria hii kuna *schedules* mbili, *schedule* ya kwanza na *schedule* ya pili. Sasa nafikiri ingewekwa hasa ni *schedule* gani ambayo Waziri anaruhusiwa *ku-amend*. Lakini pia inasema kwamba Waziri, anaweza akakubali au akakataa ushauri ambao amepewa na Bodi. Sasa nafikiri anapokataa ni vema kwa utaratibu wa kiutawala bora, huyu Waziri atoe sababu ambazo zinamfanya akatae ushauri ule.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 35 ambao huu ni pamoja na ukurasa wa 37 katika vifungu vyta Ibara ya 41 na ibara ya 42 pamoja na Ibara ya 49, hizi zote wanasema kwamba: “*Application for Special Mining License shall be in the prescribed form and shall be accompanied by the prescribed fee*”.

Mheshimiwa Spika, wasiwaso au tatizo langu ni kwamba hata unapopeleka *application* ndio wakati ule ambapo unatakiwa uweke zile ada, au zile ada zinakuja baada ya kukubalika ile *license* ambayo umepewa? Sasa ikiwa ni hivyo, unalipa *fee* baada

ya kukubalika, kwa hiyo nafikiri Ibara hizi zinahitaji angalau marekebisho kidogo ili kuonekana kwamba zile *fees* zinalipwa mara baada ya kukubaliwa. Lakini unapopeleka *application* na ukaweka *fee* nafikiri hiyo inaweza kuleta matatizo kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 71, Ibara ya 103, hapa ndio kuna matatizo makubwa kwa sababu inasema kwamba, Kamishna yeye ndio atakuwa kama ndio Hakimu. Sasa Uhakimu huu ambao anaufanya amepewa nguvu gani za kisheria na je, mtu ambaye atakuwa *aggrieved* na ushauri huu au na maamuzi haya ambayo yatatolewa na Kamishna? Je, kuna utaratibu wowote wa kwamba mtu huyu anaweza ku-*appeal*? Hayo hayakuelezwa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri huu sio utaratibu mzuri kwa sababu Kamishna huyu amepewa nguvu nyingi sana za kisheria ambazo kwa utaratibu wetu haiwezekani kupewa nguvu hizo. Kwa hiyo, nahisi labda kifungu hiki kingerekebishwa kidogo ili kuzipunguza hizi nguvu za Kamishna, kwa utaratibu unaoleweka kwa mujibu wa utawala bora.

Mheshimiwa Spika, halafu katika sheria yote hii kuna kitu kimoja ambacho sikukiona, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri anifahamishe. Tumezungumzia kuhusu wachimbaji wadogo wadogo na humu tunesema kwamba madini aina fulani ambayo yamewekwa humu, hayo yatahusiana na wachimbaji wadogo wadogo. Sasa utaratibu wote ule wa wachimbaji hawa wadogo wadogo kuhusiana na utaratibu wao, namna gani wanaweza wakafanya shughuli hizo, namna gani wanaweza wakazi-*dispose* au kuziua au kufanya mambo yanayohusiana na hayo na kwa utaratibu gani, hazikuwekwa katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kwamba, tunapoacha hivi hivi, tunatoa mwanya kwa hawa wachimbaji wadogo wadogo waweze kutafuta njia nyingine za kwao wao ambao wanazijua. Baadaye ndio utaona kwamba wachimbaji wadogo wadogo mara wamekwenda Kenya au wamekwenda nchi nyingine kwenda kuuza madini yao. Kwa hiyo, nahisi hii sheria ina kasoro moja kubwa ambayo ni hiyo, haikuweka hasa utaratibu wa wachimbaji wadogo wadogo katika mwelekeo mzima wa ku-*control* ule uchimbaji wa madini kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo na kwa sababu kuna mengi ambayo yamesharekebishwa katika *schedule* hii, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kuwashukuru na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuleta huu Muswada hapa Bungeni, kwa maana ya kwamba Sheria hii ya Madini ambayo imerekebishwa ya mwaka 2010 iwe sahihi na kufuta ile ya zamani ya mwaka 1998. Lakini vile vile nichukue nafasi hii kushukuru sana wale waajiri wangu walionileta hapa, kwa maana ya wapiga kura wa Njombe Magharibi, kwa jinsi wanavyonipa msaada wa kuniunga mkono na kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kwa sababu nilikuwa na wasiwasi kwamba huenda hujaniona au umeona labda pengine kule Iringa au Njombe hakuna madini labda pengine nitakosa, kwa kweli nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye mada. Mengi wamezungumza Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wamejitahidi sana kuchangia mambo mazuri sana. Lakini na mimi kama mdau, kama Mbunge ambaye nawawakilisha wananchi wa nchi ya Tanzania, ni lazima nitoe mchango wangu kwa upande wa madini. Napata kigugumizi, napata shida sana ninapoona madini ya nchi hii kama yanachezewa hivi, kama hayana mwenyewe. Tanzania tuna utajiri mkubwa sana wa madini lakini hali ilivyo inavyoonekana inasikitisha.

Mheshimiwa Spika, hawa watu wanaoitwa wawekezaji wanakuja hapa, wanapokuja wanakuwa kama nusu Miungu hivi kiasi kwamba sisi tuna madini ni matajiri, lakini bado tunakuwa kama ombaomba hivi. Kuna kitu kinaitwa *royalty* – mrahaba, sasa *why mrahaba?* Wakati sisi ndio wenyе mali, tunamwomba mwekezaji atujengee zahanati, atujengee barabara au atufanyie nini! Wale wawekezaji inatakiwa tuwape sheria, isiwe kama ni hisani iwe ni lazima. Kwamba unataka madini yetu, unataka ujenge zahanati yenyе kiwango hiki, unataka ujenge barabara yenyе ubora huu, unataka ujenge mabwawa yenyе ubora huu. Lakini isionekane sisi tunakuwa wanyonge kwenye nchi yetu, inatutia aibu sana. Kwa hiyo, nilifikiri kwa sababu Mheshimiwa Waziri, ameingia kwa kasi nzuri, tunategemea atayafanya marekebisho hayo.

Mheshimiwa Spika, labda niseme kidogo kwa upande wa wachimbaji wadogo wadogo, hawa ni Watanzania wenzetu. Juzi nilikuwa na kipindi hapo *Star TV* na mdau wa Haki Madini; alizungumza kwa uchungu sana, nilimwelewa sana, kwamba wale wachimbaji wadogo wadogo bado wanaonewa sana, bado wananyanyaswa sana. Wanachimba madini lakini hali inakuwa mbovu kabisa, hali inakuwa sio nzuri; yaani anaishi kwa matumaini. Tunategemea wale wachimbaji wadogo wadogo, kwa kweli Serikali ni lazima iwawezeshe. Sio wawekezaji wawawezeshe, hapana! Unambana mwekezaji kupitia Serikali, ili hawa wachimbaji wadogo nao wawe wazuri. Yaani isionekane wale wawekezaji kila kitu wao ni wao tu.

Mheshimiwa Spika, kuna madini mengine wasiruhusiwe kabisa wawekezaji wakubwa, ieleweke kwamba haya madini ni kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Pia ikiwezekana kuna sehemu nyingine hawa wachimbaji wadogo wadogo wawe wanawauzia wawekezaji wakubwa. Isiwe kila kitu wanachimba, wanachimba, wanachimba, sisi wanatuachia mashimo makubwa. Watanzania inatakiwa tubadilike, tujiamini, hii ni nchi yetu, la sivyo tutaachiwa mashimo na mazingira watatuachia mbovu halafu wanakwenda nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, lakini nashukuru sheria imerekebishwa na sisi Wabunge tumeona kuna haja ya kuchangia kwa bidii, i inanipa moyo. Lakini wasiwasi wangu ni suala la utekelezaji, suala la usimamizi. Kwa sababu, tunaweza tukatunga sheria nzuri lakini kama haina msimamizi, haina mtekelezaji, *is nothing*. Kwa hiyo, nafikiria kwamba Watanzania tubadilike, wote hapa tunapitisha sheria lakini kusimamia tunawaachia wenzetu wachache, sisi Wabunge wote tunapitisha, ni lazima tuhakikishe huko tunakotoka tunawabana wawekezaji, tupige kelele kwa sababu tutakuwa tunawaumiza hawa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, sasa niliona ni nafuu nizungumze hili, sawa tunasema kwamba kuna suala la chombo kwamba tutengeneze chombo. Kwa mfano, kuna hili suala la mrahaba, naona nimeshalimaliza. Lakini sasa naomba nizungumzie kidogo kuhusu suala la mamlaka ya Waziri au Kamishna. Nimesoma hiki kitabu, kwa kweli mamlaka ya Waziri na huyu Kamishna ni makubwa sana. Pamoja na kwamba Waziri utanielewa vibaya, lakini kwa kweli huna sababu ya kung'ang'ania madaraka yawe makubwa, ni lazima tuyapunguze. Tuunde chombo ambacho chenyewe kitakuwa ni *regulatory*. Kwa mfano, tunatengeneza *Mining Authority* (Mamlaka ya Madini), ambayo yenyewe itahakikisha kwamba inahangaikia suala la masoko, teknolojia na utaalam mbalimbali na suala la elimu, kwa kuhakikisha inawafundisha wale wachimbaji wadogo wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hawa wawekezaji, wapewe muda mfupi na baadaye waondoke, sisi wenyewe tukalie uchumi. Isionekane sisi kila siku tunakuwa omboomba kwa hawa wawekezaji, *no!* Itatutia aibu sana. Tutengeneze chombo kama *EWURA, SUMATRA* na hata katika madini kwa sababu madini inaonekana kama ni kitu cha ovyo ovyo yaani hakina thamani. Sasa kuna wakati wa kusema haya madini yetu yawe na thamani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumza kwa uchungu sana, ukienda maeneo kama ya kule Geita, hali za watu pale sio nzuri. Kuna maeneo mbalimbali yanayotoa madini, watu wa sehemu zenyе madini hali zao sio nzuri sana. Sasa ile ni aibu sana, tena Mheshimiwa Ngeleja, unatoka Geita pale, nilitegemea watu wako wawe na hali nzuri zaidi. Kwa hiyo, ilikuwa ni vizuri hizi sheria tunazozitengeneza tusiwigandamize Watanzania wenzetu Wazalendo, wazawa.

Mheshimiwa Spika, kingine nilichotaka kuchangia ni kuhusu suala la *Mining Tribunal*. Hii ni Mahakama ambayo inashughulikia mambo ya madini, ni kitu muhimu sana, lakini suala la kusema kwamba Kamishna azungumzie migogoro ya yule aliyempa leseni, kwa sababu ile leseni alitoa Kamishna na watu wanamlalamikia huyu huyu Kamishna aliyetoa leseni ya madini, lakini huyu huyu ndio anatakiwa awe mwamuzi wa hii kesi! Pale kwa kweli haki haipo. Yaani ni wazi wale wananchi wa kawaida, hawa wachimbaji wadogo wadogo watashindwa hii kesi. Huyu bwana anatakiwa awe kama shahidi tu.

Mheshimiwa Spika, kuwe na chombo cha kisheria kiundwe, kuwe na Majaji au Mahakimu, Wanasheria, Mawakili, yule mtu anaitwa anakuwa kama shahidi –

mlalamikiwa, kwamba bwana ni kwanini hii leseni ilikuwa hivi, kwanini imekuwa hivi? Au kama sio mlalamikiwa lakini awe kama shahidi, isionekane yeye ndio anakaa katika kitu cha enzi, ndio asemr wewe umekosa, wewe hujakosa. Wakati mwininge utakuta Makamishna wale pengine sio Wanasheria, wenzangu wamezungumza hapa. Kwa hiyo, naona hapa kwa kweli ni lazima yafanyike marekebisho, kuwe kuna *Mining Tribunal*.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna kitu kingine kuhusu suala la *ku-add value* ya madini yetu. Miaka ya nyuma nilikuwa nasikia kuna ndege zinachukua mchanga zinapeleka Japan kwa ajili *ku-process*. Sasa ule mchanga unapochukuliwa una dhahabu, una kila kitu, matokeo yake ni kwamba tunapata hasara kubwa sana. Sasa hii sheria naona imesharekebishwa na kwamba kuna vipengele mbalimbali tutakuwa tunafuatilia. Kwa hiyo, ni vizuri tuwe na viwanda vyetu hapa hapa, tuwe tuna mitambo, kama ni mchanga, tuutengenezee hapa hapa kusudi isionekane wenzetu wanasesma ni mchanga tu kumbe kuna mali kubwa inatolewa pale halafu ule mchanga unaacha shimo. Sasa yale mashimo yale ni nafuu baadaye yawe endelevu kwamba labda tutengeneze mabwawa ya samaki au kitu kingine. Kwa sasa tunaona mwekezaji anaondoka anatuachia mashimo, Serikali inaanza kuhangaika kuyafukia fukia. Kwa hiyo, madhara yanakuwa ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nafikiria kwamba na madini yetu tunayoyachenjua, kwa maana ya kwamba madini tumeshayapata, sawa, isipokuwa tuhakikishe yale madini tunawaajiri watu wa kwetu, tunawapa elimu na ikiwezekana hiki chuo chetu cha madini kiendelezwe ili tupate wataalam wetu, nimesikia hapa Chuo Kikuu Cha Dodoma kuna taaluma ya madini au pale Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam nilikuwa pale, kuna elimu ya madini pale. Kwa hiyo, wale wataalam wetu tuwatumie vizuri. Unaweza ukaona kijana wetu anasoma lakini anakosa kazi, anashindwa kupata kazi kwa sababu alisoma mambo ya jiolojia. Sasa imefika wakati hawa wataalam wanaosoma tuwaingize kwenye hizi taaluma, kusudi haya madini tunapoyachimba na tunapoya-*process* *tu-add value*.

Mheshimiwa Spika, ni sawa sawa na upande wa wakulima, tuchukulie mfano, unataka kusafirisha mahindi kama mahindi, badala ya kuhakikisha unasafirisha unga au kitu kingine kiasi kwamba unakuwa *ume-add value*, au mbao, unasafirisha magogo badala ya kuzalisha mbao ambayo bei itakuwa kubwa. Kwa hiyo na madini haya iwe ni hivyo hivyo, tuhakikishe kwamba haya madini angalau tunayaongezea thamani, tunaya-*process* hata tunapouza yanakuwa na soko kubwa.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye kipengele kingine. Kipengele cha 108, ukurasa wa 70, kinahusu mambo ya *radio-activity*. Yaani madini yanayotoa mionzi. Mwenzenu nilikuwa na kasafari kidogo, nilikuwa kule Korea Kusini, kule Seoul. Kule kuna soko kubwa la madini ya *Uranium*. Bahati nzuri niliingia kwenye lile Bunge lao kwa nia ya kuwawakilisha, kwa kweli kuna soko kubwa la *Uranium*. Nchi ile imeendelea sana, lakini miaka kama 30 nyuma walikuwa kama Tanzania tu, lakini sasa hivi ni watu wameendelea sana, kilichowaendeleza sehemu kubwa ni madini. Kwa hiyo, hii *Uranium* hawachimbi wanaagiza, lakini ile *uranium* inasadia kutoa nishati ya umeme. Umeme wao kule haukatikikatiki, sasa huku tuna *uranium* lakini matokeo yake ile *uranium* inakuwa

kama ni *useless*, tunahangaika na umeme wa maji, tunahangaika na umeme wa magogo, wakati tungetumia *uranium* tungekuwa mbali sana.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nilimweleza Mheshimiwa Ngeleja kwamba bwana, kule bwana kuna soko, kule kuna teknolojia ya juu sana ya *uranium*. Namshukuru kwamba alituma Mtaalam, sielewi na sijafuatilia sana yule mtaalam amefikia wapi, lakini kwa kweli haya madini tunayo mengi nasikia hata huko Ruvuma yapo na sehemu nyingine madini ya *uranium* tunayo. Kwa hiyo, haya tukiyatumia vizuri na tukaita wawekezaji lakini wawekezaji hawa tuwape sheria ya kutosha kwa sababu wana mitaji na teknolojia, tungeweza kufika mahali pazuri sana.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Nashukuru sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu, Muswada ambao ni muhimu sana katika nchi yetu. Lakini ni Muswada muhimu kwa sababu pia unakuja katika kipindi ambacho Watanzania wengi wanahisi kama ni majeruhi, watu walioumia na sekta hii kwa sababu hawaoni na hajajidhihirisha faida wanayopata kutoka na maliasili waliyojaliwa katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, lakini nichukue nafasi ya pekee kabisa ya kuwapongeza na kuwashukuru vijana wenzetu Mheshimiwa Ngeleja, Waziri na Mheshimiwa Malima, Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuongoza gurudumu ya mageuzi haya ya sekta hii ambayo kwa muda kumekuwepo na manung'uniko makubwa. Vijana hawa ni ushahidi tosha kwamba wazee wajue kwamba na sisi tukipewa kazi tunaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa wazee utabakia pale pale siku zote na wao ni muhimu kwa nafasi tunahitaji kuchota ujuzi na uzoefu mkubwa walionao na Bunge linapaswa kuwa na watu wa namna hiyo, vijana na wazee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Kamishna wa Madini Dr. Kafumu na Katibu Mkuu Jailo kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini niwape changamoto kwamba wanatakiwa wawe Wazalendo na kutangaza jina na kuondoa manung'uniko ya wananchi ambayo yako mikononi mwao. Ofisi yao tunaifahamu sana, tunajua wanachokifanya na tunajua ambao hawapendi mabadiliko wapo. Kwa hiyo, waijiangalie sana tunajua, kuna

haja ya kuangalia kwa makini na Serikali iangalie ofisi hii kwamba tunapohitaji mabadiliko kama haya basi hatuhitaji watu wenye kigugumizi cha kuleta mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na maneno maneno kwamba Muswada huu umekuja katika kipindi ambacho unalazamishwa kuja kwa haraka, uharaka hakuna hapa ni utaratibu tu, kuleta Muswada kwa *certificate of agency* ni utaratibu tu wa kupeleka mambo kwa umuhimu wake na kwa wakati ambapo yanahitajika. Kwa hiyo, wenzetu waliokuwa wanajaribu kuwaambia umma kwamba Muswada huu unaletwa katika hali ya haraka pengine una malengo fulani. Kwa hiyo, sisi kama watu waliotuchagua na ni watu makini na pengine tumeshiriki katika Muswada huu kwa kina sana, kwa undani sana na kwa hakika katika wiki hii hakuna ambaye ana uchungu na sekta hii ambaye alilala na kupumzika. Mchana wote tulikuwa tunashinda masaa yote, tunatoka saa tano usiku hadi leo tumevida na kitu kimekuja hapa katika hali hii. Watanzania waamini kwamba sisi wananchi waliotuchagua tunafanya kazi kwa niaba yao kwa maslahi ya Taifa na wananchi wote wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie namna ambavyo pengine matarajio ya wengi wanadhani katika Muswada huu tunaweza tuka-*fill all the gaps* yaani ukatengeneza sheria ambayo inamaliza, inaziba kila kitu *water tight*, hakuna sheria ya namna hiyo duniani. Sheria inatungwa na ndiyo maana kunaachwa habari ya *regulation* na ndiyo maana kunaachwa kuna kuwepo na *distraction* na ndiyo maana mtu anapewa madaraka huwezi ukampa mtu madaraka ukamfunga kukawa *no distraction that is not a good law*, hiyo itakuwa ni sheria mbaya tu. Kwa hiyo, tuamini kabisa kwamba sheria na kwa tabia ya sheria inayotungwa sheria *must be general* lazima sheria iwe *general* isiwe sheria inayolenga kurekebisha kitu fulani *specific otherwise* inaweza ikakumbwa na dosari kubwa katika utungaji wa sheria ambayo inakuwa inasema *the law can not apply retrospective* sheria haiwezi ika-*apply* kwa kurudi nyuma. Kwa hiyo, hapa ni kwamba yaliyopita sindwele tugange yajayo, tufikirie tunatoka hapa tunakwenda wapi na sekta yetu hii ya madini ili iweze kuongeza pato la Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hakika pamoja na uzuri wa sheria, sheria hii ina sehemu kubwa tatu, ina sehemu kubwa ambayo ni nzuri sana ambayo imeleta mabadiliko na Watanzania sasa watajisikia kwamba wao ni sehemu ya sekta hii na kwamba hawajawekwa pembeni. Lakini sehemu ya pili ni ile ambayo ina mapungufu, sasa haya mapungufu ni mchakato endelevu hatuwezi leo tukamaliza kila kitu sheria hii inapita, lakini tunajua kabisa kwamba bado tunahitaji marekebisho muhimu. Kwa mfano, mamlaka ya madini ni lazima iundwe, Mheshimiwa Waziri, anapomaliza atupe *a really commitment of the government*, Serikali inasemaje juu ya suala la kuunda mamlaka ya madini, atuambie kabisa na ili iwe *recorded* vizuri kwa wazi na sio kwa ujanja ili baadaye kuwepo na muda mrefu wa kuunda mamlaka hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba kuunda mamlaka ni gharama, lakini mamlaka ndiyo itakayopunguza na kufanya kazi halisi na kumshauri vizuri Mheshimiwa

Waziri au Waziri atakayekuja wakati wowote ule ili nchi hii iweze kunufaika na sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, suala la nguvu kubwa na kazi nyingi anazopewa Kamishna na lenyewe ni upungufu mwingine ambao kwa hakika ni lazima pia uangaliwe kwa sababu kwa kweli kumweka Kamishna wa Madini mtaalam ana *Ph.D* ya mambo hayo, anafanya kazi ya usuluhishi si kutomtendea haki lakini, pia kumpa kazi ambayo sio ya kwake! Haya ni mapungufu ambayo tumeyaona na tunaya-*register* hapa na ninyi muone namna ambayo mtayapeleka mbele lakini tunaamini kabisa sheria hii ni muhimu kwa upande ule wa uzuri wake ambao sasa naomba nichukue nafasi ya kuuelezea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upande mzuri wa sheria hii, ni kwamba umetambua umuhimu na nafasi ya wachimbaji wadogo katika nchi yetu. Wamekuwa na manung'unico na wao ndiyo wanaishi katika sekta hiyo. Lakini manung'unico yao nataka niwahakikishie wachimbaji wadogo wa nchi hii yamekwisha kutokana na sheria hii. Kwa maana hiyo kwa mujibu wa sheria hii, madini yote ya vito, *gemstone mines* yatachimbwa na wachimbaji wadogo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kinatakiwa kitu gani kingine zaidi ya hicho, hakuna mgeni atakayechimba na pia mnaruhusiwa ninyi kwenda kuuza *share* na kushirikiana na wageni, mtajua ninyi mtakavyofanya lakini pamoja na haki hii kipengele hiki muhimu na eneo kubwa la sheria hii kusema juu ya hawa wachimbaji wadogo au kupewa nafasi kubwa na sheria hii bado nina mashaka na maandalizi yao na wao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kibakwe Wilaya ya Mpwapwa, kumegundulika madini muhimu sana yenye thamani kuliko hata *Tanzanite*, nashangaa tunazungumzia *Tanzanite* lakini iko Safaya ambayo kwa hakika ina thamani kubwa hata katika soko la madini la dunia kuliko hata hiyo *Tanzanite* wala madini mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini nimejifunza na kuwajua wachimbaji wadogo ni nini? Wachimbaji wadogo ni kundi la watu wanaovamia kama nzige, sasa tafsiri inayotolewa katika sheria hii ya wachimbaji wadogo imezungumzia kiwango cha fedha wanachotakiwa kuwanacho kama mitaji?

Mheshimiwa Spika, ni lini mtu anakuwa mchimbaji mdogo bado ni tatizo, pale kinachotokea kwenye machimbo ya Winza ya Safaya, yaliyopo katika Jimbo la Kibakwe Wilaya ya Mpwapwa, kwa hakika ni mgogoro mtupu na *industry* haiwezi ikaendelea kama wachimbaji wadogo wataachwa bila kuwa *organized*. Tatizo kubwa kwao ni kwamba kwanza wagumu wakukubaliana katika kushirikiana kivikundi jambo ambalo Wizara lazima mliangalie.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo hawa sasa watakuwa wanaauza kila kitu kwa hawa wageni kwa sababu tuna *provision* ambayo inawaruhusu kushirikiana na wageni. Badala ya kushirikiana nao kwa kupatana katika mikataba mizuri nina wasiwasi

kwamba bila kuwa *trained* hawa watauza kila kitu. Kwa hiyo, badala ya kazi iliyokuwa inafanywa na Serikali wao ndiyo watakuwa wanafanya kazi ya kuuza maeneo yote ya uchimbaji. Kwa hiyo, bila kuwezeshwa, bila kupewa nyenzo za kufanya kazi, bila kuwa na *access* kwenye kupata mitaji au mikopo basi wasiwasi wangu ni kwamba wachimbaji wadogo hawa ni tatizo kubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia wasiwasi mwingine ni namna gani wanachangia mapato kutoka kwa wachimbaji wadogo, maana hizi leseni za wachimbaji wakubwa ambazo zinaruhusu uwekezaji kutoka nje wao watapata kupitia mrahaba. Je, Wilaya ya Mpwapwa ambayo ina madini ya Winza na imevamiwa na wachimbaji wadogo na wengi pale ni wageni na wala sio Wagogo wala Wahehe wa Kibwake, wanapataje maslahi ya madini yanayochimbwa pale? Maana wote waliokuja pale ni wageni wa kutoka mikoa mingine? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa napata wasiwasi kwamba je, Halmashauri ita-*benefit* vipi, je una-*control* vipi yale mapato, naomba Mheshimiwa Waziri wakati wanapotengeneza *regulations* kwa sababu kama nilivyosema sheria haiwezi ikasema kila kitu, wakumbuke sana namna ya kuwaweka sawa hawa wachimbaji wadogo kwa kuwa-*control* kwa sheria hiyo ndogo. Lakini je, mazingira na wao wachimbaji wakubwa tunasema warudishe hali kama ilivyokuwa, je, wachimbaji wadogo wanafanyaje? Basi nadhani *regulations* ziseme kwa sababu sheria hii imekuwa iko *general* na ilikuwa na malengo yake, kwa hiyo hatuwezi kuipa kila aina ya dozi hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumzie jambo ambalo ndiyo msingi wa uchungu na wa sekta hii, kama Serikali yetu haitaamua kumiliki hasa madini makubwa *in strategic minerals*, hakika hatutasikia habari kwamba sekta ya madini na madini haya ni *resource*, *there are always limited, resource* hizi zinakwisha, madini yanakwisha, itafika siku yatakwisha, Serikali yetu isione aibu na wala sio kwamba itaingia kwenye shughuli ambayo inafanya Serikali yetu kwa madini makubwa makubwa kwa mfano, tuchukulie kwa mfano yale makaa ya mawe, gesi, chuma kwa kweli kwa hakika hatuwezi, lazima Serikali yetu iwe *state ownership*, ni kitu cha msingi sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, iwe ni *State ownership through* makampuni yetu, kwa mfano ya *STAMICO* na *NDC* ni muhimu sana. Mashirika haya ni makubwa na yakiwezeshwa yanaweza kufanya *exploration*, *STAMICO* wanafanya hata leo, hii wanaweza wakafanya utafiti na *problem* kubwa ni pale tunapouza haki yetu ya kujua kilicho chini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba hatuna uwezo lakini hivi kweli hatuwezi kuupata huo uwezo, huu uwezo lazima wawe wageni tu wa kuchunguza kwamba kuna nini chini? Sisi hatuwezi kujua, kweli tunakiri na kukubali kwamba hatuwezi, siamini, utafiti ufanyike hilo tunaweza. Tunaweza tukachunguza, tukajua kilichoko chini na tukapata *bargaining power or contract power* wakati wa ku-*bargain* kwa sababu tunajua kilichoko chini. Haiwezekani *feasibility study* ikafanywa na mgeni huyu anayekuja kuwekeza halafu mnakaa mezani mnakubaliana kwenye mkataba kwa kutumia vigezo na *feasibility study* ya kwake, wewe unaye *bargain* huna, *where do you get the power* maana yake wewe ni *weak part* katika kupatana. Mnapokaa kwenye *round table* wewe utakuwa *weaker* kwa sababu huna vielelezo, huelewi kuna nini ila mgeni ndiyo anayeelewa.

Mheshimiwa Spika, naamini tunaweza na habari ya kusema hatuwezi kufanya utafiti hebu neno hilo liishe, kama hatuwezi leo tutaweza kesho. Mwalimu hakuruhusu uchimbaji wa madini, hivi fikirieni Awamu ya Kwanza ya nchi kama ingeruhusiwa kuchimba madini tungekuwa tunazungumza haya tunayozungumza hapa, tusingekuwa na habari yote hapa, kila kitu kingekuwa kimeshakwisha. Lakini alizuia kwa sababu aliona bado hatuna uwezo wa kuweza kufanya *industry* hii, na sisi kama kile ambacho hatuwezi tuiseme tu, uwekezaji uwekezaji kama hatuwezi tuseme hatuwezi tunasimamisha kwani yanakwisha, hivi maisha ya nchi hii ni sisi tulipo tu humu, ni Watanzania wa leo tu, si watu wanaendelea kuzaliwa, watakuja wengine watakuja na teknolojia watagundua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Simbachawene, imebakia nafasi ya wachangiaji nadhani wawili tu kwa jioni hii, kwa hiyo nitamwita Mheshimiwa Nyalandu, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucas Selelii.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba kusema tuna imani na uongozi wako. Pia nichukue nafasi hii ya kipekee kumshukuru sana Mheshimiwa William Ngeleja, kumpongeza akishirikiana na Mheshimiwa Adam Malima kwa uhodari wao kwa kazi nzuri waliyoifanya kutafsiri kwa haraka maagizo na utashi wa Mheshimiwa Rais kwamba Sheria ya Madini ije kwa *agency* kwa *certificate of agency*, ifanye haraka kabla ya uchaguzi wetu mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi kuwapongeza na niliwaambia nje, ndugu David Jailo pamoja na Dr. Peter Kafumu, kazi waliyoifanya katika maandalizi ya sheria hii inakuwa mfano wa kuigwa kwa watendaji wengine wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza kwa dhati Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo, kazi mliyofanya kwa niaba yetu ni nzuri inatukuka na inaheshimika, alitajwa na naomba nimitaje kipekee Mheshimiwa Andrew Chenge, mchango wake wa dhati umekuwa mzuri na naomba nitaje hapa kwamba tunakushukuru kwa niaba ya Watanzania wote ambao sasa wataipata sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naongea kwa niaba ya mikoa yote yenye madini, mikoa yote isiyo na madini wachimbaji wanaonisikiliza wa pale Mpambaa, Singida, walioko katika Tarafa ya Mtinko, wale wa Ilongero Mgori maeneo ya Londoni pale Manyoni na sehemu zote katika nchi hii. Sheria hii ambayo Serikali inaileta ni sheria nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu na mengi yameelezwa, Tanzania kuwa nchi ya tatu kwa *deposit* ya madini ya dhahabu ukiacha Afrika ya Kusini na Ghana na habari ambazo tunazipata ni kwamba Tanzania hivi karibuni itaizidi Ghana kutokana na uvumbuzi mbalimbali unaoendelea. Nchi hii ndiyo sehemu pekee yenyе *Tanzanite*, nchi hii ina utajiri mkubwa, nchi hii ni nchi chache katika Afrika ambako watu wangependa kwenda, wakae wajisikie vizuri, hivi karibuni wale waliokuwa wakimbizi katika nchi yetu kutoka nchi ya jirani. Umoja wa Kimataifa umetupongeza kwa kuwapa uraia nchi hii inapendwa na wageni, inapendwa na wenyeji, ni nchi ya heshima na tunaendelea kumwomba Mungu awabariki na Mungu awabariki wenyeji wa nchi hii katika kuendelea kuifanya nchi yetu iwe ya heshima zaidi.

Mheshimiwa Spika, sheria hii kwa maneno mafupi na kwa kuitazama inatafsiri kwa uhakika kabisa jinsi ambavyo nchi yetu itauchukua utajiri tulionao wa ardhini uwe utajiri wa matumizi *wealth of the nation* nchi yetu ifike mahali kama watoto wanavyoimba tunapokwenda kwenye kampeni, wanaimba CCM bomba, mgombea huyu ni bomba sana, naomba watoto wale katika shule zetu waendele kuimba Tanzania ni nchi bomba. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nchi hii ni nchi nzuri, ni nchi ambayo tunaitazama kwa matumaini makubwa na nashukuru sana kwa mara ya kwanza sheria ya madini inakita kwa walichosema wenzangu uhimili wa Serikali katika kushiriki sehemu ya hisa kwa ajili ya wananchi wa sasa na vizazi vijavyo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nilitembelea Botswana ni nchi ambayo inaendeshwa na wingi wa ng'ombe, wakulima wana ng'ombe wengi sana. Jambo la pili wana almasi *diamond*, halafu la tatu na la mwisho wana Hifadhi za Taifa. Mpango wao wa kufanya almasi ya nchi hiyo iwe inakuwa *processed* katika Gaboloni. Jambo la kwanza wameiongezea heshima nchi hiyo, Serikali imeshika hisa nyingi sana kwa niaba ya wananchi na watu chini ya milioni tatu ina utajiri mkubwa sana katika Afrika ukiacha Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, heshima ya Botswana imepanda, nchi nyingine ni Sierra Leon, wenzetu hawa wana almasi, sinema ya hivi karibuni ikachezwa wanaita *blood diamond*, maana yake wenzetu waliamua kuzipiga kweli kweli kwa sababu ya dhahabu walizonazo. Nchi yetu ina heshima ya amani, ni matumaini yangu kwamba rasilimali hizi na kwa sheria hii kukubali kushika sehemu ya hisa kwa niaba ya wananchi italeta heshima sana. Napongeza sana nia hiyo ya Serikali na juhudhi hiyo za Serikali kuweza kuiweka hii katika sheria. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba kwa sababu wimbo mkubwa ambao unaimbwaa tangu nikiwa mdogo, nchi yetu ni nchi maskini, alisema Mzee Mzindakaya, hakuna umaskini wowote katika Tanzania katika kijiji kimoja ambacho wana mifugo 2000 karibu kwa familia zaidi ya mia moja na wao wanaamini ni maskini? Watu ambao wamekaa juu ya dhahabu, juu ya almasi, juu ya madini mbalimbali, wameendelea kuamini kwamba wao ni maskini, nafikiri sheria hii inafikisha nchi mahali ambapo tunaamini kwamba umaskini wa Tanzania ulikuwa ni umaskini wa kutokujua ni nini tulichonacho. Naomba nchi hii chini ya uongozi madhubuti wa Rais wetu na chini ya

uongozini madhubuti wa Waziri wa Wizara hii kwa sheria hii tukasimame kidete tuifaidi na tuyafaidi madini ya aina mbalimbali yaliyopo katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itakapokuwa ina-*negotiate* na wageni na wawekezaji mbalimbali juu ya *free carried interest*, ihakikishe kwamba ile *negotiation* inakuwa kwenye *higher end*, asilimia kubwa kwa kadri itakavyowezekana kwa kadri ya matakwa ya uwekezaji na masharti yatakayokuwepo wakati huo.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme suala zima ambalo limeongelewa na wenzangu la ongezeko la thamani, suala la *processing, smelting* na *refining* litakuwa ni suala muhimu sana katika sheria hii na naiunga sana mkono Serikali kuileta sasa hivi. Wamesema wengi kuhusu ukuaji wa ajira, ongezeko la thamani kwa madini na vitu mbalimbali vitakavyozalishwa hapa vitaifanya Tanzania ijiwekee heshima na kuwa *produce of Tanzania* kwa sababu hata nguo ikitengenezwa China wataandika pale pembeni *made in China*.

Mheshimiwa Spika, dhahabu ya Tanzania itakapoanza kuuzwa popote tunataka ijulikane kwanza hii ni dhahabu ya Tanzania, tunataka *tanzanite* ya Serikali ijulikane kwamba hii ni *tanzanite* ambayo *origin* yake ni Tanzania. Haiwezekani ikatokea bila kuwa na *processing*, bila kuwa na *smelting* na bila kuwa na *refining*. Katika *refining* Serikali ni lazima kwa kutumia vyombo vyake wamesema wenzangu iwe na hisa. Udanganyifu mwangi sana wa makampuni ya madini ni pale ambapo tunashindwa kujua thamani ya mali tuliyonayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, *interest* hii ni lazima ilindwe kwa vizazi vyaa sasa hivi na vizazi vingi sana vijavyo. Napendekeza kama ilivyo katika *Istanbul* kule Uturuki kuwe na *establishment* ya *Tanzania gold exchange* hii inatokana tu na *refining* na bila kuwa na *gold exchange* vitu vingi sana vitapotea. Naomba sana Serikali ifikirie uwezekano wa kuweka *Tanzania Gold Exchange*.

Mheshimiwa Spika, katika miaka 25 ijayo inakisiwa Watanzania watakuwa wamefika milioni 75 na kuendelea. Tatizo tulilonalo kiuchumi Tanzania sasa hivi ni ukosefu wa umeme wa kutosha. *Of course* sisi tuna *hydropower resources* za kutosha na *capabilities*. Lakini kwa kuwa katika Mkoa wa Singida, Songea na Mikoa mingi sana *potential* ya *Uranium* ni kubwa sana, madini haya ndiyo madini pekee duniani ambayo yanaweza yakatusaidia kwenye teknolojia ya *nuclear power*, Tanzania ikiweza kutengeneza *nuclear power station* moja inatosha kutoa nguvu ya nishati ya umeme kwa zaidi ya watu 50,000, usambazaji wake unakuwa mgumu kama unakwenda kila kijiji. Lakini inategemewa miaka 25 ijayo zaidi ya nusu ya Watanzania watakuwa katika maeneo makubwa ya miji.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Kenya wameanza ku-*negotiate* na *UN atomic agency*. Naomba Tanzania tusilale kwa uwezekano wa kupata vibali, tuenze kufikiria na kuelimisha watu kuwa tayari na *nuclear atomic technology* katika nchi yetu katika miaka

ijayo. Hivi karibuni katika Tanzania matumizi ya umeme katika Tanzania ni KH 85, katika nchi nyingi za *sub Sahara Africa* nchi zote tunazopambana hapa wastani wao wa matumizi kwa mwaka ya umeme ni 432 na katika dunia wastani ni 2176.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine matumizi yetu ya nguvu ya umeme ni madogo sana kwa sababu umeme wetu ni wa gharama kubwa, unapatikana kidogo na unatumika maeneo machache. Wananchi wengi wa Tanzania katika Tanzania kwa wastani leo na hizi ni kumbukumbu za mwaka 2007, asilimia 95.8 ya Watanzania wote wanapika kwa kutumia kuni na kwa kutumia mkaa. Katika Mji wa Dar es Salaam asilimia 71 leo wanapika kwa kutumia kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, hizi ni takwimu za Serikali yenye. Ni lazima tufanye kila tunaloweza kuhakikisha kwamba vijana wanaandalisha kwa sababu ni suala la elimu, shule zetu, vyuo vikuu vyetu vianze kuwa na vitengo vya *nuclear technology*, watu waanze kufundishwa, tuanze kufanya maandalizi tutakapokuwa tayari *uranium* tuliyonayo iweze kufanya kazi ya kuipeleka nchi yetu katika hatua nyingine. Kuna suala la *balance of power* katika Afrika Mashariki, Uganda wamegundua mafuta mengi sana na wengi wameanza kutembea kifua wazi.

Mheshimiwa Spika, lakini hakuna aliye na madini mengi kama alivyosema Mzee Mzindakaya na mtu mwagine kama Tanzania na *The DRC* ni lazima Watanzania popote waliko dunia wafahamu nchi yao ni nchi nzuri, ni nchi iliyo na *endowment*, ni nchi ambayo wanapaswa huko waliko watamani na wafikirie kurudi kwao huku Tanzania. Ni lazima tuandae matumizi ya rasilimali hizi kwa ajili ya *ku-balance power*. Rwanda wanatumia madini mengi sana ambayo hatujui yametoka wapi. Lakini unaweza ukahisi na *waka-export*. *Tanzanite* ya Tanzania inakuwa *exported* through Nairobi na South Africa. Tungependa *Tanzanite* na madini mengine yote kama nilivyosema yaonyeshe katika *certificate* zake *origin* yake ni Tanzania. Yapate kuwa *registered*, kodi zote zilipwe hapa Tanzania na tuhakikishe kwamba nchi yetu inasonga mbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pasipo kutumia maneno mengi zaidi wengi wameyasema, wachimbaji wadogo wadogo popote walipo na hasa wale wa Jimboni kwangu natumaini mnianisikia, Serikali iko pamoja na ninyi, sheria ndiyo hii Chama cha Mapinduzi, wameileta kwa ajili ya uchaguzi kuhakikisha kwamba chama hiki kinachowajali wananchi daima dumu kinaendelea kushinda. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyalandu kwa kauli ya Uzalendo, Mungu aibariki Tanzania. Tunaendelea, nadhani ni zamu sasa ya Mheshimiwa Lucas Selelii na nadhani kwa muda ulivyo itakuwa ni ndiyo msemaji wa mwisho kwa sababu si rahisi kwa Mheshimiwa Selelii kutumia dakika tano au kumi.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba unisamehe na Wabunge wenzangu nina *flu* mbaya. Lakini ni makamasi ya kawaida siyo *flu* ya mafua ya ng'ombe wala ya kuku.

## **MBUNGE FULANI:** Tutakusikia.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu katika suala hili muhimu la madini. Lakini kabla ya kutoa mawazo napenda kutoa salamu kwa wachimbaji wadogo wadogo wote Tanzania na hasa walioko katika Jimbo la Nzega kule Isungangwanda, Mbogwe na Lusu na katika Jimbo la jirani la Mheshimiwa Teddy Kassela–Bantu, wale wa Itanana na Igusulu; Jimbo la jirani yangu wa Igunga wale wa Ikompatulu kwa teknolojia hii wanania na wanansikia nataka niwafikishie salamu kwamba Serikali yenu ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu na imesikia kilio chenu cha muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya salama hizo nitoe pongezi kwa Serikali, kwanza kwa kupokea na kusikiliza maoni na ushauri mbalimbali wa Wabunge. Lakini pongezi zaidi kwa Kamati ya Nishati na Madini inayoongozwa na Mheshimiwa William Shellukindo. (*Makofi*)

Hata hivyo nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sitataja Kamati ya Mheshimiwa Jaji Bomani nao walifanya kazi nzuri sana ambayo imetuongoza kufikia hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kusikia kilio na kuwakumbuka wachimbaji wadogo, nina ushauri ufuatao, kwanza kuwakumbusha kwamba, madini ya vito sasa yachimbwe na wananchi wadogo wadogo wenyewe. Ni jambo zuri sana kwa kweli Serikali inahitaji kupongezwa kwa uamuzi huo, hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina ushauri mdogo na hasa juu ya wachimbaji wadogo wadogo. Namwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake, ni vijana wachapakazi sina wasiwasi nao. Lakini vile vile hata watumishi wa Serikali Kamishna, Katibu Mkuu na wengine nao ni wafanyakazi wazuri sana. Baada ya hii ningeomba sasa tufanye namna yoyote ya makusudi kuhakikisha tunawawezesha wachimbaji wetu wadogo wadogo, kwa mitaji, kwa kupata zana, lakini cha msingi na cha muhimu ni kuwawezesha kupata utalaam. Wachimbaji hawa wadogo wadogo tukiwawezesha wakawa katika *stage* ya wachimbaji wa kati baadaye tutakuwa na Watanzania amba ni wachimbaji wakubwa amba wanaweza kushindana na wachimbaji wanaokuja kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini uamuzi huu wa makusudi lazima urasimiwe na Serikali yenye kwa makubaliano ya makusudi kabisa. Kwanza kuondoa urasimu amba unapatikana pale Wizarani katika kupata leseni hasa kwa wachimbaji wadogo wadogo. Lakini kubwa ni kuweka mfumo rasmi ukajulikana kabisa mfumo rasmi wa kuuza na kununua madini. Kwa sasa wachimbaji hawa wadogo wanauzwa kiholela, wanauzwa kwa kificho hebu ifikie mahali ambapo dhahabu yetu, madini yetu ya almasi pale Mwadui na jirani yake yakajulikana kwamba yanauzwa kwa nani. Tukiweka maduka rasmi ya kuuza kama ilivyokuwa wakati ule Benki Kuu ilipoamua ikauza kuitia NBC na dhahabu ikanunuliwa, tukiweka kama tunalivyoweka maduka ya kuuza dola itasaidia sana kujua bei ya dhahabu, bei ya almasi ambayo inapatikana kuitia *internet* kwa dunia nzima hata uki-tune leo.

Mheshimiwa Spika, iweje uweze kujua bei ya dola, iweje uweze kuanzisha *exchange* ya kuza dola, iweje unaweza kufanya hivyo, inatakiwa Wizara hii iweke bei dira, kama vile unavyoweka bei kwenye mafuta ili mchimbaji au muuzaji mdogo wa madini aweze kujua hata kama anauza kwa Mhindi, hata kama anauza kwa Mwarabu asipunjwe. Sasa hivi anauza kwa hiari kwa mnunuzi ambaye bei haijui sawa sawa. Lakini tukiweka bei dira, tukatangaza kwenye gazeti kwamba bei ya dhahabu duniani leo ni hii, itawasaidia wachimbaji wetu wadogo kupata manufaa na kupata bei nzuri sana ambayo itawasaidia.

Mheshimiwa Spika, vile vile napendekeza uwekwe mfuko maalum ambao utaimarisha *STAMICO* ambayo *STAMICO* itakuwa ni kichocheo cha kuwapa wachimbaji wetu wadogo mitaji ya kuwapa ujuzi ili waweze kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushauri mwengine, nafurahi kwamba Serikali imesikia maombi ya wadau na hasa ushauri wa Jaji Bomani katika kupandisha mrabaha kutoka asilimia tatu na kufikia asilimia tano kwa almasi na asilimia nne kwa dhahabu, siyo haba ingawa nilikuwa nategemea kwa sababu wote tulikuwa asilimia tatu dhahabu na almasi ingeweza kufikia asilimia tano. Lakini ushauri wangu ni kwamba mrabaha huo wa dhahabu ambao unatolewa na almasi ambao unatolewa kwa Serikali na sasa hivi imesemwa katika sheria ya sasa ilipe kwa *gross value*. Nadhani mtindo huu bado ni mwanya wa kufanya wachimbaji wakubwa katika kuipotosha Serikali hasa kuficha ukweli wa mapato.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hivyo tu naomba kwa makusudi mazima baada ya kupata huo mrabaha wa asilimia tano au mrahaba wa asilimia nne sehemu ya asilimia hiyo iende moja kwa moja kwenye Halmashauri kama kilio cha Wabunge pamoja na wadau ambacho kimekuwepo kwa muda mrefu sana. Napendekeza asilimia 25 ziende kwenye Halmashauri husika ili maeneo ambayo yanatoka madini angalau yawewe kufanana na madini. Ukiangalia maeneo kama ya Nzega, Kahama, Shinyanga, ukiingia kule kwenye mgodi ni tofauti sana na miji ambayo inamilikiwa na wenyewe. Angalau basi hizo asilimia 25 zingeweza kufanya miradi ya maendeleo katika maeneo husika, miradi ya kijamii. Ukienda Mwadui, ukienda mgodi wetu wa Nzega, ukienda Kahama wana migodi miwili, ukienda Geita hapafanani na hadhi na fedha ambayo inatokana na dhahabu ambayo wenzetu wageni wanaipata. Kumbe kama tungewekeza asilimia 25 kwenye Halmashauri ingeweza kufananisha sehemu hiyo ikapendezesha na ikawa nzuri kama ambavyo ipo katika migodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini hebu tuweke makusudi kwamba kwa sababu Halmashauri hizo zimekuwa na bahati ya kupata dhahabu, Serikali itumie kutoa sehemu ya hisa katika mgodi huo iwe inamilikiwa na Halmashauri husika. Itasaidia sana kuwa na mkono wa Serikali katika migodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwengine nataka nitoe ushauri katika kile kifungu cha 10, sehemu ya 2, hasa katika ile *government negotiation team*. Katika ile *government negotiation team* napata mashaka sana kwa sababu hapo ndipo tunapolipa.

Tumewawezeshaje watalaan wetu, kuwapa ujuzi wa kutosha kupambana katika *ku-bargain*? Hawa wachimbaji wakubwa wana watalaan, wana wanasheria waliobobe. Watalaan wetu hawa wanahitajika wawezeshwe, wapewe *bargain power* ili uelewa wao, uwezo wao wa *ku-negotiate* uwe kwa manufaa ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda eneo hili ambalo liko katika kifungu cha 10(2), Waziri aweze kuliangalia kwa macho yote mawili hasa ukizingatia unapounganisha kile kifungu cha 25 na kifungu cha 100 ambacho kinaweka usiri katika makampuni na uwazi unakuwa ni mdogo sana hasa katika kuuza mazao ya madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kushauri ni umiliki wa madini makubwa ambayo ni msingi mkubwa wa viwanda ambavyo vinaweza kuleta maendeleo. Madini makubwa kama vile chuma, mkaa wa mawe, magadi, gesi, hapa tuwe na uamuzi wa moja kwa moja kwamba mkono wa Serikali uwepo bila kusita. Hapa ndiyo mahali ambapo tunaweza kuinuka. Tunajivuna sana na kujidai nchi yetu ya amani, nchi yetu ni tulivu, lakini hatujathubutu kuwa na maamuzi ya kutumia rasilimali zetu. Tumesharuhusu migodi, sisi tunaotoka kwenye maeneo ya migodi tunaelewa, tumesharuhusu mgodi wa dhahabu, mgodi wa almasi na kadhalika ikamilikiwa na wageni kwa asilimia 100. Lakini tukishazubaa tena tukaruhusu hata haya madini makubwa ambayo yanaweza kuanzisha viwanda vikubwa napo tunajiongezea umaskini.

Mheshimiwa Spika, utajiri hapa ndipo upo. Kwa hiyo, hatua za makusudi ziweze kufanyika, uamuzi wa makusudi uweze kufanyika ili utajiri huu tulionao mkubwa wa chuma, mkaa wa mawe na magadi uweze kumilikiwa na Serikali na ningependa kushauri kwamba umiliki huo uwe chini ya *NDC* au uwe chini ya *STAMICO* ambao wanaweza kutusaidia sana. Kwa sababu *STAMICO* tayari ni shirika ambalo limekuwepo muda mrefu sana toka wakati wa Uhuru na toka wakati wa Uhuru lilikuwa linaangalia madini yote hayo na limeonyesha uzalendo wa hali ya juu sana. Bahati mbaya bado hatujawawezesha kiasi cha kutosha kwa teknolojia lakini vile vile hatujawawezesha kiasi cha kutosha kwa fedha za kuijendesha. Kwa hiyo, nashauri umiliki wa madini makubwa uwe upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia fungu la 16 katika sheria. Katika fungu la 16, napata mashaka sana, mamlaka ambayo tunampa Mheshimiwa Waziri kwamba akishakaa na ile bodi akishafanya *consultation* na bodi ile anaweza aka-*declare*, anaweza akaamua eneo lolote likawa eneo la madini. Tunahubiri hapa dhana ya utawala bora, tunahubiri hapa dhana ya ushirikishwaji, kule kwenye maeneo ya Wilaya zipo Serikali ambazo tungezishirikisha zingewenza kutushauri na kutushauri vizuri sana. Maeneo haya ya sheria ya namna hii ni sheria ya ukandamizaji na ni sheria ya ubabe. Napendekeza kwa uzuri wa sheria hii ambayo sisi wote tunaikubali na hata ambao wanatoa mapungufu ni katika maeneo kadha wa kadha. Kifungu kama hiki cha 16 ambacho kinampa Waziri uwezo mkubwa kabisa wa kuondoa eneo la mtu ama liwe shamba au nyumba ya mtu na kuamua ni sheria ya ubabe...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Selelii kengele ya pili.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge zimesalia dakika tano tu kwa hiyo, hatuwezi kuendelea. Nimebakiza wachangiaji wafuatao kwa asubuhi, nina lengo la kukamilisha suala la uchangiaji kwa hoja hii ya Muswada wa Sheria ya Madini saa 6.00. Kwa hiyo, nitawaruhusu wafuatao, wa kwanza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, atafutiwa na Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na baada ya hapo ni Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na tutahitimisha na Mtaalam Ustadh John Shibuda.

Waheshimiwa Wabunge, kesho kutwa naanza kuitangaza leo kwa sababu ni muhimu sana, mhakikishe mmepokea kitabu hiki ndio kanuni za sheria ya matumizi ya fedha katika uchaguzi. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri, Sera Uratibu na Bunge amefanya jambo moja kwamba ameiweka hii iwe wazi kwa kujadili. Mtakumbuka sheria yenye imekuwa na matatizo hapa na pale ambayo yangeweza kabisa kurekebishwa ndani ya kanuni kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, semina hii tutakayoifanya ambayo tulikusudia ifanyike Dar es Saalam lakini tumeona itakuwa ni gharama ya bure. Jumamosi saa nne ukumbi wa Pius Msekwa tuzingatie hilo. Nasema hivi kwa sababu nimesoma hizi siruhusiwi kuchangia lakini nadhani ni zoezi zuri sana kwa sisi Wabunge wote. Tukiacha mapungufu yaliyomo yapite kwenye kanuni basi itakuwa hakuna tena wa kumlaumu, ilimradi tumepewa fursa hii ya kutoa mawazo yetu kuhusu kanuni hizi basi tuitumie kikamilifu. Tukifanya vizuri tunaweza kumaliza na wale wenye haraka sana, kuna watu huwa wana haraka sana ya kwenda Dar es Salaam basi hata kama tumemaliza saa 8.00 mtu unaweza ukaondoka. Lakini nasihi sana mahudhurio yetu yawe mazuri tupate mchango mzuri unaochambua kanuni hizi.

Waheshimiwa Wabunge basi kwa shughuli tulizopangiwa leo ndio tumefika mwisho. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi hapo kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.42 usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Ijumaa,  
Tarehe 23 Aprili, 2010 Saa Tatu Asubuhi*)